ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Hamad Masoud Hamad	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ole.
9.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa
11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa
12.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Gando
13.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Kuteuliwa.
14.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Jang'ombe

15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la Makunduchi
18.Mhe. Mansoor Yussuf Himidi	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Kiembesamaki
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu
22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka
23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
29.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
30. Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa na Rais
31.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe

32.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
33. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
34.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
35. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
36.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
37.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
38.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
42.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
43.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
44.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
45.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
46.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
47.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
48.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
49.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
50.Mhe. Marina Joel Thomas	Kateuliwa na Rais
51.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Jimbo la Mkwajuni
52.Mhe. Mgeni Hassan Juma	Nafasi za Wanawake
53.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma	Jimbo la Bumbwini
54.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile

55.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad Jimbo la Chambani

56.Mhe. Mohammed Said Mohammed Jimbo la Mpendae

57.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak Nafasi za Wanawake

58.Mhe. Mussa Ali Hassan Jimbo la Koani

59. Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali Jimbo la Uzini

60.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa Nafasi za Wanawake

61.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi Nafasi za Wanawake

62.Mhe. Nassor Salim Ali Jimbo la Rahaleo

63.Mhe. Omar Ali Shehe Jimbo la Chake-Chake

64.Mhe. Panya Ali Abdalla Nafasi za Wanawake

65.Mhe. Rashid Seif Suleiman Jimbo la Ziwani

66.Mhe. Raya Suleiman Hamad Nafasi za Wanawake

67.Mhe. Rufai Said Rufai Jimbo la Tumbe

68.Mhe. Saleh Nassor Juma Jimbo la Wawi

69.Mhe. Salim Abdalla Hamad Jimbo la Mtambwe

70.Mhe. Salma Mohammed Ali Nafasi za Wanawake

71.Mhe. Salma Mussa Bilali Nafasi za Wanawake

72.Mhe. Salmin Awadh Salmin Jimbo la Magomeni

73.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman Nafasi za Wanawake

74.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha Jimbo la Mwanakwerekwe

75.Mhe. Shawana Bukheti Hassan Jimbo la Dole

76.Mhe. Subeit Khamis Faki Jimbo la Micheweni

77.Mhe. Suleiman Hemed Khamis Jimbo la Konde

78.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
79.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
80.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake
Ndugu Yahya Khamis Hamad	**Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

Kikao cha Thalathini na Tisa – Tarehe 09 Agosti, 2012

(Kikao kilianza saa 3.00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika, (Pandu Ameir Kificho) alisoma dua

HOJA ZA SERIKALI

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo:

Mhe. Spika, kwa heshima kubwa naomba kuweka mezani Mswada wa Sheria ya Kuidhinisha Makisio na Matumizi ya Shilingi Bilioni Mia Sita na Arobaini na Nane, Mia Tisa na Arobaini na Tatu Milioni. Mia Saba na Tisini na Nane Elfu Kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha unaoishia Siku ya Tarehe Thalathini Juni, Mwaka wa Elfu Mbili na Kumi na Tatu na Kuruhusu Utoaji na Uhaulishaji wa Fedha hizo Pamoja na Mambo yanayohusiana na Hayo. Kusomwa kwa mara ya Kwanza.

Naomba kuwasilisha.

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013 –
Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Spika: Waheshimiwa wajumbe majadiliano yanaendelea lakini kabla ya kuendelea majadiliano naomba tuelewe tu kwamba shughuli hii kufatana na ratiba ya shughuli zetu tunalazimika kuimaliza leo. Hivyo niombe waheshimiwa wajumbe wasaidie kiti ili tumudu kuimaliza shughuli hii na kuacha nafasi kwa baadhi ya shughuli zilizobaki zimalizike kesho na hatimae kumuomba Mhe. Makamo wa Pili wa Rais Kiongozi wa Shughuli za Serikali Barazani aweze kuja kutoa hotuba ya kufunga mkutano wetu wa nane.

Kwa hivyo niwaombe waheshimiwa wajumbe tujitahidi wale ambao baadhi watapata nafasi ya kuchangia twende kwenye hoja moja kwa moja, tupange *points* zetu vizuri ili hatimae tutumie muda mfupi lakini mchango wa kutosha kusaidia hotuba hii ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara ya Fedha Uchumi na Mipango ya Maendeleo.

Baada ya hayo basi waheshimiwa wajumbe ukumbi wangu umekuwa mtupu kidogo nataka nimwite mtu ambaye yupo.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Ahsante sana Mhe Spika, nataka nikushukuru kunipa nafasi hii na mimi nikaanza kuzungumza machache kabisa katika hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais Fedha Uchumi na Mipango ya Maendeleo.

Mhe. Spika, mimi kwanza nataka nianze kwa kumpongeza sana Mhe. Waziri wa Nchi, Fedha Uchumi Mipango ya Maendeleo kwanza ni mtu wa mwanzo au waziri wa mwanzo kuanza kutuelewa hoja zetu tunakusudia nini. Mhe. Spika, katika bajeti ya mwaka jana tulikuwa wakali sana na miongoni wa waliosimama hapa tukazungumza kwamba Serikali pesa inazo lakini bado haijataka kuzisimamia vizuri. Na Mhe. Waziri alituahidi kwamba jamani nisaidieni nitafutieni, nyie wenzangu mko siku nyingi, tumejitahidi tumetumia uzoefu wetu tumeshirikiana na wenzetu Mhe. Waziri nadhani katika hotuba yake safari hii ametuthibitishia yeye mwenyewe kwamba kweli michango yetu imeweza kusaidia kuokoa fedha nyingi za wananchi na sasa hivi zinalengwa katika eneo maalum ambalo la kuondoa kero za wananchi. Mhe. Waziri tunakushukuru na umetupa changamoto kubwa na bado tutaendelea kukusaidia kuhakikisha kwamba kila ambalo tunahisi hapa Serikali yetu tuishauri vizuri basi tutaweza kufanya kazi hii.

Mhe. Spika, nataka nianze katika PBZ Mhe. Spika, kwanza nataka niwapongeze wenzetu Benki ya watu wa Zanzibar kwa kazi nzuri wanayoifanya lakini Mhe. Spika, hapa sasa hivi inabidi Benki yetu hii tuiangalie kwa vizuri, na ninamuomba sana Mhe. Waziri sasa hivi aangalie jicho lake Benki ya Watu wa Zanzibar. Mhe. Spika,

Benki yetu ilikuwa inakaribia kufilisika tunamshukuru Rais wetu wa Awamu ya Sita Dr. Karume alisimama kidete na akasema kwamba serikali sasa hivi mwisho kukopa Benki ya Watu wa Zanzibar. Serikali kila ilichokopa Benki iweze kurejesha Mhe. Rais alilisimamia hilo na mpaka ikafika pahala Benki ya Watu wa Zanzibar ilikuwa katika sakaral mauti lakini matokezeo yake sasa hivi ina-*survive* katika hali ya kwamba anaweza kuingia katika ushindani wa aina yoyote.

Mhe. Spika, lakini katika miaka ya hivi karibuni kumeanza kujitokeza matatizo na waswahili wanasema mgema akisifiwa tembo hulitia maji. Mhe. Spika, Benki yetu inaanza kuibiwa nakumbuka kama sikosei ilikuwa mwaka 2009 Benki hii kuliibiwa pesa karibu dola laki nne na thamanini. Fedha hizi baada ya kuibiwa tunashukuru benki walichukuwa hatua wakawatafuta wale waliowadhania ambao wanahisi wameingia katika hatia wakawekwa ndani, lakini kitu ambacho cha kushangaza hakuna hukumu iliyotolewa na watu wale sasa hivi wote wako nje. Sasa tunajiuliza wanoiba ndizi, wanoiba kuku miaka mitatu lakini wanaoiba mamilioni ya mapesa wanatembea kifua mbele.

Sasa Mhe. Spika, mimi nataka niseme hii benki itafilisika kwa sababu kama wale wa mwanzo unasadikiwa kuwa ulitokezea wizi hakuna mtu aliyekamatwa sasa Waziri akija anambie pesa hazikuibiwa mwaka 2009 na kama ziliibiwa je wale walioiba wamechukuliwa hatua gani. Maana tulisikia kuna mpaka wafanyakazi wengine wakakimbia, wengine wafanyabiashara lakini kuna baadhi ya wafanyabiashara mpaka leo fedha zao zimezuia hukumu haikutoka na wale wameachiwa kesi imefutwa kwa hivyo kama kesi imefutwa kama mtu ana haki yake arudishiwe lakini vile vile kama kesi haikufutwa, kesi tumefikia hatua gani mpaka sasa hivi. Lakini ninavyojua mimi kesi ilifutwa na ndio maana nikaamua kuisema hapa kama kesi bado iko mahakamani nisingesema hivi lakini nitakuja kutaka jawabu. Lakini Mhe. Spika, baada ya ndugu zetu hawa kuanza ku-*beep* wakaona tumepokea sasa hivi wameanza kutupigia.

Sasa hivi kuna wizi mwengine umefanyika tena Benki ya Watu wa Zanzibar na serikali imekaa kimya na ninaamini kwa kuwa wale wa mwanzo waliachiwa na hawa wapili wataachiwa. Mhe. Spika, kuna taarifa za ndani kabisa kuna wafanyakazi wa Benki ya Watu wa Zanzibar wameibia benki kuna fedha tunaambiwa aidha za wastaafu au za viinua mgongo, Mhe. Waziri *at least* aje atwambie kadhia hii na taarifa tuliyokuwa nayo hawa wanaambiwa waandike barua wenyewe ya kuacha kazi. Sasa mtu keshaiba halafu unamwambia aandike barua ya kuacha kazi, mtu akiandika barua ya kuacha kazi of course ina maana na haki zake nyengine utamlipa.

Sasa Mhe. Spika, hii benki sasa badala ilikuwa ikifanya vizuri sasa hivi benki kuna watu wanaihujumu kwa makusudi. Sasa mimi nadhani Mhe. Waziri hili asilikubali na ninafikiri, mimi nataka tujifunze, mawaziri tunakusulubuni kwa makosa ya watendaji wenu. Sasa Mhe. Waziri kama hili utashindwa kulisimamia, sisi pamoja na urafiki wetu lakini kwa kweli tutashindwa kukustamilia. Sasa Mhe. Waziri naomba sana uwe mkali kama unavyotaka kwamba fedha ya umma sasa hivi ibakie ili iingie katika mfuko wako itumike kwa maslahi ya wananchi, basi na hawa naomba uwasimamie. Lakini hili nitakuja kuomba maelezo ya kina kabisa. Mhe. Spika, pamoja na yote lakini bado Benki ya Watu wa Zanzibar inafanya kazi vizuri, wafanyabiashara wanaridhika wanakwenda wakitaka mahitaji na vile vile wananchi wetu wanaweze kufaidika vile vile.

Jengine Mhe. Spika, ninakuja kwenye Taasisi yetu nyengine ya kukusanya fedha TRA. Mhe. Spika, tunawapongeza sana TRA wanafanya kazi nzuri pamoja na lawama ndogo ndogo, kila ukipata lawama basi unafanya kazi vizuri, jitahidini na sisi tuko pamoja na nyinyi. Lakini bado tunaomba kwa yale mambo madogo madogo hasa bandarini, mambo ya kufumbia fumbia macho baadhi ya kodi tunawaomba wenzetu haya muanze kuyarekebisha.

Lakini jengine katika TRA Mhe. Spika, mimi nataka nizungumze kwa sababu TRA ni chombo cha muungano sasa kuna tatizo, kadhia kama tulivyoizungumza kwa wale wenzetu wafanyabiashara ya magari magari yao yaliyozuiliwa pale bandarini Dar es Salaam tayari tumezungumza nao na tumewambia kwamba kwa sasa hivi kwa kuwa una bajeti wasikushughulishe, wakuachie umalize bajeti yako zile document watakuletea ili uhakikishe na Mheshimiwa nataka nikuthibitishie, wafanyabiashara hawa *document* zao tumeziona wamelipa ushuru Zanzibar, wamelipa tena ushuru mwengine wa difference pale Dar es Salaam bandarini lakini bado magari yao yamezuiwa mpaka leo hayajaweza kutolewa.

Sasa hapa Mhe. Spika, naomba sana labda Mhe. Waziri wa Fedha mwenyewe kama ataliweza hili na kama hili litakuwa zito kwake atusaidie kwa Mhe. Makamo wa Pili wa Rais, kwa sababu kuna hatari wafanyabiashara wa Zanzibar wenye magari wengi wao wakaja wakafilisika. Kwa nini nikasema hivyo, Mheshimiwa kuna

wafanyabiashara ambao walolipa ushuru gari hapa, mfano mtu hapa kalipa milioni nne na nusus, kufika Dar es Salaam bandarini anaambiwa alipe tena milioni tatu na nusu. Kwa hivyo pia kaamua kulipa ina maana ukifanya total milioni nane keshalipa. Lakini baadae anafika getini anaambiwa gari inazuiwa tena anaambiwa kuna kitu kinaitwa iko lugha yao wanaita inazuiwa gari inarudi tena, anaambiwa mtu alipe tena milioni nane. Sasa Mhe. Spika, wananchi wetu hawa wanaofanya biashara hii ya magari wanasema sisi wakati hapa tulilipa nne na nusu, Bara tumelipa tatu na nusu, halafu baadae tunaambiwa tulipe nane Mheshimiwa gari zitatushinda kuzitoa Dar es Salaam. Kwa hivyo tunaomba gari zetu zirudishwe Zanzibar.

Sasa wameomba gari zao warejeshewe Zanzibar kule bandari ya Dar es Salaam hawataki. Sasa Mhe. Spika, huu ndio unyanyasaji wananchi wetu ili wasiweze kujitegemea katika biashara. Sasa hapa nilikuwa naomba Mhe. Waziri kama hili ataweza kulibeba kwa wale ambao wanashindwa kuzipeleka kule basi waruhusiwe wageuze wazipakie tena warudi haidhuru watakuja kupandia wenyewe hizo gari, maana hawatakuwa na mtu wa kumuuzia. Sasa Mhe. Spika, hili nilikuwa ninamuomba sana Mhe. Waziri, kama ataliweza yeye basi atujibu, kama haliwezi basi Makamo wa Pili wa Rais kwa sababu hii ni kero alichukuwe tunataka tupate kauli hasa ili wenzetu hawa wajue wanaishi vipi katika kuendeleza biashara zao.

Mhe. Spika, tumewapa kazi kubwa ya kutulelea maslahi ya wazee wetu baada ya kustaafu, kuna kadhia moja ambayo tumepata taarifa nilikuwa nahisi na hii tuiseme. Bado katika sheria zetu wafanyakazi wanasema tofauti na zile sheria za wenzetu mfuko kule Bara. Na tulikuwa tunajua mfuko huu baada ya kuanzishwa ulikuwa unafanya study kuangalia ni eneo gani labda wataweza kusaidia ambapo ili mfuko usije ukafilisika kuna wafanyakazi wetu hawa wengine hasa wanaofanyakazi katika makampuni haya ya binafsi wanaoachishwa kazi ovyo, sasa utakuta fedha zao zinakaa muda mrefu na anaambiwa mpaka afike umri wa kustaafu ndio aje apate fedha zile. Wanasema sasa hivi mtu anaangalia *value for money* fedha yake bora wengine wanasema kama anapostaafu kazi kama ameshindwa kupata kazi sehemu nyengine apewe ili apate kuania maisha. Maana yake kama mtu alikuwa anafanya kazi alikuwa anakatwa mfuko wa hifadhi ya jamii, sasa hivi yuko mtaani hana kazi hakuna benki ya kwenda kukopa, ile akiba yake apewe ili akanunulie machungwa akauze. Sasa hili nilikuwa naomba Mhe. Waziri naamini jawabu yake atakuwa nayo akija anaweza akaja akatusaidia.

Mhe. Spika, kuna jambo moja nilikuwa nataka niligusie, ingawa halimgusi moja kwa moja Waziri lakini amelitaja katika kitabu chake katika suala zima la kuokoa fedha zile ambazo tuloangalia katika maeneo mbali mbali, kwa ajili ya kununua meli. Mhe. Kwanza mimi ninampongeza Mhe. Rais kwa ujasiri wake wa kutoa amri wa kutoa amri na amri ile waziri wetu ameipokea kwa mikono miwili na ameshaanza kuifanyia kazi na taarifa yake imo humu. Lakini bado ninarejea Mhe. Spika, meli hii tukishainunua tunaikabidhi Shirika la Meli, tuangalie Shirika la Meli lilikuwa na meli ngapi, wamezalisha ngapi, Mhe. Spika, tutawanunulia meli kila siku hebu tuiangalie na management yenyewe ya Shirika la Meli wana uwezo wa kuongoza hili Shirika? Mhe. Spjika, isije kuwa huku kwa sababu hizi fedha tulizozikamua tunaamini safari hii wizara watafanyakazi katika mazingira magumu. Kwa sababu leo tunaweza sisi tukenda katika kamati, ukaambiwa mzee leo mtakunywa maji tu japa, potelea mbali ndio tumeamua kufunga mkanda miezi kumi na nane tumeshakubali, lakini hizi meli tunazowapa leo hebu tuulizeni hawa watu waliopo katika Shirika leo wapo mwaka wa ngapi faida gani wameleta. Mimi nadhani Mheshimiwa naomba tuna imani sana na serikali, tuna imani na waziri wetu tunaomba fedha utakayoinunulia meli utakapoipeleka utizame na management yake iko vipi.

Mheshimiwa haiwezekani kuna Shirika la Biashara ya Magari juzi tushalitia kitanzi, hawa Shirika halionekani matunda yake bado tunaendelea kununua meli. Mimi naomba sana *management* tuiangalie na lazima tuwawekee malengo kila baada ya muda wahakikishe na hizi fedha kwa sababu zako wewe unatoa uhakikishe kwamba unaletewa return, tujuwe wanazalisha nini na vile vile wakupe mpango wao wa baadae, baada ya miaka mingapi watakuwa na uwezo wa kununua meli nyengine. Hatutaki kuwapa watu watumie wakaue tu. Mheshimiwa sasa hivi hii nchi tunataka ijiendeshe, tushachoka tena kila siku tunarudi humo kwa humo.

Lakini jengine Mhe. Spika, hili natoa angalizi serikali sana itajitahidi kununua meli mbili kwa sababu wananchi wana mahitaji mengi, lakini je wafanyabiashara bado wataendelea kuleta usafiri wa vyombo vya baharini, bado naomba Mhe. Spika, serikali yetu iweze kuwa na supervision hasa katika masuala ya usafiri wa meli, hata hizo meli zetu zitakuja kustahiki vile vile kuja kukaguliwa.

Mhe. Spika, nataka nizungumzie ZIPA kidogo, Mhe. Spika, mimi nataka niwapongeze sana ZIPA na ninaomba ZIPA waendelee na msimamo wao huo huo, kuna watu wanawababaisha kwa tama zao. ZIPA wakeshatoa kibali

kwa mwekezaji wakati mwengine kuna maeneo ambayo Muekezaji ameshapewa kibali na ZIPA kujenga baadae kuna taasisi nyengine vibali vile wanawanyang'anya yale maeneo bila ya kuwasiliana na ZIPA halafu wanawalazimisha ZIPA kuweza kutoa vibali vyengine. Mimi ninawapongeza sana waendelee kuwa na msimamo wao kufata sheria za nchi. Kwa sababu wawekezaji wanapokuja wakishapata kibali cha ZIPA tayari ina maana wamesharuhusiwa kuekeza ndani ya nchi.

Sasa Mhe. Spika, mimi kwa upande wa ZIPA kwa kuwa kuna mambo ambayo tumeshayatolea maamuzi hicho kipindi cha nyuma tutakuja kwenda kufanya kazi huko, lakini nataka nizungumze na hawa wawekezaji ambao wanaoingia katika upande wa maeneo huru ya kiuchumi. Mheshimiwa juzi nilizungumza katika wauzaji wa Mitumba hapa Savana maeneo ya Amani Viwanda VidogoVidogo. Mheshimiwa nilizungumza siku ile kwamba wale wanaleta mitumba mingi iko katika law quality. Lakini vile vile Mhe. Spika, wana bei yao inakuwa haitulii wamekuwa kama na wao walanguzi, leo wanauza bei hii kesho asubuhi wana kuja bei hii vijana wetu wanashindwa kujua. Kwa kuwa yule ni muekezaji ambaye ana-import moja kwa moja bila shaka akishalipa ushuru na kila kitu anajua mimi mzigo wangu natakiwa niuze kiasi gani.

Vijana wangu wamenisikia jana wengine wamenifata, akanambia Mheshimiwa nyinyi mmezungumza kuhusu uuzaji wa mitumba tu, lakini kuna kadhia ya unyanyasaji ndani ya kampuni ile. Mheshimiwa kampuni vijana wanafanya kazi kuanzia asubuhi saa moja mpaka saa kumi, hawana mapumziko. Hii ni kuvunja hata hizo haki za ILO, Mhe. Spika, sisi tumewahi kwenda Uingereza umetupeleka sisi wengine, tumekwenda tumeonana na vijana wetu wa Kizanzibari wanapiga box kweli kweli kule, lakini wanafanya kazi ikifika saa sita wanapumzika wanakwenda wanakula halafu wanarudi. Wenzetu pale hakuna kula hakuna nini, leo maji wanasema wanakwenda kunywa chooni sasa hawa watu imekuwa kama wamefungwa.

Mhe. Waziri wa Biashara amewahi kwenda vijana wamenambia, lakini alipokwenda kenda kuzungumza na wakubwa hakupata nafasi ya kuzungumza na wale wafanyakazi. Kuna kadhia kubwa kuna unyanyasaji mkubwa na wao kule wanaambiwa hamruhusiwi kuzungumza jambo lolote ndani ya kiwanda nje. Sasa wale mpaka wafe ndio waje waseme. Vijana wetu wamekuja wametwambia kwa kweli hii ni hatari na katika mpaka mkataba wao wanaambiwa hakuna ruhusa ya kuzungumza jambo lolote linalohusu humu ndani ya kazi. Kwa kweli ndio haki ya binaadamu hiyo.

Mimi naomba Mhe.Waziri wa Kazi, Mhe. Waziri wa Biashara na Mhe. Waziri wa Fedha ambao wewe ndio mwenye uwekezaji tunaomba hawa wawekezaji mkae nao wahakikishe kwanza muangalie utaratibu wao wa kazi, wanafanyisha kazi watu vipi lakini vile vile na Wizara ya Afya vile vile wale vijana hawakaguliwi afya zao ipasavyo, watu wa Wizara ya Afya tunaambiwa wakwenda pale, wanaonana na mabosi wanakunywa soda na sambusa wanarudi sasa wamekwenda kukagua haki za watu au wamekwenda kunywa soda na kurudi. Mheshimiwa wale wanafanya kazi ya ku-*sort* mitumba, mitumba tunajua imeshavaliwa kuna madawa kuna nini, wale vijana wanahitaji wapimwe afya zao kila baada ya miezi sita au miezi mitatu, ili kuhakikisha usalama wa watu wale. Mhe. Spika, haiwezekani mtu anafanya kazi masaa kumi kasimama bila ya mapumziko hata ya kwenda kupata lunch au kupata kitu chengine.

Mhes Spika, nadhani leo sitaki niseme mambo mengi, maana yake kimsingi Waziri wa Fedha ametufurahisha sana kwa jinsi anavyokubali hoja zetu na mimi naunga mkono hoja hizi lakini nitakuja kupata maelezo zaidi nitapopata maelezo ya PBZ.

Mhe. Spika, ninakushukuru. Ahsante.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Spika, ninakushukuru na mimi asubuhi hii ya leo kunipa fursa na mimi kuchangia hotuba hii ya kaka yetu Waziri wa Fedha na Uchumi wa serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Spika, na mimi sitakuwa na mengi kama alivyozungumza Mhe. Hamza nilitaka niingie kwenye *Hansard* ya kuchangia hotuba hii ya Mhe. Waziri. Kwanza kabisa Mhe. Spika, nimpongeze sana Mhe. Waziri wa Fedha na Uchumi kwa uwasilishaji wake, pia kwa kuwa msikivu kabisa kuonesha mfano wa kuwa msikivu kwa michangio ya wajumbe walioitoa concern zao na akakubali. Kwa hivyo nimpongeze sana kwa ajili ya kukubali na kutuahidi kama atapunguza vile vifungu vya fedha na tutaziona na kweli katuletea tumeziona. Kuna vifungu hivi 19 ambavyo kuwa vimepunguzwa, kwa hivyo nimpongeze sana.

Suala jengine Mhe. Spika, pia nimpongeze Mhe. Waziri kuona kwamba kuna baadhi ya sheria zinazotahiki kufanyiwa marekebisho kuhusu mambo ambayo yanaingiliana ingiliana kwa mfano kama suala la mambo ya nishati kuona kwamba ZRB suala la mafuta wao wasimamie kuhusu kodi za mafuta tu, lakini usimamizi wa bei na kusimamia mafuta wakaachiwa Idara ya Nishati yenyewe. Kwa hivyo nimpongeze sana na hili kuona kama haya ni mambo ambayo yanaingiliana ingiliana akaweka sawa.

Suala jengine nimuombe tu basi Mhe. Waziri kwamba kuna suala hili la leseni nalo pia linaingiliana kwa sababu ZRB wanasimamia leseni au wanatoa leseni lakini kumbe huko nyuma kuna chombo cha Mamlaka ya Usafiri na Nchi kavu kwa hivyo wao ndio wanaostahiki kutoa na kusimamia hizi leseni kwa hivyo na hili aone kwamba kuna haja ya kuachiwa Mamlaka ya Usafiri wan chi kavu watu wa Idara ya leseni ili wasimamie mambo haya. Kwa sababu mambo yakiingiliana huku na huku yanakuwa hayaleti picha nzuri.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo nataka nilizungumzie ni suala la ugavi wa mapato kutoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Muungano. Kwa kweli Mhe. Spika, mimi suala hili kidogo naona linaniumiza kichwa kwa upande wangu mimi kuwa Zanzibar tokea tumeanza kuingia kwenye muungano huu gawanyo letu la mapato 4.5 kwa kweli hili mimi linaniumia kweli kweli. Kwa sababu sijui kigezo gani kilitumika mpaka Zanzibar ikawa ipate gawio hilo. Mimi naona kama Zanzibar inanyimwa haki yake, kwa sababu tangu tulipoanza watu ni mia mbili gawio ni hili mpaka sasa hivi tumeshafika milini moja na laki tano gawio ni hili. Yaani kiwango chetu hiki hakipandi ni hiki hiki hakipandi mimi sijui vigezo gani vimetumika.

Kwa hivyo ninamuomba Mhe. Waziri kidogo mimi anielimishe hapo kwa sababu ninawasiwasi nacho hili kwa nini sisi tuwe tunapata gawio hili haliondoki. Ukija kwenye mabenki hisa ya benki kuu ya Zanzibar ambayo tuna hisa zetu ingawa zina, kataliwa gawio ni hili. Ukija mapato ya fedha zinazoingia kwa wafadhili kuhusu GBS gawio ni hili. Kwa hivyo Mhe. Waziri namba hapa anielimishe na anielekeze kidogo kwa mimi naona kama sikaliwi sawa.

Suala jengine Mhe. Spika, nilalamike tu kwamba naona kodi pamoja na kwamba tumesema tutapandisha kodi lakini naona kodi imepanda zaidi kuhusu mambo ya kupasisha magari. Leo sasa hivi kupasisha vespa inafika zaidi ya shilingi sitini elfu, magari hayatajiki kwa hivyo Mheshimiwa na hili naomba kidogo ee pamoja na kusema tutapandisha kodi lakini aone kwamba wananchi wetu hali yetu kama tunavyoiona wanyonge sana na hili linatakiwa lifikiriwe. Kwa hivyo na Mhe. Waziri na hili aone kama kweli tumekubali kukodisha kodi hasa kodi hizi za ndani aone kama kidogo watu wetu hali zao dhulihali kwa hivyo kidogo na hili anatakiwa aliangalie.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo nataka nizungumze ni suala la TRA hili limezungumzwa sana na wajumbe wengi na mimi nalizungumza. Kwa sababu na mimi ni shahidi kuona kama kwa nini wafanyabiashara wetu wa Zanzibar walipishwe mara mbili hivi kuna nini? Kwa hivyo hili mimi ninalitilia mashaka kwamba hili ni mpango maalum ili kuidumaza Zanzibar, wafanyabiashara wanaokuja Zanzibar kufanya biashara ili waone kwamba hawaji hapa na wanafika kule moja kwa moja. Kwa sababu gani mimi shahidi nimeona na mimi mtu keshalipa gari yake kodi zote hapa keshalipa kila kinachostahiki kwa TRA lakini kufika kule Dar es Salaam anaambiwa alipe tena milioni kumi na tano na wakati hapa keshalipa kila kitu. Kwa hivyo hili Mheshimiwa nalo bado hili suala ni sugu na halijapata ufumbuzi.

Kwa sababu watendaji wa kule ukenda kuzungumza nao wanakwambia kwa kupiga kelele Bungeni na kupiga kelele katika Baraza la Wawakilishi, mtamaliza kupiga kelele zenu, kwa sababu mnapiga kelele kule tu huku hatujapewa maandishi siye kodi ichukuliwe upande mmoja. Kwa hivyo kama hakuna na vitabu vyetu vina maandishi ya kuwa mtu akilipa na huku aje achukuwe tena mtapiga kelele mpaka mtamaliza. Kwa hivyo hili nalo naomba lipatiwe ufumbuzi wa kudumu, kwa sababu tunakuja kuambiwa limeshapatiwa ufumbuzi tukiondoka suala linaendelea vile vile. Kwa hili linaumiza kweli kweli na wafanyabiashara wetu wananun'gunika wanaumia kweli kweli na sisi wenyewe tunaumia.

Kwa hivyo hili nalo Mhe. Waziri linatakiwa ufumbuzi wa kudumu kwa sababu ni suala sugu, limekuwa kama donda ndugu, lakini mimi nasema hili ni mpango maalum wa kuidumaza Zanzibar kibiashara ili wafanyabiashara wende wakalipie kule ili sisi huku tudumae. Kwa hiyo Mhe. Waziri hili ni uti wa mgongo wa Zanzibar, mapato ikiwa hayapatikani wafanyabiashara wanatukimbia kwa kulipa mara mbili halatu sisi tutabakia kama tunavyobakia. Naomba Mhe. Waziri hili mlikalie kikao cha hali ya juu ili kupata maamuzi kwa sababu lishakuwa suala sugu.

Suala jengine ninalotaka kuzungumza ni kuhusu mabenki. Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri na hili nalo aone kuwa riba za mabenki ni kubwa sana na ndio maana wafanyabiashara wanapungua kukopa kwa sababu ya riba kuwa ni kubwa sana. Riba ni Benki ya Watu wa Zanzibar tu (*PBZ*), lakini benki nyengine zote afadhali. Kwa hivyo, kama benki kuu ndio inayosimamia na hili suala la riba tunaomba lisimamiwe vizuri kwa sababu riba imezidi sana kwenye mabenki. Watu ndio maana wanapungua kule kukopa benki kwa sababu ya riba kuwa kubwa sana.

Mhe. Spika, suala jengine kama nilivyosema kuwa sina mchango mkubwa isipokuwa naomba Mhe. Waziri anipatie ufafanuzi kuhusu hayo niliyomuuliza. Pia nampongeza sana na kuunga mkono hotuba hii ya bajeti na nimuombe aendelee kusimamia mapato ya kodi zinazopatikana za serikali yetu ili tuweze kuendelea zaidi na tupunguze utegemezi wa bajeti. Kwa sababu kodi kama zitasimamiwa vizuri basi tutapunguza ule utegemezi wa bajeti zetu. Mhe. Spika, naunga mkono.

Mhe. Ali Salum Haji: Ahsante Mhe. Spika, na mimi nichukue fursa hii nikushukuru kwa kupata nafasi hii asubuhi ya leo. Lakini pia nimshukuru Mhe. Waziri kwa uwasilishaji wake wa hotuba hii yenye mwelekeo na kutoa matumaini kwa wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Spika, mimi kwanza nataka nianze kwa pongezi kwa Mhe. Waziri, kama wenzangu walivyotangulia kusema kuwa tumpongeze sana Mhe. Waziri wa Fedha kwa umahiri wake, usikivu wake na upeo aliokuwanao na *experience* iliyojijenga kutokana na kufanya kazi katika maeneo mbali mbali kwenye nchi yetu ya Tanzania na Zanzibar kwa ujumla.

Mhe. Spika, tulikuwa tukipiga kelele sana hapa katika kuzungumzia masuala ya mafungu jinsi yalivyokuwa yamejitokeza na mashaka tuliyokuwanayo. Mhe. Waziri ametuahidi kwamba hili atalibeba na atalifanyia kazi na ninashukuru kwa dhati kabisa kwamba kazi imeonekana na wananchi wa Zanzibar wameanza kujenga matumaini kwa serikali yao. Mhe. Spika, kuweza kuokoa shilingi 17,166,560,250/- ni kitendo ambacho kwa kweli sisi kimetujengea matumaini. Lakini pamoja na pongezi hizo nimuombe Mhe. Waziri huu usiwe mwanzo au mwisho wa kuchunga pesa za serikali, serikali hii bado ina matatizo mengi na kwa kweli tunahitaji viongozi mahiri katika kuona pesa za wananchi zinatumika kwa umakini kabisa.

Mhe. Rais wetu alijipiga kifua kwa kutoa maamuzi mazito na magumu ya kumtaka waziri akanunue meli na akiamini kwamba fedha zipo na waziri akachukua hilo kwa kuchukua kadhia hiyo. Lakini niseme kwamba nimtake tena Mhe. Waziri wa Fedha aendelee kujenga mawasiliano mazuri na Mhe. Rais mwakani tupige kifua katika sekta nyengine, bado nchi yetu inakabiliwa na majanga mengi ukiachilia janga la meli lakini bado tuna janga la maji. Kelele zimekuwa kubwa, mashaka yamekuwa mengi, basi tuna haja ya mwakani kuangalia kitengo chengine ili kuweza kuondosha kadhia hii.

Mhe. Spika, pia tuna janga la umeme tumechoka kutumia umeme wa Tanzania Bara ambao unarejesha nyuma maisha ya Wazanzibari, kodi zimekuwa kubwa, mishahara yetu bado duni, Mzanzibari anapolipa umeme unamkuta kwamba hajabakiwa na kitu, basi maamuzi magumu kama haya ya kunusuru fedha kwa kupunguza vifungu ambavyo havistahiki au havina umuhimu kuweza kununua meli basi mwakani tukatafute umeme wetu ili Zanzibar iweze kujitegemea katika suala la umeme.

Mhe. Spika, baada ya shukurani hizo mimi nina mambo ya kuzungumza kidogo kidogo tu na ni maombi, nimuombe Mhe. Waziri kwamba mara nyingi tumekuwa tunajiwekea malengo ya makusanyo katika taasisi zetu zinazokusanya pesa. Nimuombe Mhe. Waziri kuna haja ya kufanya utafiti wa kutosha katika vianzio vyetu vya mapato. Wasiwasi wangu kwamba yale makadirio tunayowapa wakati mwengine yanakuwa madogo na watu wanayavuka kwa wepesi na wakishayavuka tu basi inakuwa zile jitihada za kukusanya zinapungua wakati mwengine hata matumizi yanakuwa hayaeleweki. Sasa nimuombe Mhe. Waziri tufanye utafiti wa kutosha katika taasisi zinazokusanya mapato, nina wasi wasi mnawapa makadirio madogo na uwezo wa kukusanya unakuwa ni mkubwa na uwezo upo. Hilo ndio ombi langu la kwanza.

Jengine Mhe. Spika, niende katika ngazi ya wahasibu. Nimuombe Mhe. Waziri ajitahidi kulitizama hili, tuna mashaka kwamba baadhi ya wahasibu wanakaa muda mrefu katika taasisi za serikali bila ya kuhamishwa kama utaratibu unavyotakiwa na hili linapelekea kujenga mazowea na wale watendaji wa maeneo yale husika, wanapojenga mazowea inakuwa ni suala la ubadhirifu inakuwa ni jepesi katika kulifanya. Sasa niombe kwamba hiki

ni kitengo nyeti na ni kitengo ambacho kina utaratibu wake ule muda wa *rotation* unapofika basi ufanyike kwa mujibu wa utaratibu Mhe. Spika.

Nikitoka hapo Mhe. Spika, nilikuwa nina ombi jengine kwa Mhe. Waziri, nimuombe basi wakati tuliokuwanao sasa hivi watu wamehamasika, watu wamekuwa na muwamko nimuombe Mhe. Waziri aandae taratibu za kuweza kuwahamasisha wawekezaji. Kuna haja sasa hivi ya kuongeza mabenki tunahitaji mabenki ya kisekta. Sasa hivi wananchi wengi wanahitaji mikopo lakini benki zetu zimekuwa na riba kubwa, sasa nafikiri kama tutakuwa tuna benki za wakulima, benki za wafanyabishara, benki za kinamama na benki za vijana nafikiri hili kidogo linaweza kusaidia wananchi wetu kuweza kuondokana na umasikini. Sasa hili nalo nimuombe Mhe. Waziri ajaribu kutafuta njia mbadala ya kuweza kuhamasisha wawekezaji wetu ili kuweza kusaidia wananchi wetu kuweza kuondokana na umasikini.

Nikiendelea Mhe. Spika, nilikuwa naomba niingie katika maeneo ya Mkaguzi wetu wa Mahesabu. Mhe. Spika, hii sekta ni nyeti na niombe sana hii taasisi basi ijitahidi kufanya kazi zake kwa ufanisi zaidi. Mhe. Spika, hatupendelei kabisa kuweza kuona madudu ya ubadhirifu kuwa mara nyingi yanaibuliwa na Waheshimiwa kupitia Kamati Teule. Ni vyema basi *CAG* ikafanya kazi ili sisi tusimamie zile kazi za madudu ambayo yameibuliwa na *CAG*. Hapa niombe tu kwamba wajitahidi kufanya kazi zao kwa ufanisi zaidi ili kutupa wepesi sisi wasimamizi wa fedha za serikali kuweza kutoa mashirikiano yaliyokuwa mazuri zaidi.

Mhe. Spika, nikitoka hapo nina mashaka kidogo kwa baadhi ya watendaji wa Wizara ya Fedha kwamba wamekuwa na tabia ambazo sio nzuri za kuwalazimisha wakaguzi wao wa ndani kufuata matakwa wanayotaka wao sio matakwa ya serikali yetu. Hili Mhe. Spika, linapelekea kurejesha nyuma utendaji wa kazi zetu na upotevu wa pesa. Sasa Mhe. Spika, nimuombe Mhe. Waziri ajaribu kuliangalia hili zaidi baadhi ya wakaguzi wetu wa ndani wanafanya kazi kwa hali ya kufuata mabosi wao na kinachoonekana ni kwamba mtu asipomridhia bosi wake basi anakuwa mara nyingi anapata vitisho vya kuondoshwa katika ile nafasi na kupelekwa sehemu nyengine. Sasa hii si tabia nzuri nafikiri tabia nzuri tuliyojijengea ni watu kufuata taratibu za sheria kwa mujibu zilivyowekwa kwa kuweza kunusuru fedha za walalahoi.

Mhe. Spika, nikitoka hapo naomba niendelee katika suala la yadi zetu zinazouza magari. Niombe kwa dhati kabisa Mhe. Waziri ajaribu kuliangalia hili kupitia chombo chetu cha *TRA*, tuna mashaka labda taratibu zao haziko vizuri juu ya magari yetu yanayouzwa ambayo mara nyingi unayakuta hayana namba sijui taratibu zikoje, magari haya yamekuwa yanatembea pasipokuwa na nambari nataka anisaidie hizi taratibu zikoje na zinasemaje. Mara nyingi gari hizi huwa zinatolewa usiku usiku na sasa hivi imefikia pahala magari haya yanasababisha ajali na yanatuulia wananchi wetu na tabu kulitambua.

Mhe. Spika, ukiachilia hilo la kulitambua, wakati mwengine pia wanachukua nambari za bandia. Kuna gari ambazo tayari zishapata namba inachukuliwa namba hiyo ambayo tayari imeshakuwa *register* inatiwa katika gari nyengine gari ile ikipata ajali ikija ikikamatwa au namba ikija kudondoka unakuta kuwa ni tofauti, utakuta namba ya *ciao* imetumiwa kwenye gari au namba ya pikipiki. Sasa hili ni tatizo Mhe. Spika, nimuombe Mhe. Waziri atusaidie hawa *TRA* jinsi wanavyofanya taratibu zao katika kuhakikisha zile gari ambazo ziko ndani ya yadi kujua kwamba kam azinastahiki kutiwa namba basi zote zitiwe namba na kama hazistahiki basi tuondoshe huu usumbufu ambao umeanza kujitokeza Mhe. Spika.

Lakini Mhe. Spika, niombe kumalizia tu katika eneo la Viwanja vya Kufurahishia Watoto. Mhe. Rais wetu wa Kwanza, Abeid Amani Karume kwa nia njema tu alianzisha mambo mengi, lakini tumekuwa na masikitiko kwa muda mrefu baada ya kupiga hatua moja mbele tumekuwa mara nyingi tunapiga hatua moja nyuma, sasa hili ni tatizo sana.

Mhe. Spika, viwanja vile vimekuwa chakavu lakini habari tulizokuwanazo ni kwamba wenzetu wa *ZSSF* ndio wamevichukua kwa ajili ya kuvifanyia ukarabati na kuweza kurejea katika hali yake ya kawaida na kuweza kutoa huduma. Lakini tangu tupate habari hizi za kukabidhiwa *ZSSF* muda umekuwa ni mrefu na tunaamini kwamba uwezo wa kifedha wanao. Sasa labda Mhe. Waziri atapokuja hapa atueleze, tatizo ni nini kwa muda wote huo *ZSSF* tangu wamechukua viwanja vile kutokuvifanyia huo ukarabati na kuweza kurejea katika hali yake na watoto wetu wakaweza kwenda kujistarehesha katika yale maeneo. Pia kuondosha usumbufu ambao hivi sasa unatupata kwa vijana kuelekea katika maeneo mawili ambayo yamekuwa hayatoshelezi na inakuwa ni hatari kwa watoto wetu.

Mhe. Spika, baada ya hayo niseme na mimi nashukuru kwa upande wangu, nimshukuru Mhe. Waziri, nimshukuru Mhe. Rais, narudia tena kwa maamuzi magumu. Maamuzi magumu tunayahitaji kwa mara nyengine katika maeneo mengine. Baada ya kusema hayo kwa niaba yangu na kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo la Kwahani naunga mkono hoja Mhe. Spika ahsante.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, naaza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kutupa neema zake za uhai na uzima tukiwa tunajadili shughuli mbali mbali zinazohusu maendeleo ya nchi yetu na maslahi ya watu wetu wa Zanzibar.

Mhe. Spika, nakushukuru na wewe vile vile kwa kunipa nafasi hii na mimi kuchangia niliyonayo kuhusu bajeti ya wizara hii muhimu ya Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo.

Mhe. Spika, nina maeneo mengi kidogo ambayo nataka kuyachangia kwa hivyo naomba niende moja kwa moja katika hoja zangu, lakini kabla sijenda huko Mheshimiwa nataka nianze na mimi vile vile kwa kumpongeza Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo swahibu wangu mpenzi Mhe. Omar Yussuf Mzee. Mhe. Spika, nampongeza kwa sababu ameonesha umahiri mkubwa katika kipindi hiki ambacho amekabidhiwa wizara hii muhimu sana katika nchi yetu na amekabidhiwa kwa niaba ya Rais na matokeo ya kazi nzuri na usikivu wake kutokana na hoja mbali mbali ambazo tumeziibua nafurahi kusema kwamba, kazi yetu imezaa tija hatimaye Mhe. Waziri ameweza kupata zaidi ya shilingi 17 bilioni ambazo amezinusuru kutoka mafungu mbali mbali tuliyokuwa tukiyapigia kelele tangu kikao hiki kimeanza Mhe. Spika.

Mhe. Spika, hilo limenitia moyo kwa sababu inaonesha kwamba serikali yetu ni sikivu, kwamba yale maeneo tuliyokuwa tukiyapigia kelele sio tu kwamba yametiwa kwenye siko moja yakatoka kwenye sikio la pili, lakini serikali imeyafanyia kazi na hatimaye imeweza kupata fedha muhimu kwa ajili ya ununuzi wa meli. Sasa Mhe. Spika, nasema isiwe hili kwa sababu tulikuwa na dharura ya kununua meli ikawa ndio kipaumbele kwa mwaka huu, niiombe wizara na waziri katika hili kila mwaka yale maeneo ambayo tutakuwa tukiboresha katika vikao vya bajeti na katika vikao vyengine tutakapokuwa tunajadili ripoti za kamati tukionesha kuna sehemu ambako mapato yanaweza kuokolewa yakaingia katika shughuli za maendeleo ya watu wetu, basi serikali na wizara kila wakati Mhe. Spika, wawe tayari kuchukua ushauri ambao tunawapa na ku-*act* kutokana na yale maeneo ambayo tunayaonesha.

Lakini hilo la meli Mhe. Spika, na mimi niseme haraka haraka kwamba mimi nadhani Mhe. Waziri ajikite vizuri kuzitumia hizi 17 bilioni ambazo anakusudia kuziokoa kutokana na makato yale ambayo wameyafanya. Kwanza Mheshimiwa pengine ushauri tu, badala ya kufikiria kununua meli moja kubwa sana pengine itakuwa uwezo wake wa kuhudumia hapa kutokana na idadi ya abiria ikawa ni kubwa sana, pengine tutizame uwezekano wa kuangalia meli mbili za kiasi ambazo zinaweza zikapishana baina ya maeneo haya ambayo yanahitajika.

Vile vile Mhe. Spika, kumekuja malalamiko mengi ya wananchi juu ya vifaa vya uokozi zinapotokezea ajali zetu. Kwa hivyo, vile vile kama kitapatikana chochote kikaweza kusaidia serikali kununua vifaa vya uokozi zinapotokea ajali kama hizi basi ningeomba pia fedha hizi zikatazamwa. Mhe. Spika, nasikitika muda haunitoshi kwa hivyo hilo naliacha hapo hapo.

Lakini pia Mhe. Spika, naomba niwapongeze sana *backbenchers* wenzangu katika Baraza lako, kwa sababu ni kazi yetu ambayo imefanya hata Mhe. Waziri kaona katika hotuba yake na akasifu kwa mara ya kwanza Waziri wa Kwanza kwamba kazi yetu imezaa tija katika serikali hii. Naomba tuendelee kuifanya kazi hii kwa niaba ya wananchi wa Zanzibar kwa sababu ndio kazi tuliyoletewa kuja kuifanya hapa. Lakini kazi hii Mhe. Spika, itakuwa haina tija ikiwa hatukukupongeza wewe, kwa sababu tumeshuhudia katika kikao hiki Mhe. Spika, Baraza la Wawakilishi limeandikiwa tahariri mara mbili na Magazeti yanayoheshimika kupongezwa kwa kazi linayofanya chini ya Spika wetu wewe Mhe. Pandu Ameir Kificho, kwamba utaratibu wetu wa kupitisha vifungu na kuzinatia bajeti ya serikali zinaruhusu mjadala mpana unaoweza kutupeleka katika tija sio tu kuonekana tunajadili kwa ajili ya kujadili tu.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, uokozi huu wa shilingi 17 bilioni hauwezi kupongezwa bila ya kuzungumzia nafasi muhimu uliyoifanya wewe katika kuliongoza Baraza hili kutupa uhuru mpana wajumbe wako kuweza kuisimamia serikali.

Sasa Mhe. Spika, baada ya utangulizi huo niseme mimi namuomba Mhe. Waziri kwamba, mbali ya hicho alichofanya bado kuna maeneo mengine ambayo akiyasimamia vizuri yanaweza kumuokolea mapato na hayo naomba nimtajie kwa uchache. Moja Mhe. Spika, namuomba waziri aimarishe mfumo wa udhibiti wa ndani (*Internal Control Mechanism*). Mhe. Spika, huu mara nyingi unafanyika kupitia kwa wakaguzi wa ndani, ndugu yangu Mhe. Ali Salum Ali Mwakilishi wa Jimbo la Kwahani kaligusia sasa hivi hapa. Hili namuomba Mhe. Waziri alitazame kwa umakini sana suala hili na mimi katika hili nimuombe Mhe. Waziri kwanza aiangalie tena *Public Finance Act* yetu Mhe. Spika.

Sheria hii Mhe. Spika, tuli-*copy* na ku-*paste* zaidi kutoka kwa seria kama hii kwa wenzetu Bara, lakini wao wenyewe hivi sasa wanaipitia sheria hii nadhani kipindi si kirefu wataipitisha marekebisho yake kama watakuwa hawajaipitisha. Sasa nadhani Mhe. Spika, na sisi tuitazame, kuna mambo mengine ukitizama unaona hasa kwamba haya yamechukuliwa yakakopiwa tukaletewa sisi, sasa yako maeneo ya kutizama. Moja katika mapungufu ya sheria ile Mhe. Spika, sheria ile haijataja shughuli za ukaguzi moja kwa moja, shughuli za ukaguzi zimetajwa katika *regulation* za sheria ile badala ya kuwemo katika sheria yenyewe na hivyo kuwapa nguvu wakaguzi wetu wa ndani. Naomba hili Mhe. Waziri wa Fedha aliangalie.

Vile vile Mhe. Spika, nilikuwa nadhani kuna utekelezaji wa sheria yenyewe pia. Ukiangalia sheria ile Mhe. Spika, kuna maeneo mengi ambapo ikibidi kufanyika marekebisho serikali imetakiwa lazima ipate idhini ya Baraza na inatakiwa ilete hapa taarifa mbali mbali ambazo ukitizama utaratibu haziletwi. Sasa sina muda wa kutaja mfano mmoja mmoja, lakini naomba Mhe. Waziri aliangalie. Labda nimpe mfano tu, kifungu cha 25 cha sheria ya *Public finance Act* kinasema kwamba, "Itapotokezea kuna fedha za maendeleo ambazo hazikutumika katika mwaka uliomalizika inabidi ripoti yake ilewe katika Baraza la Wawakilishi ili kuoma ruhusa ya kuendelea kwa mwaka wa pili", hilo halifanyiki Mhe. Spika, tunapewa taarifa tu katika hotuba jumla jumla lakini halifanyiki na yako mengi lakini bahati mbaya muda hauruhusu. Lakini nimuombe Mhe. Waziri kwa ujumla aiangalie *Public Finance Act* akitizama ku-*strength* katika utekelezaji wake akatoa nafasi nzuri katika ukaguzi wa ndani basi mimi naamini Mhe. Spika, tutapata nafasi nzuri ya kuokoa mapato zaidi.

Lakini Mhe. Spika, katika kuendelea na hizo nimuombe Waziri wa Fedha hebu aliangalie tena suala la kuanzisha ofisi ya *Internal Auditor General* wa Zanzibar. Watendaji wa Wizara ya Fedha hasa Mhasibu Mkuu amekuwa mzito kulitekeleza hili, na yeye kiasi akatae kulitekeleza na tatizo hili lipo kwa muda mrefu sana, karibu nchi zote za *Commonwealth* tayari zimeanzisha *Internal Auditor General Office* lakini Zanzibar bado inakataa. Kwa nini Mhe. Spika, wanakataa kuanzisha ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani katika serikali, kwa sababu hivi sasa inafaidika, anaweza kufanya madudu yake anavyotaka, wakaguzi wa ndani na wahasibu wote wanaripoti kwake wanawajibika kwake. Sasa Mhe. Spika, anayetumia na anayemkagua matumizi yake wote wanawajibika kwa mtu mmoja hatuwezi tukanusuru fedha za walipa kodi hapo.

Kwa hivyo hili Mhe. Spika, tunamwambia Mhe. Waziri tusije tukafika bajeti ya mwakani hapa tukawa hatujapata sheria ya kuanzisha ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Zanzibar ili kuimarisha mfumo wa kudhibiti mapato.

Mhe. Spika, katika kudhibiti mapato vile vile kumekuwa na uzito katika wizara yake ya kutumia mfumo ambao wameuanzisha wenyewe *IFMS*. Hili Mhe. Spika, linatekelezwa kwa fedha za *recurrent*, matumizi ya kawaida, lakini kumekuwa na ugumu mkubwa katika Wizara ya Fedha kukubali ku-*apply* mfumo huu wa *IFMS* katika hasa fedha za Washirika wa Maendeleo.

Mhe. Spika, wanasema kwamba wale wenyewe hawapendi wana utaratibu wao wa kutizama fedha zao, lakini tumefuatilia kwa washirika hao wa maendeleo wanaonekana mara nyingi wanaaminishwa hivyo ili watu kuficha chaka hili, mfumo huu usitumike ambao unahakikisha kwamba fedha zilizoingizwa zinatumika kwa mujibu wa vipaumbele vyake. Ndio maana Mhe. Spika, mara nyengine kuna suala nitakuja kulizungumza nikifika katika sheria ile ya *appropriation* sitaki kuutumia muda wangu sasa hivi kwa hilo. Lakini kuna tatizo vile vile kwa mfano, katika uhaulishaji Mhe. Spika ndio maana huko chini kuna watu wanachukua mpaka fedha za miradi ya maendeleo kuongezea katika bajeti za safari zao, kwa sababu *simple* huu mfumo wa *IFMS* hawautaki wenigne katika matumizi yao.

Kwa hivyo, nilikuwa namuomba Mhe. Waziri na hili pia alitizame. Hilo lilikuwa ni eneo langu moja nililotaka kulisema kwa urefu kidogo linalohusu vipi kumsaidia Waziri wa Fedha kudhibiti na kuongeza zaidi udhibiti wa mapato yake ili fedha hizi zitumike kwa tija ya wananchi wa Zanzibar.

Sasa Mhe. Spika, nikitoka hapa naomba niende katika eneo la pili. Mhe. Spika, kama kuna taasisi mbili katika Zanzibar zinazofanya kazi vizuri sana na zinaonekana tija yake katika kipindi hiki na wenzangu walitangulia kusema hapa, zilizoko katika Wizara ya Fedha moja ni Benki ya Watu wa Zanzibar (*PBZ*) na pili ni Bodi ya Mapato Zanzibar (*ZRB*).

Sasa Mhe. Spika, nimuombe Mhe. Waziri tuna fununu kwamba Meneja Mkuu aliyesimamia mafanikio makubwa ya *PBZ* pamoja na matatizo yake hakuna binadamu aliyekuwa hakosi kasoro, lakini kazi kubwa aliyoifanya imeonekana, kuna watu tena wengine wamo katika bodi za shirika hili ambao wanamuona ni kikwazo kwao kwa sababu ni mapendekezo yao waliyoyapeleka ya kutafuta kuitumia benki kwa maslahi yao yanakwama, wanamchimba huyu wanataka kumuondoa Mhe. Spika. Macho na masikio ya Waheshimiwa Wawakilishi wa wananchi yako wazi tunaona kila kitu, hilo tutalitazama kwa macho makavu na tutalisikiliza kwa masikio mapana kama yangu mimi Mhe. Spika. Hatutakubali kuona watendaji ambao wamefanya mafanikio wakang'olewa kwa sababu tu kuna baadhi ya wakubwa katika bodi za taasisi hizi wanataka kujinufaisha kwa maslahi yao na hawa kupewa vikwazo.

Mhe. Spika, ingelikuwa sitaki kufika mbali ningekutajia mpaka jina la mtu anayeandaliwa ili kumrithi mtu huyu ili kutaka kumuwekea vikwazo watu wakubwa wapate maslahi yao katika *PBZ* hilo hatutalikubali hata siku moja Mhe. Spika.

Mhe. Spika, vile vile katika *ZRB* nataka nimpongeze sana Kamishna wa *ZRB* Mhe. Mohamed Hashim Ismail. Binadamu yeyote hakosi kasoro zake lakini sote mashahidi kuwa katika kipindi ambacho amekisimamia yeye mapato ya Zanzibar kupitia *ZRB* yamekuwa yakiongezeka mwaka hadi mwaka na Zanzibar imepiga hatua kuliko hata Serikali ya Jamhuri ya Muungano katika suala zima la kukusanya mapato na hivyo kufanya bajeti yetu kwa kiasi kikubwa kwa asilimia itegemee zaidi mapato ya ndani kuliko ilivyokuwa Jamhuri ya Muungano.

Mhe. Spika, eneo jengine ambalao namuomba Mhe. Waziri wa Fedha aliangalie utakuta kama kuna sehemu kubwa ambayo watu wamekuwa wanafuja fedha za umma ni katika manunuzi. Sasa Mhe. Spika, mimi nimuombe Mhe. Waziri huko zamani tunakotoka wazee wetu wanatwambia kwamba serikali ilifika kuwa na utarafibu hapa ikawa manunuzi yote yanafanywa kupitia kwa wakala, kwa hivyo ikawa fedha za serikali zote zinapotaka mahitaji yake zinapatiwa na serikali yenyewe kupitia *crown agent*, lakini huu utaratibu wa kwamba kila mmoja anafanya manunuzi ndio unaongoza mianya ya watu kutafuna fedha za walipa kodi. Nilikuwa naomba hili Mhe. Waziri wa Fedha alitizame.

Mhe. Spika: Umebakiwa na dakika tano.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Ahsante Mhe. Spika, niende haraka haraka eneo jengine ambalo naomba waziri alitazame Mhe. Spika, nimeangalia mimi katika shughuli zinazofanywa na idara ambazo ziko katika wizara yake, moja ni Idara ya Uratibu wa Shughli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Dar es Salaam.

Mhe. Spika, mimi hasa naona idara ile haina sababu tena ya kuendelea kuwepo, tunatafuna fedha bure, tunapoteza fedha bure, ukitizama shughuli zake katika ku-*coordinate* kuratibu masuala ya mashirikiano ya kimataifa shughuli zile zile ukitizama katika Kamisheni ya Fedha za Nje katika wizara hiyo hiyo zinafanywa na idara ile. sasa badala yake Idara ya Uratibu ya SMZ imekuwa ni idara ya wakubwa inayowapeleka Dar es Salaam kuweza kuhudmiwa vizuri wanachukua posho hapa fedha wanazolipwa kama inavyokuwa mtu mwengine katika safari, lakini akifika pale anataka ahudumiwe na ofisi ile kwa hivyo huyu anafaidika mara mbili. Sasa Ofisi ya Uratibu wa SMZ imekuwa zaidi ya kuwahudumia wakubwa ili kupunguza matumizi ya posho zao za safari badala ya kufanya hio kazi iliyokusudiwa.

Kwa hivyo mimi mapendekezo yangu kwamba idara hii imefika pahala Rais ashauriwe aiondoe, tutanusuru fedha nyingi ambazo zinatumika bure pale zingeweza kabisa zikafanywa na idara nyengine.

Naomba pia nigusie kwa ufupi sana umenipa dakika tano Mhe. Spika, suala la *pension*. Kuna maeneo mengi Mhe. Spika, tumeshayaangalia, tumerekebisha viwango vya mishahara lakini tuwatizame na wazee wetu wastaafu, bado viwango vyao vya pencheni *pension* vinasikitisha. Ukiangalia juzi tumewapandishia kodi za nyumba kwa mfano Mji Mkongwe pale, lakini mwengine hana kazi anaishi kwa pencheni ya shilingi 40,000 au 30,000 huyu unampandishia

kodi ya nyumba ya wakfu anaambiwa alipe kwa shilingi 50,000, 100,000 yeye anapokea shilingi 30,000 kwa mwezi au 40,000 ategemee vipi Mhe. Spika huyu.

Kwa hivyo nasema hili serikali iliangalie katika mapato ya wafanyakazi waangalie na wazee wetu katika *pension*. Lakini vile vile waangalie na *formula* inayotumia katika kulipa *pension*.

Mhe. Spika, bahati mbaya kuwa muda ni mdogo lakini ninao mfano mmoja hai ningekupa hapa, kuna mtu aliyestaafu mapema lakini katumikia muda mrefu zaidi na kamaliza kwa kiwango kizuri cha mshahara lakini unakuta mwenzake aliyekuja kustaafu baadae anapata zaidi kuliko yeye. Hii si haki na namtaja kwa jina hasa Mheshimiwa Maalim Mabofu sote tunamjua hapa, Mhe. Abdulrahman Bakari Omar Mfamau alimalizikia kuwa katika Ofisi ya Waziri Kiongozi mwaka 1985 akastaafu. Lakini ukitizama kuna watu wamemzidi ambao yeye alikuwa anawazidi, sasa Mhe. Spika, hilo sio jambo zuri hivyo naomba pia Mhe. Waziri alitizame.

Mwisho kabisa Mhe. Spika, naomba nizungumzie unipe dakika japo tatu nimalizie suala la Muungano katika Wizara ya Fedha. Mhe. Spika, wamezungumza wenzangu hapa na najua Mhe. Waziri anayafuatilia haya, lakini tuantaka pia tupate taarifa tusirudi kila siku tukapata yale kwa yale. Siku zote tunazungumza tume ya pamoja ya fedha leo Mheshimiwa nimekuja na ripoti hii ambayo iliambiwa ni ya siri ya Aprili, 2006. Hii Mhe. Spika, ni ripoti iliyotolewa na *PricewaterhouseCoopers* washauri elekezi walioajiriwa na serikali zetu mbili ili kwenda kuangalia suala zima la mapato.

Mhe. Spika, ukiangalia ripoti hii katika ukurasa wa 33 inaonesha hii kwamba samahani katika ukurasa wa 29 Mhe. Spika, kwamba matumizi yote ya shughuli za Muungano yanayofanywa na Serikali ya Muungano ni shilingi 537,258,000,000/-. Lakini mapato Mhe. Spika, ya vyanzo vya fedha za Muungano kwa ujumla wake hii ilikuwa kwa mwaka 2003/3004 ni *trillion* moja, thalathini bilioni mia nane na ishirini na sita milioni nukta moja.

Ndio kusema Mhe. Spika, ukitoa yale matumizi yote ya muungano niliyoyataja pale mwanzo utabakiwa na bakaa ya mia tano na tisini na tatu bilioni mia tano na sitini na tisa nukta tisa ambazo hizi zilikuwa ziligaiwe kwa fungu litakalokubaliwa baina ya serikali mbili. Hii Mhe. Spika, ndio siri iliyokuwa haitaki kusemwa kwamba ukenda uki-apply mapendekezo ya tume hii Zanzibar itafaidika, wenzetu hivi sasa wanatumia mgongo wa muungano kufaidika wao. Haya Mhe. Spika, ndio yanayowafanya wananchi wa Zanzibar waseme waachiwe wapumue, wamechoka kutumiliwa. Tunaambiwa siku zote kwamba ni mzigo kwao, kumbe ukweli Mhe. Spika, wao ndio waliobeba mambeleko ya Zanzibar.

Sasa mimi siku zote husema kama sisi ni mzigo kwao, watutue Mhe. Spika, tumechoka kubebwa, tujisimamie wenyewe na kujiendesha wenyewe. Lakini vile vile ukiangalia katika taasisi nyengine kama BOT, kilipoanza kikao chako tulipewa ripoti ninafikiri na wewe utakuwa umepewa na wewe.

Hili Mhe. Spika, ukitazama huku mwisho kuna kiambatisho ambacho kina orodha kuanzia ukurasa wa 269 mpaka ukurasa wa 273, kina orodha ya viongozi wote wale wa Benki Kuu, pale katika ngazi ya utawala na katika matawi yake yote Tanzania. Mhe. Spika, watu hawa hawapungui 80, ninafikiri Mzanzibari ni mmoja. Hii unaambiwa ni taasisi ya muungano inaratibu uchumi wa pande zote mbili. Katika hali kama hii Mhe. Spika, hatuwezi tukaendelea hata siku moja, hawawezi wakatutendea haki. Kwa hivyo ninataka kauli ya Mhe. Waziri haya kuwa tutaendelea kupiga kelele katika Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, kuna points moja ambayo nimeisahaui naomba unipe dakika moja tu, ilikuwa ni point muhimu sana niliisahau. Pale mwanzo nilipokuwa nikimsaidia Waziri wa Fedha katika maeneo ambayo yanapaswa kuyatazama, kuna siku Mhe. Spika, Waziri wa Fedha alitwambia hapa aliwanasihi mawaziri wenzake kwamba wao ndio wanaokuja hapa kutetea bajeti, kwa hivyo katika matumizi pia wizarani wasikubali kuekwa mkiani na Makatibu Wakuu wao na watendaji wengine. Akawataka pamoja na kwamba sheria zote zinatambua Chief Accountant Officer ni Katibu Mkuu lakini na wao wahakikishe kwamba wanajua mapato wanayokuja kuyaomba hapa yanatumika vipi.

Sasa Mhe. Spika, nilikuwa ninataka kusema hili moja tu hebu Waziri anisaidie. Mimi nikitazama Katiba ya Zanzibar Mhe. Spika, kifungu cha 43(5) kinazungumzia uwajibikaji wa pamoja wa mawaziri chini ya Makamu ya Pili wa Rais katika Baraza la Wawakilishi.

Lakini nilipo hasa Mhe. Spika, kuna kifungu hapa kinazungumzia kifungu cha 50(1) cha Katiba yetu ya Zanzibar, kinasema kwamba pale Makamu wa Kwanza wa Rais na Makamu wa Pili wa Rais au Waziri yeyote mwengine anapokuwa na dhamana ya wizara yoyote ya Serikali atakuwa ndiye kiongozi na msimamizi mkuu na bila ya kuathiri masharti yoyote ya usimamizi Katibu Mkuu ambaye afisi yake itakuwa ni utumishi wa serikali atakuwa ndiye afisa mtendaji mkuu wa wizara.

Naomba ni-underline pale aliposema Mhe. Spika, na bila ya kuathiri masharti yoyote ya usimamizi. Kwa hivyo pamoja na Katibu Mkuu kutajwa katika Katiba hii kwamba ndiye afisa mtendaji mkuu wa wizara, lakini bado role kubwa kapewa waziri katika kusimamia wizara. Na usimamizi Mhe. Spika, ni pamoja na matumizi.

Sasa niwaombe mawaziri mwaka huu tumewatesa sana hapa lakini si kwa nia mbaya, ni kwa nia ya kuhakikisha tunalinda fedha za walipa kodi. Sasa niwaombe watumie hii Katiba Mhe. Spika, mawaziri na wachukue ushauri aliowapa Mhe. Omar Yussuf Mzee wasimamie katika kamati zao za uongozi za wizara, wajue kwamba kila fedha wanayokuja kuiomba wao mawaziri tukawapitishia hapa kule wizarani kwao inatumika vipi ili mambo yaliyojitokeza mwaka huu yasije yakajirejea Mhe. Spika.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo ninashukuru sana kwa kunivumilia, ninajua umenivumilia kwa sababu ninazungumzia ambayo ni ya msingi kabisa katika maendeleo ya nchi yetu, naomba sana Mhe. Waziri wa Fedha anipatie majibu za hoja zangu hizo, na baada ya kusema hayo ninafikiri kwa mara ya mwanzo tangu tumeanza bajeti hii, ninasema ninaiunga mkono bajeti hii asilimia mia moja.

Ahsante sana Mhe. Spika. (*Makofi*).

Mhe. Abdalla Mohamed Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi ya kuzungumza machache kuhusu wizara hii inayotuwezesha. Kiujumla mimi sitokuwa na mengi kwani ninayafahamu kwa vile kamati hii imo katika jukumu letu sisi. Isipokuwa nitakuwa na baadhi ya mambo pengine ningeomba nipate maelezo na mengine labda nitatoa mchango wangu kama ninavyofahamu.

Mhe. Spika, mimi nikitaka kidogo nipate maelezo kuhusu eneo la Bwawani. Ukifuatilia eneo hili unaambiwa lipo katika Kitengo cha ZIPA kwa wawekezaji. Mwaka jana tuliambiwa lipo chini ya Wizara ya Biashara. Sasa labda Mhe. Waziri angekuja hapa akanipa maelezo kidogo, jee lile eneo la Bwawani lipo chini ya wizara gani.

Mwaka jana Wizara ya Biashara pia ilitwambia kwamba eneo hili inalitafutia wawekezaji kwa ajili ya kuekeza labda pengine kuondoa ule uchafu na kupata wananchi wengine ajira baada ya kuweka wengine makontena au kujenga ili kuweka vitega uchumi vyengine.

Sasa sijui wale wawekezaji wamepatikana au hatua gani iliyofikiwa mpaka hivi sasa ya kuwapata hawa wawekezaji. Kwani vile vile tulisikia fununu kwamba kuna watu wameshajitokeza kulitaka eneo lile.

Lakini jengine ni kwamba kila mwaka ninachokifahamu kuwa serikali yetu hupokea msaada wa mchele kutoka Serikali ya Japan na mwaka jana nina imani kwamba mchele huo ulitufikia. Sasa jee baada ya kuuzwa kwa mchele huo zilipatikana fedha kiasi gani na zilipelekwa katika mchango wa maendeleo yepi au sekta gani pesa hizo zilipelekwa kwa ajili ya maendeleo.

Mhe. Spika, jengine ni kwamba ninataka nipate ufafanuzi kidogo kuhusu Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali. Moja katika shughuli zake ni kulipa mishahara serikalini lakini hivi sasa kumejitokeza wafanyakazi ambao wanakuwa hawapo au tuseme ni wafanyakazi hewa au wapo masomoni. Sasa sijui idara hii inahakikisha vipi kwamba huyu mfanyakazi ana ngazi hii ya ukweli na anastahili kulipwa mshahara huu. Kwa nini ninasema hivyo.

Mhe. Spika, kwa sababu baada ya Wizara ya Utumishi wa Umma kufanya uzoezi la wafanyakazi serikalini imegundua kwamba kuna pesa zimebakia labda niseme Wizara ya Elimu katika miezi mara mbili tofauti walizofanya utafiti huu, waligundua kwamba kuna bakaa ya karibu milioni 60 na walipofanya mara ya pili waligundua kwamba kuna bakaa ya karibu milioni 70.

Sasa jengine labda jee hizi fedha ambazo huwa zinabakia zinarudishwa katika mfuko mkuu wa serikali au zinabakia wapi. Lakini la msingi jee, kuna uridhikaji wa kiasi gani wa Idara hii ya Uhasibu kwamba wafanyakazi hawa wapo na wanastahiki kulipwa mishahara hii kama walivyoombewa na Wizara ya Utumishi wa Umma.

Mhe. Spika, nikiondoka hapo nije kidogo Mfuko wa Hifadhi ya Jamii ambao Mhe. Hamza na yeye ameugusia. Ninafikiri Mhe. Spika, hivi sasa tumeshafikia wakati wa kufanya marekebisho ya sheria, kwa sababu wengi katika wanaostaafu wanalalamikia mapato yao au viinua mgongo vyao lakini wengine huwa wanafukuzwa kazi bila ya kufika huo umri ambao unaohitajika mtu alipwe pesa hizi.

Sasa ningeomba tu wizara ikaangalia kwamba hivi sasa kuna haja ya kuirekebisha sheria ili kuruhusu watu kupata pesa zao mapema wakaanza kutumia wakiwa nguvu na sio kuwangojea wameshakuwa hawana nguvu tena ndio wakaanza kupata pesa yao hii.

Lakini jengine ni katika sekta ya misamaha ya kodi. Ninafikiri nia ni nzuri kwamba sisi tunawaomba wawekezaji waje katika nchi yetu ili na sisi tupate kuendelea. Lakini kuna malalamiko makubwa kutoka kwa hawa watu ambao wanakuja kuekeza katika nchi yetu. Wengi wao wanacheleweshewa kupata bidhaa zao kutokana ama waziri hayupo au yeye atakuwa yeye ni peke yake ambaye anafanya shughuli hii.

Ninafikiri hili tungeliangalia kwa kina tukaona sasa labda kwamba ikiwa ni mtoaji kodi ni waziri peke yake, basi labda aka-delegate power kwa watu wengine ili kuwaondoshea watu hawa usumbufu. Kwani wengine wanadiriki kusema kwamba labda sisi tulifanya kosa kuja kuekeza katika nchi hii ya Zanzibar kwani mzigo wake pengine unaweza kubakia bandarini si zaidi ya miezi sita akiwa tayari ameshaanza kufanya booking ya wageni na anachelewa kuupata mzigo wake.

Sasa ninahisi tungeiangalia tena hii sheria tukawaruhusu na wengine wakaweza kutoa misamaha ili hawa watu wasilalamike zaidi. Kwani Waziri safari zake za nje zimekuwa ni nyingi kiasi kwamba inachukua muda kuwa haapatikani.

Mhe. Spika, nimalizie kwa suala la BOT. Hivi sasa BOT ndio inayomiliki au iliyo na sheria nyingi na sisi tuna wafanyakazi wetu; kuna wafanyabiashara wetu ambao huwa wanahitaji fedha za nje kwa ajili ya biashara zao. Lakini ukenda BOT hakuna ile inayoitwa Bureau de Change kwa ajili ya kupata pesa hizo. Mara nyingi wafanyabiashara hawa hulazimika kwenda Tanzania Bara kubadilisha pesa zao.

Sasa ningeiomba wizara ikaangalia kwamba kuna umuhimu hivi sasa wa kuwa na sisi kitengo hiki kipo ili kuwarahisishia wafanyabiashara wetu upatikanaji wa pesa hizi za kigeni na biashara zao kwa jumla.

Kwa hayo machache Mhe. Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*).

Mhe. Ali Mzee Ali: Mhe. Spika, na mimi ninakushukuru kunipa nafasi hii.

Mhe. Spika, sasa hivi tunahitimisha hili Baraza letu labda kesho tunafunga. Kwanza nikupongeze kwa nguvu ulizonazo kwa kipindi cha mwezi unusu Baraza hili kuliongoza. Mhe. Spika, una nguvu na una uwezo.

Sasa leo tunazungumza Wizara ya Fedha ndio roho ya taifa hapa Zanzibar. Maana kuna maneno mengi, malalamiko mengi kwenye vyombo vya muungano; Benki Kuu, fedha ya pamoja, TRA. Haya ni matatizo sugu ya muda mrefu sana.

Sasa tumepata waziri Ndugu Omar Yussuf Mzee. Ndugu Omar yeye alikuwa Katibu Mkuu Mipango, akawa Katibu Mkuu Afisi ya Waziri Kiongozi, akaamua kuingia katika siasa, akagombania katika Jimbo la Kiembesamaki akashinda, akenda Bara akawa Naibu Waziri wa Fedha. Baada akarudi na Dr. Shein akamkabidhi wizara hii.

Ni mzoefu na anajua mengi. Hata ile Tume ya Watalaamu siku za nyuma, yeye alikuwa ni mjumbe. Benki Kuu kuifanyia reform hii Benki ya Watu wa Zanzibar, yeye alikuwa ni mjumbe. Amepata uzoefu, ameona idhilali, matatizo alipokuwa Naibu Waziri wa Fedha. Naamini akiwa na nia njema na tukimsaidia, haya matatizo ya muungano wa fedha tutayamaliza kabla ya Katiba mpya haijaja.

Lakini Mhe. Spika, sijabahatika kuchangia michango ya semina hii. Hapa Mhe. Spika, wakati wa mfumo wa vyama vingi Mhe. Spika, wewe ulikuwa ni mjumbe wa Baraza hili, Mhe. Asha Bakari Makame alikuwa ni Naibu Waziri na Mhe. Ramadhani Abdalla Shaabani basi. Nyinyi ndio muliopitisha sheria ya kuanzisha mfumo wa vyama vingi, kutoka sera ya chama kimoja kuanzia 1964 mpaka 1992, nyinyi watatu mukiwa ndani ya Baraza hili lakini si peke yenu mulikuwa ni 70.

Nyinyi ni mashujaa mulioanzisha mfumo wa vyama vingi. Kwa bahati nzuri wewe Mhe. Spika, ulikuwa ni mjumbe wa Tume ya Vyama vingi, wewe ni Spika. Mhe. Spika, simamia sera ya vyama vingi, simamia culture ya vyama vingi tulipitisha wenyewe sisi CCM.

Sasa muungano wetu umekuwa wa muda mrefu mpaka kufikia miaka 48, una matatizo mengi na wala sio siri. Niruhusu nimnukuu Waziri Kiongozi wakati anaahirisha Baraza mwaka 1992 wakati sheria ya vyama vingi tunapitisha ambapo wewe ulikuwa ni mjumbe, Bi. Asha.

Anasema,

> "Mhe. Spika, ninapenda kuhakikishia Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imekubali sana wazo hili, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeshaunda Tume ya Baraza la Mapinduzi ambayo itachagua yale mambo ambayo yapigiwa kelele na watu kusikitika pande zote mbili. Mapendekezo ya Tume hiyo baada ya kuthibitika na Baraza la Mapinduzi tutawasilisha kwa wenzetu kupitia taratibu zitakazoekwa ili serikali zote mbili ziweze kukaa kujadili kupatiwa ufumbuzi muafaka. Kiongozi au mwananchi yeyote atakayekuwa na maoni ya kuimarisha muungano wetu kwa mfumo wetu huu tuliokubaliana ya serikali mbili anaweza kupeleka kwa Waziri wa Nchi Afisi ya Rais na Mwanasheria Mkuu".

Hiyo ni ahadi ambayo ameitoa Waziri Kiongozi alikuwa ni Marehemu Dr. Omar Juma.

Kwa upande wa wenzetu Tanzania Bara, Mhe. Waziri Mkuu na Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais wakati akifunga mjadala wa marekebisho ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano kuhusu suala la serikali zetu mbili kukutana ili kufuatilia ufumbuzi wa matatizo yaliyojitokeza alisema na ninanukuu,

> "Mhe. Spika, kwa niaba ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano ninapenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge, wananchi wa Tanzania na watu wote duniani wanaoutakia mema kuanzia sasa kazi moja wapo itakayopewa kipa umbele na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kujadili kwa kina, uwazi na kwa ukweli matatizo yote ya kimsingi yaliyojitokeza katika utekelezaji wa muungano na kisha kuyapatia ufumbuzi wake ili kuimarisha muungano wetu".

Hayo alisema Waziri Mkuu, yaani yule Prime Minister alikuwa Ndugu Machela mwaka 1992.

Mwaka 1995 Rais Kikwete anasema anaunda hizi kamati za Waziri Kiongozi na Waziri Mkuu watatue matatizo ya muungano, hawana wakutane wanywe chai. Inasikitisha tunatoa ahadi tu na ukirudi nyuma kwa Mhe. Aboud Jumbe halikadhalika.

Sasa ninasema hivi haya matatizo naomba tuyamalize kabla ya Katiba mpya haijaja, Katiba mpya tusipeleke uouza na uchafu, tupeleke kitu kipya. Na ninafikiri Balozi Seif aliahidi haya mambo atayamaliza. Nimeona nitoe nibaji hiyo kwa sababu hii ni wizara ambayo inashughulikia kero za muungano. Ndugu Omar jitihidi tupo nyuma yako.

Mhe. Spika, BOT haina sura ya muungano. Tumesema sana humu ndani ya Baraza la Wawakilishi, tukapewa Deputy Governor akawa mmoja, baadae wakabadilisha wakaweka watatu. Sisi tulitaka tupate nafasi kuongoza Benki Kuu sio kuwa wasaidizi. Sasa wasaidizi watatu, wetu sisi ni karani tu, administration. Hatwendi hivyo. Lazima tuende pahala kwa nia njema tuweze mambo kuyarekebisha. Yapo mengi lakini leo ninaelezea hayo.

Sasa nije kwenye suala hili la meli. Sisi Mhe. Spika, tumesema sana kwenye Baraza hili, hapa ninaye Professor Ali Denge mwaka 2006 kaomba meli inunuliwe, waziri kajibu tutanunua meli. Hapa ninayo ripoti ya Said Ali Mbarouk mwaka 2006 anasema tutanunua meli.

Sasa meli ni tatizo ambalo tulilisema siku nyingi. Kwa nini tulilisema mwaka 2006 kwa sababu tayari MV Mapinduzi ilikuwa inaanza tena kufa. Kulikuwa hakuna ajali. Ilikuwa tununue meli. Mimi bado ninaunga mkono kuwa tununue meli.

Lakini tatizo sasa hivi sio meli. Hizi ajali zinazotokea Mhe. Spika, utanisamehe sana, hapa nina ripoti ya mwaka 1956, ripoti ya Commision Enquiry, kuna Skuna ilipata ajali 1956 Sir John Grey jaji ndiye aliyepewa kazi hii. Mhe. Spika, tangu mwaka 1956 ajali hii ya Skuna Hiyari Yako hakuna ajali tena iliyotokezea mpaka mwaka 2009.

Mwaka 2009, 2011 na 2012 lakini ajali zote hizi zilianzia Dar es Salaam. Meli ya kwanza ilianzia Dar Es Salaam ikafikia pwani ya Forodha mchanga, meli ya pili ikapita transit ikafia Nungwi, hii juzi pia imeanzia Dar Es Salaam.

Kuna management meli kule haiwezi kuondoka mpaka ipate kila kitu, safe clearance. Naomba kwa serikali alijibu suala Mhe. Mohamed Aboud sijui tume, naomba tushirikiane tufanye utafiti meli zote tatu zilitoka kule na kule meli haiondoki mpaka iwe na kila kitu. Lakini kuna chombo hapa tumeunda cha usajili, hichi chombo kina matatizo makubwa sana Mhe. Spika, kinataka kurekebishwa. Tusione haya chombo hiki kina matatizo asubuhi meli inampa registration, jioni inamfutia.

Vile vile mambo ya uokozi ni matatizo, tukipe nguvu kikosi cha uokozi ambacho kile cha fire. Kama tuna pesa tuwape wale za uokozi. Hakuna shortage ya meli hivi sasa juu ya usafiri lakini serikali inategemea kuleta meli. Sasa hizi fedha tutizame tunafanya nini.

Sisi Mhe. Spika, mwaka 1974, Zanzibar kwa nini tuwe na meli kwa sababu sisi ni kisiwa, ndio sababu kubwa tunayotakiwa tuwe na meli. Lakini Mhe. Spika, usidhani jambo hili ni jipya.

Mhe. Spika, niruhusu kidogo nikupe historia ya meli ili tujue. Mwaka 1831 palikuwa na meli hapa, meli hiyo ya serikali ya nchi hii ilikuwa ya Sayyid Baraghash. Mwaka 1905 meli ya SS Badra ilitengenezwa Calcuta India, SS Copie mwaka 1912 ilitengenezwa Ujerumani, SS Dreg mwaka 1930 ilitengenezwa England, Alhadhara iliuzwa baadae, Al-Sayyid meli hii ilibeba askari kupeleka Barma baadae ikauzwa.

Halafu ikaja meli inaitwa Salama na Khalifa mwaka 1957. Meli hizi za Salama na Khalifa zilirithiwa na mapinduzi; jina ikabadilishwa moja ikaitwa Jamhuri na moja Afrika baadae zikisha muda wake tukamuuzia jamaa wa Pemba yule zikazama sijui Mtambwe mwisho wa hadithi yake.

Ndio anaitwa Mapete kauziwa. Ndipo Serikali ya Mapinduzi – Mzee Karume akatoa order ya meli ya MV Mapinduzi. Jumbe ndiye aliyemalizia 1974 meli zikaja. Meli ya MV Mapinduzi tumelipa pesa cash kwa sababu Aboud Jumbe pesa nyingi alirithi za Mzee Karume alilipa cash.

MV Mapinduzi tumeitumia. Hizi meli Mhe. Spika, zina sheria zake. Meli za abiria ni miaka 20 baada ya hapo lazima, kwa hivyo baada ya miaka 20 wale Wajapan wakatoa certificate kuwa sasa meli hii haifai. Kwa hivyo meli hii ilitakiwa imalizike lakini tukaitumia kwa miaka saba zaidi. Mwaka 2006 meli ikalala fofo.

Mwaka 2009 meli tukaiuza. Nilibahatika kuwa mimi ndiye mwenyekiti wa Shirika la Meli. Nikakuta meli ile dola laki moja watu wanaitaka. Lakini Mhe. Mwakanjuki Mungu amrehemu wakasema meli hatutaki kuiuza, wanasema meli ni mapinduzi na mapinduzi yatauzwaje.

Mimi na bodi yangu tukenda kwa Rais Karume tukamwambia, mimi nikatoa wazo na yeye alikuwa mgumu kuuza mapinduzi. Nikamwambia sikiliza mzee tuuze tununue meli nyengine, halafu meli mpya tuite mapinduzi daima, akasema aah! hiyo sawa. Meli tukaiuza.

Lakini siku hiyo hiyo kwenye BLM tulipitisha azimio la MV Maendeleo iuzwe. Mhe. Haroun hayupo aliunga mkono. Mhe. Machano alikuwa Waziri akasema aah! unajua MV Maendeleo tuipe muda iende ikafanye service ikirudi iuzwe, haijauzwa mpaka leo. Nayo imekwisha muda wake. Wala serikali isitie pesa pale imeshakwisha, itakuwa kazi bure.

Sasa kuna meli Maendeleo ilinunuliwa na meli ya Ukombozi. Meli mbili hizi tulikopa mkopo kutoka Japan. Huyu Karume Rais Mstaafu alikuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Mawasiliano na Balozi Idiria alikuwepo Japan wakati wa Aboud Jumbe, wakafanya utaratibu wakapata mkopo wa kununua meli ya Maendeleo na ya Ukombozi kwa mkopo wa long term.

Mkopo ule Mhe. Spika, kwa taarifa yako hatujalipa baadae tukasamehewa. Senti moja hatujalipa baadae tukasamehewa. Dunia ya leo ni dunia ya kukopa, unaweza ukakopa. Kwa hivyo ninataka nitoe historia hiyo wajue kuna nafasi za kukopa, ushahidi mzuri wa meli ya Maendeleo na Ukombozi.

Lakini meli ya Ukombozi Mhe. Spika, kwa taarifa ya serikali kwa wananchi ikifika middile of thirteen 2013 Juni, meli ya Ukombozi itakuwa haitakiwi itembelee. Hakuna atakayekodi na hakuna atakayeitaka kwa sababu ni single engine itakwisha.

Sasa tutafute meli ya abiria lakini tujue na meli ya mafuta nayo ina umuhimu wake. Meli zipo nyingi hizi. Kwa hivyo mimi nimeona nitoe taarifa hii ili ikae kwenye *record*, sasa mimi ni mtu mzima nimefanya kazi hapa na mimi mwenyewe Mhe. Spika, hii *insurance broker* ambaye nilikuwa nina *lead* katika biashara ya meli Tanzania nzima sio Zanzibar, hiki cheo nilichokipata nimekipata kutokana na kazi hiyo.

Mimi Mhe. Spika, niliona hayo niyaeleze, lakini nampongeza sana Mhe. Rais wa Zanzibar Dr. Shein kuwa agizo alilolitoa la kununua meli, meli tunaihitajia lakini tunaweza kwenda polepole tusifanye papara na haraka, cha muhimu kwanza tunasoma ripoti hii ya meli zilizozama zote tatu kila ripoti mwiso wake inasema management, rushwa, uchafu. Tulikubaliana pamoja kuwa tununuwe meli. Sasa nimeona mheshimiwa nizungumze hayo.

Mhe. Spika: Bado dakika mbili Mhe. Mjumbe.

Mhe. Ali Mzee Ali: La mwisho kabisa Mwalimu Nyerere ni muasisi wa Muungano wetu alisema hotuba yake hii hapa, anaita nyufa. Nyufa hizi mheshimiwa kazieleza sana. Amesema kuna nyufa tano. Haya maneno ni ya 1995. Ufa wa kwanza, ni Muungano, sio Ali Mzee Ali ni Julius Kambarage Nyerere.

Ufa wa pili kupuuzwa na kutojali katiba, ufa wa tatu kuendesha mambo bila kujali sheria, ufa wa nne rushwa na ufa wa tano ni ukabila na udini.

Mhe. Spika, haya ni maneno ya Nyerere tuyafanyie kazi. Mimi naunga mkono bajeti hii, niko tayari kwa haya niyoyasema kuyathibitisha ikiwa kuna mtu anaona nimekosea au anataka uthibitisho. Lakini nasema wakati sasa umeshafika Mhe. Spika, wananchi wetu wanakwenda kutoa maoni yao, wakatowe maoni yao, tuwaelimishe, tuwafahamishe ili tuweze kupata katiba mpya. Kwa hayo Mhe. Spika, nakushukuru sana ahsante sana.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Nakushukuru Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi ili niweze kuchangia kwenye hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo.

Mhe. Spika, mimi nikianza mchango wangu nianzie kwenye ukurasa wa 53 wa kitabu cha Mhe. Waziri kwenye hitimisho pale. nianze pale kwa kumpongeza sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa uamuzi wake wa makusudi kabisa wa kuiagiza Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, kutafuta fedha haraka iwezekanavyo kwa ajili ya ununuzi wa meli ili kukabiliana na tatizo kubwa linalowakumba wananchi wa visiwa hivi.

Mhe. Spika, kwa kweli Mhe. Rais ameonesha hekima na busara zake katika hili. Ni lazima tumpongeze na atakaye beza katika hili kwa kweli huyo haitakii mema Zanzibar.

Mhe. Spika, katika hili basin a mimi nimsaidie Mhe. Waziri katika kutafuta vile vianzio, kuna kianzio kimoja mimi nimekiona kinaweza kikamsaidia kama tutabadilisha baadhi ya sheria kidogo tukaweza kukusanya zaidi akaweza kuzipata fedha zaidi katika kulifanikisha hili.

Kwa mfano, kuna viwango vya kodi *with only in tax*, katika eneo la *service fees* na *individual consultant*. Sheria inasema kazi hiyo ikifanywa na mgeni ukatwe asilimia 15 ya pato, lakini ikifanywa na raiya wa Tanzania hatakiwi kukatwa kitu. Sasa mimi nimefanya uchunguzi wangu mdogo kidogo, nimegundua kwamba kuna mapato mengi

pale ambayo tunaweza kuyakusanya, kwa sababu watu wengi wanaofanya kazi hizi wanapata kipato kikubwa pale. mfano milioni moja, milioni tano mpaka milioni 50 huko wanaweza kulipwa kutokana na kazi hii ya *consultant*. Lakini hakuna kodi ambayo inalipwa pale. Sasa mimi nafikiria Mhe. Waziri kama tutarekebisha kidogo baadhi ya mambo hapa zipo pesa tutaweza kuzikusanya vizuri na tukaweza kuziongezea katika mipango yetu.

Vile vile Mhe. Spika, sheria hii haiendani na wakati, kwa sababu kazi hizi sasa hivi wako wengi wanaozifanya sio wageni ni wazalendo. Lakini ukitizama pale ile sheria imewapa nafasi kwamba wasitozwe kodi. Ndio maana nikasema pale tunapesa nyingi ambazo tunaweza tukazipata.

Mhe. Spika, mimi namuomba Mhe. Waziri afanye utafiti katika wizara na taasisi za serikali na mashirika yetu yale ya ndani na ya nje, basi unaweza ukagundua kwamba watu wetu wapo wanaofanyakazi katika mashirika yale ya kimataifa kwa njia ile ile ya kwamba ni ma-*consultant*, wanalipwa pale, lakini hakuna kodi inayokatwa ya *income tax* katika mishahara yao. Sasa na eneo hili nalo uliangalie kwamba wanakuwa ni wafanyakazi wa serikali au wa mashirika ya serikali, lakini wanafanyakazi katika mashirika haya kwa njia ile ya *consultant*, wanakuwa ni ma-*consultant* katika yale mashirika lakini wanalipwa, lakini fedha zile wanazolipwa huwa hawatozwi kodi ya *income tax*. Kwa hivyo, mimi nafikiria Mhe. Waziri hebu paangalie vizuri hapa, unaweza ukatunisha mfuko wako kidogo hapa.

Mhe. Spika, nikiendelea mbele nisogee kwenye ukurasa wa 8 wa kitabu cha Mhe. Waziri hiki

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, mnaotoka nje kupasha moto miguu, basi tuelewe tu kwamba baada ya muda fulani nitamuomba Mhe. Waziri ikifika mnamo saa 5:30 afanye majumuisho na hatimaye tufanye uamuzi wa hoja hii. Kwa hivyo, niwaombe basi tukumbuke kurudi ili saa 5:30 tusikilize majumuisho na hatimaye kupitisha vifungu, nawaomba sana.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Spika, nikiendelea mbele mimi nasogea kwenye ukurasa wa 8 wa kitabu cha Mhe. Waziri kwenye Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali. Mhe. Spika, mnamo mwezi wa Oktoba 2011, SMZ iliongeza mishahara ya watumishi wote kwa kuzingatia kiwango cha elimu na muda wa utumishi wao serikalini. Tunaishukuru sana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kupandisha au kwa hatua hii muhimu. Jambo ambalo lilishindikana kufanyika kwa muda mrefu ambapo limeongeza ufanisi katika utendaji kazi.

Mhe. Spika, kuondosha tofauti kubwa ya mishahara au kuweka tofauti kubwa ya mishahara baina ya watendaji hawa wa kada ya uhasibu, imeleta malalamiko, yamejitokeza malalamiko. Mimi nafikiri serikali yetu iko mbioni katika kuyapatia ufumbuzi. Lakini Mhe. Spika, baada ya mabadiliko yale yaliyofanywa na serikali kwa ujumla, wizara ya fedha ilifanya zoezi la peke yake la kubadilisha ile kada ya uhasibu tu pale, wanaita kwenye Wahasibu Wakuu wa Mawizara na Wakaguzi, iliongeza mshahara kiasi mpaka milioni 1,500,000 kwa Muhasimu Mkuu wa Wizara na Mkaguzi Mkuu. Jambo hili lilipata baraka za utumishi wa umma.

Sasa mimi kidogo nimekuwa na mashaka Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri atueleze ni kitu gani kilichomfanya kupandisha mishahara kwa watendaji hawa baada ya zoezi la serikali kukamilika. Kwa sababu ongezeko la mishahara huzingatia elimu na uzoefu wa kazi, yaani utumishi wa muda mrefu na uzoefu, angalau basi wanasema katika kada hii ya uhasibu wanasema angalau basi mtu awe na uzoefu wa kuanzia miaka mitatu na kuendelea.

Basi hebu Mhe. Waziri unisaidie kidogo ni kitu gani kilichowasukuma kuwapa nafasi hizi watumishi wengine ambao hawajafika hata muda ule wa miaka mitatu katika kazi zao. Maana yake kuna wafanyakazi au watumishi baadhi yao ndio kwanza wana miaka miwili au mwaka mmoja katika kazi unampandisha mpaka kuwa Muhasibu Mkuu wa wizara. Mimi nafikiria hili ni tatizo na hili linaleta mgawanyiko kidogo au malalamiko kwa wale wengine ambao wana elimu kama zile wana uzoefu, lakini hawakuweza kubahatika kuwekwa katika nafasi hii. Ingawa sio wote wanao bahatika kuwekwa katika nafasi hizi kwa sababu ni chache na wizara zetu ziko 16 tu. Lakini ukiangalia wale ambao wamewekwa katika nafasi ile basi wawe wanalingana na vile vigezo vinavyotakiwa. Kwa hivyo, Mhe. Spika, nilikuwa namuomba Mhe. Waziri atakapokuja anisaidie maelezo katika hili.

Mhe. Spika, nikiendelea mbele hapo hapo kwenye Idara hii ya Mhasibu Mkuu wa Serikali, niangalie katika kitabu kilichotolewa na Mhasibu Mkuu wa Serikali, yaani *accounting manual* na *auditing manual* ambacho ndani yake mule amewagawa wale wahasibu katika kada 4 tofauti. Kuna wahasibu wakuu au wakaguzi wakuu, kuna *principal accountant* na *principal auditor*, lakini kuna ma-*accountant* na *ma-auditor*, halafu kuna *auditor* na *accountant*.

Utaratibu huu umewekwa ili watendaji wale waweze kuwa na ngazi ambazo upandishaji wa vyeo vyao utalingana na zile ngazi husika. Sasa vitabu hivi vilitolewa tangu mwaka 2005, vimekuwa vikitumika na wahasibu na wakaguzi katika kazi zao. Lakini kutokana na kutowajibika kwa Idara ya Muhasibu Mkuu, imeshindwa kuwapanga wahasibu na wakaguzi katika ngazi hizo 4, jambo ambalo limepelekea kuwaweka Wahasibu Wakuu na Wakaguzi bila ya kuzingatia elimu na uzoefu wao katika kazi.

Mhe. Spika: Unazo dakika tatu.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: hee. Ahsante Mhe. Spika. Mimi nilikuwa namuomba Mhe. Waziri atakapokuja pia anieleze ni sababu zipi zilizopelekea kutokufuatwa kwa muongozo ule. Lakini kuna tatizo jengine la Wahasibu Wakuu kule Pemba, ambao hawa ni wasaidizi wakubwa kabisa wa Wahasibu Wakuu hawa wa Mawizara, katika nyongeza ile ambayo ilifanywa na Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo haikuwagusa wale wahasibu wa kule Pemba. Sasa Mhe. Waziri akija atusaidie sijui ni tatizo gani lililofanya kwamba wahasibu wale nao wasiingie katika nyongeza ile.

Lakini hapo hapo Mhe. Spika, ukiitizama hii nyongeza ambayo imefanywa na wizara ya fedha, kwa Wahasibu Wakuu tu wa wizara na ma-*auditor* wale wa wizara, kunaleta mgawanyo katika kada hii. Lakini hofu yangu mimi iko hapa kama itakapotokezea muhasibu yule kafanya makosa inabidi aondoshwe katika nafasi ile, je ule mshahara itabidi aondoke nao au utabakia pale. Maana yake ule mshahara kapewa Muhasibu Mkuu, sasa yeye anaondoka, ataondoka namshahara wake au inakuwaje. Nilikuwa nataka maelezo katika hili Mhe. Waziri anisaidie ili nipate ufafanuzi kidogo.

Mhe. Spika, mimi nilikuwa nina wazo vile vile kwamba ni vyema mishahara ile angeisitisha Mhe. Waziri kwa sasa, akatengeneza posho la kushika wadhifa pale, ikawa kwa yeyote yule ambaye anakuja pale kama ni Muhasibu Mkuu wa wizara analikuta lile posho, na akiondoka anaondoka na mshahara wake lile posho analiwacha. Kwa hivyo, yeyote yule atakayeteuliwa katika nafasi ile, atakwenda kulikuta lile posho atalitumia na akiondoshwa ataondoka yeye tu na ule mshahara wake wa kawaida, kuliko kumpa mshahara wa namna hii kwa sababu ya cheo cha Muhasibu Mkuu. Maana yake akiondoka na mshahara itabidi aondoke nao. Sasa je watakapotokezea watano au sita au kumi wanaharibu waondoshwa itakuwaje. Mimi nahisi hii sio sahihi.

Kwa hivyo, wazo langu Mhe. Waziri ungetengeneza posho kwa ajili ya kushika wadhifa pale, hata kama utalitononosha kidogo likawa zito, ili kila anayeshika wadhifa ule akalipata, lakini anapoondoka anaondoka na mshahara wa kawaida.

Mhe. Spika, kwa sababu ya muda umenipa haraka nisogee katika ukurasa wa 32 kwenye Idara ya Uhakiki Mali na Mitaji ya Umma. Mhe. Spika, mimi nina maswali mawili au matatu kidogo katika idara hii. Kwenye sheria ya manunuzi na ufutaji wa mali za serikali nambari 9 ya mwaka 2005 inaonekana kushindwa sheria hii kufanya kazi zake kwa ufanisi, kutokana na kasoro nyingi zilizojitokeza. Sasa mimi nilikuwa nataka kujua je, ni lini sheria hii itafanyiwa mapitio ya kina ili iweze kukidhi mahitaji ya serikali.

Mhe. Spika, vile vile nilikuwa nataka kujua idara hii ina majukumu mengi iliyowekewa na serikali ili kuhakikisha matumizi ya fedha za umma katika manunuzi zinakwenda vizuri na kwa uwazi. Je, Mhe. Waziri hatuoni kuwa idara hii kuichanganya na Idara ya Mitaji ya Umma kunapunguza ufanisi katika kutekeleza kazi zake za kila siku. Pia huoni kuwa ni vyema tukazibagua zikawa, hii idara hii ikawa inajitegemea wenyewe badala ya kukaa chini ya mitaji ya umma, ili iweze kufanyakazi zake vizuri. Ushari wangu ni kwamba tuibaguwe idara hii ikawa tofauti na mitaji ya umma, kwa sababu itakapokuwa peke yake itaweza kufanyakazi zake zila ambazo zimekusudiwa, kuliko kuwa chini ya mitaji ya umma, nahisi hapa haiwezi kufanyakazi zake vizuri zaidi.

Mhe. Spika: Muda Mhe. Mjumbe.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Ahsante Mhe. Spika, namalizia moja hilo. Mhe. Spika. Kwenye *section seven* ya sheria ya manunuzi ya ufutaji na mali za serikali idara ya uhakiki mali inatakiwa kuwasilisha kwa waziri wa fedha na kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ile *Annual Performance Evaluation Report,* za kila mwaka zinatakiwa kuwasilishwa pale. Kwa hivyo, nilikuwa nataka kujua tu sijui katika kipindi hiki cha miaka miwili idara hii imewasilisha *report* kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali mara ngapi na *report*

zile kama zipo, basi ilikuwa Mhe. Waziri pia ikiwezekana anisaidie nione ili niweze kujua ufanisi wa kazi unaofanywa na idara hii.

Mhe. Spika, kwa kuheshimu muda wako na unavyonihimiza sana, basi mimi nimalizie hapo kwa kumuunga mkono Mhe. Waziri katika hotuba hii kwa asilimia 90, zile asilimia 10 naziacha kidogo atakavyokuja kunipa ufafanuzi wa aya basi nije nimmalizie ile asilimia 10 yake iliyobakia. Mhe. Spika, nakushukuru ahsante.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchanhgia hotuba hii muhimu sana ya Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo. Mhe. Spika, wizara hii inakuja kufuatia mjumuiko wa kumaliza bajeti ya wizara zote tulizonazo katika serikali yetu.

Awali ya yote naomba nitumiefu fursa hii basi niwashukuru na kuwapongeza sana Waheshimiwa Wawakilishi wenzangu, kwa namna tulivyochangia bajeti mbali mbali na hatimaye kwa mara ya kwanza inaonekana mara hii tumekuwa *serious* sana katika kuchangia bajeti, kitu kilichopelekea kwa mara ya kwanza kumfanya Mhe. Waziri aweze kutekeleza lile jukumu muhimu sana la kutupatia fedha kwa ajili ya ununuzi wa meli.

Mhe. Spika, lakini zaidi naomba nimshukuru Mhe. Waziri kwa kukubali kwake, kwa usikivu wake na kwa hatimaye akafika kusikiliza maoni ya wawakilishi na tukaweza kusimamia vyema bajeti hii ya serikali.

Mhe. Spika, fedha hizi tunazozizungumza hapa katika bajeti zinasimamiwa na sheria ya fedha ya mwaka 2005, halikadhalika utekelezaji wake unakwenda katika sheria ya manunuzi. Kama alivyosema mwenzangu sheria hizi za fedha, sheria za manunuzi pamoja na kanuni zake, kwa kiasi kikubwa zimedhihirika kwamba zina mapungufu. Sasa kwa kipindi zaidi ya miaka saba tangu sheria hii kuundwa na tukumika, basi imeonekana kwamba zina mapungufu na kwa vyovyote vile ili tuweze kuwa na matumizi mazuri ya fedha yanayokwenda na wakati na kwa mazingira tuliyonayo, basi niungane na Mhe. Mbarouk Wadi Mussa kumtaka waziri atakapokuja kwenye kujumuisha atueleze kuwa ni lini Baraza hili litapokea mswada wa marekebisho ya sheria hizo mbili ambazo zina mapungufu makubwa katika utekelezaji wake. Hii ikiwa ni pamoja na adhabu, kwa sababu sheria yetu kwa kweli haitiwi adhabu.

Mhe. Spika, tumekuwa mara nyingi tukishuhudia namna watendaji wanavyokiuka sheria, lakini sheria inakaa kimya. Pengine kitu kikubwa kinachoweza kutokea adhabu ni kumuhamisha mtumishi, kitu ambacho sio sahihi. Kwa hivyo, tunahitaji marekebisho ya sheria hizi zikiwa ni pamoja na adhabu kwa wale ambao watakiuka na watakwenda kinyume katika sheria hizi.

La pili Mhe. Spika, ambalo napenda nizungumzie kwa ufupi sana, *report* nyingi za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali zinaonesha kwamba mashirika yetu ya umma tuliyonayo hayafungi hesabu. Tafsiri ya shirika kutokufunga hesabu maana yake nini. Maana yake ni kwamba huwezi ukafika pahala ukaona hasa shirika liko vipi, au fedha ziko vipi. Mhe. Spika, leo tunazungumzia mathalani, tunapozungumzia fedha za wafanyakazi zilizoko kwenye ZSSF, lakini ZSSF ikawa haifungi hesabu, maana yake ni kutufanya tukawa hatuna uhakika kwamba fedha zile zipo za wafanyakazi au la. Kwa hivyo, adhari ya mashirika ya kutokufunga hesabu Mhe. Spika, ni kubwa na haitupi picha na sura halisi ya kuoneshea kwamba mashirika haya ama yanakwenda kwa faida ua kwa hasara.

Sasa Mhe. Spika, naomba hilo lizingatiwe katika bajeti hii na katika suala zima la usimamizi wa Mhe. Waziri. Mashirika hayafungi hesabu na kwa kuwa hayafungi hesabu basi hatuna uhakika na kile tunachoambiwa kuwa ni kweli au sio kweli, kama shirika lipo kibiashara au halipo kibiashara. Kwa hivyo, hilo ni moja namuomba Mhe. Waziri atakapokuja aje atupe hakikisho juu ya hilo na sambamba na ule urekebishwaji wa ile sheria, kwamba iwepo *accounting officer* wa mashirika haya ikiwa hakufunga hesabu, adhabu yake vile vile nayo iwepo.

Mhe. Spika, naomba niliipongeze sana Shirika la Bima kati ya yote hayo, kwa namna linavyofanyakazi vizuri na namna ambavyo sasa hivi linajitanua sana katika soko la Bara na hata soko la Afrika ya Mashariki kwamba sasa hivi wanataka kuingia katika suala zima la Bima. Naomba nichukuwe fursa hii nimpongeze kwa dhati kabisa Mkurugenzi wa Shirika la Bima.

Vile vile naomba nizungumzie kuhusu wahasibu. Mhe. Spika, chote tunachokizungumza hapa matokeo yake wahasibu ndio watakaokishughulikia katika suala zima la kuzitumia fedha hizi. Kumejengeka utamaduni wa baadhi ya wahasibu kuendelea kukaa katika vituo vya kazi kwa muda mrefu sana, kitu ambacho kinaleta shaka. Kwa sababu utamkuta muhasibu kakaa pahala mpaka maana yake keshaota na keshafanana na pale pahala, kitu

kinachopelekea sasa hapo mipango na dili nyingi kufanyika dhidi ya fedha hizi. Natoa ombi maalum kwa wizara iwe ina utaratibu yaani iandae utaratibu wa kuwahamisha wahasibu kila baada ya kipindi fulani, hii yote itapelekea kuondokana na ile tabia ya kuzowea pahala na kufanya wanavyofanya.

Mhe. Spika, katika hili niungane na wenzangu waliotaka kama Mhe. Ismail Jussa Ladhu aliyetaka kwamba na waziri na yeye kwa sababu katiba yetu nayo imemtaja Mhe. Waziri kama ndio wasimamizi wakuu wa ofisi. Ukisema wasimamizi wakuu wa ofisi ni pamoja na kuangalia mienendo hii ya fedha. Mhe. Spika, sasa hivi tabia iliyojengekana ni kwamba mawaziri hawana *access* ya kuangalia kilichoingia nakinachotoka huo ndio ukweli na tulifika pahala mpaka makatibu wakuu wenyewe tukaambiwa ni wahasibu tu ndio wanaoweza kuona kinachoingia na kinachotoka. Baadhi ya makatibu wakuu walilalamikia hilo.

Kwa hivyo, tunaomba ule mtandao upelekee mpaka mawaziri nao waweze kuangalia. Kwa sababu huo ndio usimamizi wa wizara, ikiwa waziri hawezi kuangalia kinachoingia na kinachotoka usimamizi wake uko pahala gani, wakati yeye ndiye anayekuja kusimama mbele ya Baraza hili na kuomba fedha, lakini sasa kwa nini awe hana *access* ya kuangalia namna mwenendo wa fedha zinavyokwenda.

Jengine naomba Mhe. Spika, nizungumzie *fixed assert register*. *Report* nyingi za mdhibiti zinazungumzia kwamba hakuna *fixed assert register* katika taasisi zetu. Mhe. Spika, tukumbuke kwamba hiki tunachokipitisha hapa zaidi ya nusu kinakwenda katika manunuzi, fedha hizi zinaingia katika manunuzi au zinaingia katika matengenezo ya hizo mali za serikali. Sasa na mali yeneyewe hazina kumbukumbu katika serikali, kitu ambacho kwa kweli tunapitisha fedha hapa ambayo hatujui hatima yake ni kitu gani. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kwa hili.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri mwaka jana katuomba fedha kwa ajili ya kutengeneza *fixed assert register*, sijui mwaka huu kafanya nini katika hili, kwa sababu kama kuna kitu ambacho kinahitajika kifanyiwe kazi haraka basi hiki. Mhe. Spika, juzi hapa Mhe. Hija Hassan kaleta hoja kwamba kuna maghala hayajulikani mwenyewe ni nani. Ni kitu cha aibu kwa serikali, tunafika pahala mali ya serikali haijulikani mwenyewe ni nani, sasa ikiwa yeye kayaona mawili je, kuna mangapi ambayo hayajulikani mwenyewe ni nani. Yote hiyo ni kutokana na kwamba hakuna *fixed assert register*, kitu kinachopeleka mali za serikali kupotea ovyo ovyo na wajanja wachache kuweza kuzimiliki mali hizi za serikali.

Mhe. Spika, lakini katika hilo hilo la kuwa na buku la kumbukumbu za mali za serikali, kuna suala zima la uuzwaji wa mali chakavu. Mhe. Spika, tunapokuwa na mali maana yake baadae mali zile zinakwenda kuwa ni chakavu. Sasa moja kati ya *assert* ya serikali ambayo inaweza ikarudisha tena fedha ile ikaingia katika mzunguko, fedha ikarudi tena katika serikali ni namna ya uuzwaji wa mali chakavu. Sasa inaonekana kwamba bado hakujawa na *formula* maalum ya kuuzwa mali chakavu hizi.

Mhe. Spika, wakati sasa umefika Mhe. Waziri sisi tuko hapa kwa ajili ya kukusaidia wewe. Tumekula mkataba baina ya wawakilishi na wewe ili sisi tukusaidie kwamba katika pahala ambapo kuna fedha nyingi sana ambazo hupotea ovyo ovyo, basi ni katika suala zima la kuuzwa hizi mali, ambapo mali hizi huuzwa katika njia ya mizengwe tu na kwa utaratibu uliokuwa haufahamiki.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri katika mipango yake aweke mpango maalum, hatuhitaji sisi kuwa na mali chakavu, mali iliyokuwa tayari imeshakuwa chakavu maana yake iuzwe ili fedha ile irudi serikalini kwa njia nyengine. Kwa hivyo, na hili naomba Mhe. Waziri katika mipango yake ya kazi aliandalie utaratibu mzuri kwamba katika wizara mali ikishaonekana kuwa hii haihitajiki tena muda wake umeshamalizika, maana yake itolewe ili fedha ile ndogo iliyopatikana irudi tena katika mzunguko wa fedha za serikali.

Mhe. Spika, jengine ambalo nataka kuzungumzia ni suala zima la uimarishaji wa mfumo wa ulipaji kodi. Tuna tatizo na bado tatizo linaendelea na inaonekana bado serikali haijaandaa hasa au haijakuwa makini sana kuandaa suala zima la ukusanyaji wa kodi. Tunachokihitaji sasa katika kodi ni kuwe na *one stop center* ya ulipaji wa kodi na ikiwezekana mambo yale ya kulipa kodi kwenye mikoba na kwenye mifuko, sasa hivi imeshapitwa na wakati, watu wote waende kulipa kodi pahala pamoja panapotambulika. Kila aliye na chake katika kodi ile basi aweze kuipata kodi ile kwa njia ambayo itawekwa. Kwa hivyo, naomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa atueleze ni namna gani serikali imejipanga katika kuhakikisha kwamba tuna-*strengthen* mfumo wetu wa ulipaji wa kodi, ili kodi zote ziingie serikalini.

Mhe. Spika, takriban robo ya kodi zinazo kusanywa hazifiki serikalini, zinaingia katika mifuko. Naomba hili nilirudie tena kwa umuhimu wake. Mhe. Spika, kodi zinazolipwa kwa ajili ya serikali, hazifiki serikalini zinaishia kwenye mifuko ya watu wachache. Sasa kama hilo tumeshalifahamu, je ni nini mpango wa serikali kuona kwamba hilo chaka tunaliondosha, kuna kitu gani kinachoshindikana katika hilo. Naomba Mhe. Waziri atakapokuja aje atueleze namna serikali ilivyojipanga katika kuimarisha suala zima la ulipaji wa kodi, ili kwa asilimia 100 zifike pale zilipokusudiwa.

Mhe. Spika, kitu chengine ambacho nakusudia kukizungumza Mhe. Spika, kwa ufupi sana ni suala zima, tumeona katika bajeti hii tulipokuwa tunazungumzia katika wizara tofauti. Mfumo wa bajeti yetu ya serikali ina tofauti baina ya wizara na wizara ni lazima tufike pahala tuwe na mfumo mmoja wa bajeti. Leo kuna wizara utakuta kwamba zina mafungu madogo madogo katika kisiwa cha Pemba. Lakini kuna wizara mpaka sasa hivi hazijaingia kabisa. Hili kosa sio la hizi wizara, kosa liko katika Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, wao kwa sababu ndio wanaoandaa bajeti.

Mhe. Spika, leo inafika pahala waziri yeye mwenyewe huyu anataka na huyu hataki. Mimi nadhani hiyo sio sahihi. Hili pungufu liko katika wizara yako Mhe. Waziri wa fedha katika idara yako ya bajeti ni lazima tuwe na *format* moja tu ya kuandaa bajeti. Hii athari yake Mhe. Spika, tumeona hata *report* za mdhibiti zinapojitokeza, mara nyingi kamati yako inapokwenda Pemba kufuatia hoja ya mdhibiti, Pemba kule wenzetu hutujibu kwamba hilo sisi hatulielewe, hoja iko Pemba lakini matumizi yale yamefanywa Unguja, kwa sababu Pemba hakuna kifungu kilichopeleka fedha ile, kifungu chote kiko katika makao makuu ya wizara. Kwa hivyo, tunaomba na hili Mhe. Waziri unaliweza, naamini kwamba unaliweza. Tukijaaliwa bajeti inayokuja ya mwakani tunataka tuone bajeti yote ya serikali, wizara zote za serikali zinakuwa na *format* moja tu ya kushughulikia bajeti.

Mhe. Spika, kitu chengine kwa ufupi, katika kitu kinachoathiri uchumi wetu ni fedha haramu. Mhe. Spika, fedha haramu Zanzibar zipo na zinaingia mara kwa mara na bahati mbaya sana kwamba taasisi nyingi au wafanyabiashara wengi hawana mashine hizi zenye kugundua hizi fedha. Maana yake wafanyabiashara wengi huangalia noti kwa kuzipapasa papasa tu, aliyena utaalamu hupapasa tu. Mhe. Spika, mimi kuna siku nilikwenda kupeleka pesa pahala fulani, mfanyabiashara alipoiona tu akaniambia hii sio, kwa bahati nzuri akanionea huruma hakunichukulia hatua, lakini aliniambaia hii sio. Je, ni wangapi wenye utaalamu ule. Kwa hivyo, mzunguko wetu wa fedha huathiriwa na fedha hizi haramu. Ninachoomba katika hili wizara iandae utaratibu maalum wa kutafuta hizi mashine na kuwagaiya wafanyabiashara, kwa sababu fedha zikishaingia kwenye mzunguko hata ukenda kuzingundua benki, watu wa benki wao watazingudua, lakini itakuwa tayari mfanyabiashara keshaingia hasara. Kwa hivyo, serikali inamlindaje huyu mfanyabiashara.

Mhe. Spika, mimi nadhani sasa hivi wakati umefika serikali kuandaa utaratibu kama ni wakuwatumia wafanyabiashara binafsi kuzisambaza mashine hizi, ili kuweza kupambana na mfumo huu wa fedha haramu.

Mhe. Spika, karibu ya mwisho nataka niseme, kwa sababu naona unaniangali. Mhe. Waziri wizara yako na wewe mwenyewe binafsi ndio mwenye dhamana hasa wa kuzi- *respond* yale mapendekezo yanayotokana na *report* za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kupitia *report* ya *PAC*. Mara nyingi sana Kamati yetu ya Kuchunguza na Kudhibiti Mahesabu ya Serikali, inawasilisha mapendekezo kadhaa wa kadhaa hapa lakini ni bahati mbaya sana hatujaona serikali kuchukua hatua juu ya mapendekezo ya *PAC*. Kutokuchukua hatua na kutokuyafanyia kazi mapendekezo ya kamati ile Kuchunguza Hesabu za Serikali, kwa kweli ni kufika pahala tukaona kwamba tunazipoteza fedha za wananchi nyingi ambazo zinatumika katika kazi hiyo.

Vile vile hata ofisi ya mdhibiti uwepo wake nao unakuwa na mashaka. Kwa sababu mdhibiti anafanyakazi baadae *report* zinaletwa katika Baraza hili na Baraza kwa kupitia kamati inafuatilia. Kwa hivyo, tunataka tuone Mhe. Spika, nashukuru Baraza lako tulipitisha na mara hii katika kikao cha April, kwanza kabisa mawaziri watakuja kuwasilisha hapa namna walivyopokea mapendekezo ya kamati zao, ikiwa ni pamoja na wizara ya fedha watakavyo- *respond* kwenye mapendekezo ya kamati. Naomba nisisitize tu kwamba hili jukumu ni la wizara ya fedha, kuona kwamba mapendekezo ya kamati ya Kuchunguza Hesabu za Serikali yanafanyiwa kazi kwa ukamilifu wake na taarifa kuletwa mbele ya Baraza letu hili.

Mwisho kabisa Mhe. Spika, naomba nielezee umuhimu wa mwezi huu wa Ramadhani kwa Waislamu na kwa Wazanzibari kwa ujumla. Mwezi huu ni muhimu sana na ndio mwezi wa kuchuma. Mhe. Omar Yussuf hapa tayari yeye ni Al Hajji na Rais wetu ni Al Hajji waongeze bidii na Mhe. Spika, na wewe ni Al Hajji. Kwa hivyo, hiki ni

kipindi cha kuchuma, naomba nitowe ombi kwa serikali. Wenzetu katika nchi zile zinazoamini kuhusiana na suala la Christimas, basi kikifika kipindi cha Christimas huwa ni siku kubwa sana na baadhi ya watawala au viongozi katika nchi hiyo hutoa ofa maalum kwa ajili ya wafanyakazi katika nchi hizo zenye Chirstimas. Sisi mwezi wetu mtukufu ni huu wa Ramadhani.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, katika nia ile ile ya Rais wetu kutaka kumuombea apate daraja kubwa katika pepo na waziri wetu huyu na Spika wetu huyu kupata daraja kubwa katika pepo, basi natoa ombi maalum kwamba inawezekana na hii inawezekana ikiwa tumpata pesa za meli na kwa hili kwa nini tusipate. Serikali itenge ofa maalum ya mishahara kwa ajili ya wafanyakazi katika kipindi hiki cha mwezi wa Ramadhani, hili linawezekana japo nusu kati ya mshahara kamili na nusu ya mshahara, wafanyakazi wapewe kwa sababu huu ndio mwezi wao. Ramadhani hii inakuja pamoja na sikukuu, nasema tena kwamba hilo linawezekana ni suala la nia tu. Naamini Mhe. Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo nia hiyo anayo alininong'oneza na hata Mhe. Rais naamini na yeye hili atalikubali, ili tuone kwamba tunawatengenezea bustani nzuri katika akhera yao watakapokwenda. Mhe. Spika, nakushukuru ahsante sana.

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Spika, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametuwezesha siku hii ya leo kufika katika hali ya uzima. Vile vile nikushukuru wewe binafsi kwa kunipatia nafasi hii, kwa vile wakati nitakuwa sina basi naomba niende moja kwa moja Mhe. Spika.

Kwanza nichukue nafasi hii nimpongeze sana Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo pamoja na watendaji wake wote kwa jinsi walivyoandaa kitabu hichi, ambacho kinaeleza kwa kina tena kwa ufasaha zaidi. Lakini penye mazuri mabaya hayakosi.

Mhe. Spika, mimi nitamuwaidhi tu Mhe. Waziri na kwa sababu Mhe. Waziri ni msikivu kwa mambo yake yote ambayo anayoambiwa na Wajumbe wa Baraza lako hili Tukufu na kuyachukua kwa kuyafanyiakazi ipasavyo pamoja na watendaji wake.

Kwa hivyo, nitamuomba sana Mhe. Waziri katika Idara hii ya Uhakiki Mali na Mitaji ya Umma. Mhe. Spika, utaniwia radhi naomba ninukuu kidogo tu.

"Idara ya Uhakiki Mali na Mitaji ya Umma, ina jukumu la kusimamia mali za Serikali, ikihusisha ununuzi, utunzaji na uondoaji wake, mali hizo ni pamoja na majengo, vifaa, mitambo, mashamba na zana mbali mbali. Kwa upande mwengine idara pia ina jukumu la kusimamia mitaji, hisa na uwekezaji wa rasilimali katika mashirika na kampuni za umma binafsi".

Mhe. Spika, nitamuomba sana Mhe. Waziri kwamba idara hii ni muhimu sana, kwa sababu idara hii ina mambo mengi ambayo yanawagusa wananchi wake.

Kwa hivyo, na mimi nitilie mkazo suala alilolizungumza Mhe. Mbarouk Wadi Mussa, kwamba kama kuna sheria ambayo imeshapitwa na wakati, basi Mhe. Waziri tuletee sheria hapa tuipitie na kama kuna mambo ya kuyasawazisha tuyasawazishe. Kwa maana hiyo, lazima tukubali mambo yanayojitokeza humu yanawahusisha na yanatija kwa watu baadhi ya watu binafsi. *(Makofi)*

Sasa naomba nizungumzie kuhusu usimamizi kwa upande wa mawaziri. Mhe. Spika, nitawaomba Mawaziri wote kwa jumla kama walivyoona tulivyowahenya kipindi hichi, basi kipindi kinachokuja cha mwaka 2013/2014 ndio itakuwa aghasi kama maelekezo ambayo tumetoa hayakutekelezwa.

Lakini na hapa kabla sijamaliza namuomba Mhe. Waziri kwamba mimi nitaiunga mkono hii hoja, isipokuwa ninalo neno moja tu, katika kuchangia Wizara ya Nchi, (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ya Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini, nilisema kwamba kuna watu hawajapewa *arrears* zao na Mhe. Waziri aliniambia kwamba *voucher* zimeshapigwa na ziko.

Mhe. Spika ninavyokwambia mpaka leo fedha hizo na nitakuja kuzuia kifungu, kwa sababu wewe ndiye Waziri ambaye unahusika mpaka unihakikishie kwamba fedha hizi zitawafika walengwa na hasa kipindi hichi cha Sikukuu na Ramadhani, lazima tuwaonee huruma wananchi ambao ni haki yao. *(Makofi)*

Kutokana na hali hiyo, Mhe. Waziri hapa mimi na wewe nitauwacha udugu na udada huko nyuma na hapa nitataka jawabu sahihi, kwa sababu juzi nilizungumza na Mhe. Waziri na akaniambia hawajapewa au vipi basi ngojea, mimi mambo yangu ndio ninasema kama hivi. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Spika, naomba nichukue nafasi hii nimpongeze sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohammed Shein kwa maamuzi ambayo ameyachukua kwa ajili ya ununuzi wa meli. *(Makofi)*

Kwa kweli ni imani yangu kubwa sana kwa Mhe. Waziri huyu ambaye tunaye Mwenyezi Mungu atampa nguvu kwa sababu ni jambo la heri na *Inshallah* Mwenyezi Mungu atakupa uwezo wewe na watendaji wako kutafuta mbinu za kutafuta fedha za ununuzi wa meli, ili wananchi na wao watokane na sulubu ambazo zimewafika katika vipindi tofauti, namuombea kila la heri Mhe. Waziri. *(Makofi)*

Vile vile nichukue nafasi hii nimshukuru tena Mhe. Rais na nimuombe Mhe. Waziri kwamba alitoa msamaha hapa kwa mama wajawazito. Kwa hivyo, nitakuomba sana kwamba fedha hizi zisicheleweshwe kupelekwa Wizara ya Afya, kwa sababu ni msamaha ambao ameutoa na kusema kuwa atafidia yeye, basi ninamuomba sana Mhe. Waziri kwa sababu matatizo yanayowafika akinamama wajawazito ni makubwa sana. Kwa hivyo, nitamuomba sana Mhe. Waziri fedha hizi zisicheleweshwe, ili ziwafikie Wizara ya Afya kwa wakati. *(Makofi)*

Jambo jengine Mhe. Spika, nimuombe Mhe. Waziri kwamba niunge mkono maneno aliyoyasema Mhe. Omar Ali Shehe kwamba huu ni Mwezi Mtukufu wa Ramadhani ni Mwezi wa Toba, naomba na huko nyuma yalikuwa yanatendeka hayo, naomba sana nimuunge mkono Mhe. Omar Ali Shehe na kwa uwezo wako ninavyojua utayafanya mambo haya, ili wananchi wetu na wao wajisikie kwamba serikali yao imewathamini katika Mwezi huu Mtukufu wa Ramadhani.

Mhe. Spika, jengine ninamuomba Mhe. Waziri kuna Benki ya Akinamama, lakini imekuwa ni kama wimbo. Kwa hivyo, ninakuomba hii Benki ya Akinamama uiharakishe, kwa sababu kama unavyojua kuwa wanawake ndio wenye majukumu makubwa zaidi kwenye familia. *(Makofi)*

Lakini nitaomba Benki hii iende sambamba na Benki ya Kilimo tuanzishe na Benki ya Kilimo, kwa sababu Benki ya Kilimo nayo ndio itasabisha yale matatizo yote kuweza kuondoka kwa wakulima wetu kwa mambo madogo madogo. Kwa maana hiyo, nakuomba sana Mhe. Waziri kwamba suala hili ulizingatie, ili nalo liende sambamba na Benki ya Akinamama. *(Makofi)*

Mwisho Mhe. Spika, nichukue nafasi hii niwapongeze Waheshimiwa wote Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, kwa jinsi walivyolichangamsha Baraza hili na kutekeleza majukumu pamoja na wajibu wao katika shughuli zetu za kitaifa. *(Makofi)*

Lakini nitakuwa mwizi wa fadhila Mhe. Spika kama sikukupongeza wewe binafsi, kwa jinsi unavyotuvumilia katika Baraza lako Tukufu, kwa sababu tunakuwa wakali na wakati mwengine hatuelewani humu. Kwa kweli kutokana na busara na hekima zako unajaribu kama unavyoweza kuhakikisha kwamba Baraza hili linakwenda kwa mujibu wa taratibu na sheria ambazo sisi wenyewe ndio tuliozipitisha. Kwa hiyo, niseme nikutakie kila la heri pamoja na familia yako, kwa sababu ndio tunamaliza kipindi cha mwaka hichi. *(Makofi)*

Vile vile niwatakie kila la heri Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi na wananchi kwa jumla. Pia napenda kutoa wito tarehe 26/08/2012 tuhakikishe tunakaa majumbani, ili kujiandikisha katika Sensa ya Watu wa Zanzibar. Baada ya hayo, ahsante sana Mhe. Spika. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, tunakushukuru. Sasa tumkaribishe Mhe. Hija Hassan Hija na baadaye Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uhai na uzima. Pia nikupongeze Mhe. Spika kwa jinsi unavyotuongoza katika *speed* ya gari nzito na najua ni kutokana na muda ambao kwa kweli umetupana.

Mhe. Spika, nimpongeze Mhe. Waziri kwa jinsi alivyowasilisha bajeti yake na mimi kwa niaba ya wananchi wa Kiwani sina wasi wasi yale yote ambayo Waheshimiwa Wawakilishi wamemwambia atayazingatia kwa upeo wake na yuko tayari kuyatekeleza, kwa sababu hajawahi kutukatalia wala kufanya ukaidi katika Baraza hili.

Mhe. Spika, jambo la mwanzo ambalo nataka nizungumze ni kuhusu Mfuko wa Hifadhi ya Jamii. Kwa kweli mfuko huu unaongozwa na sheria ambayo imepitishwa na Baraza la Wawakilishi, lakini ukweli ulivyo inaonekana kwamba sheria hii imekuwa ni kikwazo kwa wafanyakazi wetu wa Unguja na Pemba.

Kwa mfano, juzi Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania siku ya Jumanne baada ya kuzikiliza kilio cha Wabunge na wananchi ambao ni wafanyakazi wa Tanzania, iliamua kurekebisha Sheria ya Mfuko wa Hifadhi.

Kwa hivyo, nachukua nafasi hii Mhe. Spika kumuomba Mhe. Waziri akubali kwamba Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar irekebishwe, ili mfanyakazi pale ambapo anastaafu aweze kupata haki yake. Mhe. Spika, wapo wafanyakazi ambao wanafanyakazi kwa muda wa miaka saba, lakini wanaambiwa wasipate maslahi yao hadi miaka 60 kwa mujibu wa sheria.

Kutokana na hali hiyo, nimuombe Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, kwa huruma alizonazo pamoja na uwezo alionao wa kuwapenda Wazanzibari, basi hili alizingatie na sheria ibadilishwe, ili wafanyakazi wa Zanzibar waweze kupata haki yao mara pale wanapostaafu.

Jambo jengine ambalo nataka nizungumze ni kuhusu suala la fedha ambazo zimetengwa kwa ajili ya ununuzi wa meli. Mhe. Spika, mimi niunge mkono moja kwa moja kwamba vyanzo vyote ambavyo Mhe. Waziri amevipendekeza kwa ajili ya kupunguza fedha, ili tupate kununua meli basi naunga mkono kwamba ni vyanzo sahihi na tuviunge mkono vipunguzwe.

Lakini nimkumbushe kwamba tulikubaliana kwenye Hotuba ya Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwamba kuna fedha za maendeleo za Mradi wa Mboga Mboga Bambi shilingi milioni 300/=. Mhe. Spika, tulikubaliana kwamba kwa sababu tulitenga shilingi bilioni 1,000,000,000/= na wala haikufanya la maana na fedha hii shilingi milioni 150,000,000/= pale iondoshwe na iingizwe kwenye fungu hili, ili mfuko wa kununua meli uweze kutuna.

Kwa kweli shilingi milioni 150,000,000/= kuipeleka kwenye Mradi wa Mboga Mboga, mradi ambao umefeli zaidi ya shilingi bilioni 100,000,000,000/= zimekwenda pale. Mhe. Spika, tulimshauri Mhe. Waziri kwamba hili alikubali na fedha ile aipunguze na iende kwenye fungu hili la ununuzi wa meli kwa ajili ya kuwatetea wazanzibari wanyonge. Mhe. Spika, imani yangu kwamba Mhe. Waziri hili atalizingatia na fedha ile itaondoka moja kwa moja kwenye Mradi ule wa Mboga Mboga, mradi ambao hauna ufanisi.

Mhe. Spika, jambo jengine haraka haraka ili nitumie dakika tano na nitoe nafasi ni suala zima la malalamiko ya wananchi kuhusu *TRA* na riba za mabenki. Mhe. Spika, mimi nadhani tusimlaumu Mhe. Waziri katika hili hata tumpe miaka 40, wakati tunalo tatizo la sheria kwenye Muungano, basi hana uwezo wa kusaidia.

Mhe. Spika, nadhani wakati sasa wazanzibari kuamua kurekebisha Katiba iliopo kama ambavyo wananchi wanatoa maoni, ili tuondokane na tatizo hili la Muungano, ambapo Muungano unakandamiza uchumi wa Zanzibar. Kwa hivyo, nafikiri wazanzibari hili wameliona na wako tayari kujinasua kwenye makucha haya ya udhalilishaji ndani ya miaka 48.

Jambo la mwisho kabisa ambalo nataka nizungumze ni ubadhirifu wa fedha mbali mbali za umma Mhe. Spika juzi nilipozungumza kwenye Hotuba ya Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko, nilimwambia Mhe. Waziri kwamba nitamsaidia pia kumwambia kuwa kuna fedha za umma zinaharibiwa chini ya wizara yake.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri amekuwa akituambia kwamba tumsaidie na sisi kama ni Wawakilishi basi tuko tayari kumsaidia pale ambapo tutabaini kuwa kuna ubadhirifu wa mali na fedha za umma ndani ya serikali na hususan ndani ya wizara yake.

Vile vile Mhe. Hamza Hassan Juma amezungumza hapa asubuhi kwamba kuna malalamiko pamoja na tetesi kuwa *PBZ* inaendelea kuhujumiwa, yaani inaendelea kuibiwa na wajanja wachache, ambao kwa kweli wamejipanga

kwenye kazi hiyo ya kuidhalilisha benki yetu. Mhe. Spika, chaka kubwa ambalo wajanja wanatumia ni chaka la mishahara ikiwemo viinua mgongo.

Sasa kama watu wanaiba kupitia mishahara na viinua mgongo maana yake na Wizara ya Fedha inahusika, kwa sababu fedha hadi inafika benki kwa maana ya kuibiwa basi maandalizi yatakuwa yametoka Wizara ya Fedha. Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Waziri awe makini sana wakati wa kuandaa mishahara na maslahi ya viinua mgongo ndani ya wizara yake.

Mhe. Spika, mimi ninayo *document* ambayo sitaki niisome. Lakini nataka nimwambie Mhe. Waziri aniambie basi kuna wafanyakazi wanne wa *PBZ* tumeambiwa kwamba wako nje ya kazi. Kwa hivyo, mimi anisaidie tu kwa nini wako nje ya kazi, pia atuambie basi wanakosa gani hadi wizara yake ikaamua kuwaweka nje ya kazi. Mhe. Spika, nasema hivyo kwa sababu ninayo *document* ambayo baadaye itanisaidia kwenye kuzuia fungu iwapo Mhe. Waziri ataamua kunijibu visivyo sahihi.

Kwa maana hiyo, anisaidie wafanyakazi hao wanne ambao wizara yake imewasimamisha kazi wanakosa gani hadi Wizara ikaamua kuwatoa ndani ya *PBZ*, ili wazanzibari pamoja na Baraza lako Tukufu Mhe. Spika waweze kujua ukweli ulivyo kwa nini wafanyakazi hao wamesimamishwa kazi kwa ajili ya kuitetea Serikali yetu.

Mhe. Spika, la mwisho kabisa Mhe. Waziri nimpongeze kwa niaba ya wizara yake Mkurugenzi wa Shirika la Bima la Zanzibar kwa jinsi alivyojipanga na kujitanua kwa ajili ya kutafuta Soko la Bima Tanzania. Mhe. Spika, hivi sasa tunashuhudia Shirika la Bima limejitawanya maeneo ya Arusha, Mwanza, Mbeya na Dodoma na bila ya shaka Mhe. Waziri hatalibana atalipa nyenzo zaidi na kulisaidia, ili litembee katika kanda zote za Tanzania Bara na Zanzibar, kwa lengo la kuongeza mtaji wake Shirika la Bima.

Mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kiwani, nimpongeze Mkurugenzi kwa niaba ya wizara yake kwa ajili ya kujitanua katika Soko hili la Biashara ya Bima. Kwa kweli ni biashara ambayo shirika letu limekuwa likifanya vizuri mara zote.

Mhe. Spika, baada ya hayo na Mhe. Waziri ni swahibu wangu na akinipa majibu mazuri kuhusu wafanyakazi wanne wa *PBZ* waliosimamishwa, basi nitaunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, ahsante. Mwisho kabisa kwa leo na nikimuomba radhi sana Mhe. Hamad Masoud Hamad, naomba nimkaribishe Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali. *(Makofi)*

Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali: Mhe. Spika, kwanza kabisa nachukua nafasi hii sote kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa afya na kuendelea na Baraza letu hili ambalo tuko ukingoni.

Mhe. Spika, napenda kuchukua nafasi hii pia kumpongeza Mhe. Waziri kaka yangu Mhe. Omar Yussuf Mzee pamoja na watendaji wake wote kwa bajeti yao nzuri yenye hekima, busara na usikivu kabisa ambao waliotuandalia. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwa sababu ya muda mimi nadhani nitoe maoni yangu tu pamoja na nasaha kwa wizara hii inayohusika, ambayo ni wizara nzito tena ni nyeti, yaani ni wizara ambayo imebeba wizara zote katika Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kwa hivyo, naomba kutoa ushauri kwa Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, kwamba katika kitabu chake *pages* 18 na 19 kuhusu suala la Mfuko wa Barabara.

Mhe. Spika, nitamuomba kaka yangu kwa heshima zote pamoja na watendaji wake, kwamba huu Mfuko wa Barabara ni fedha za walipakodi, yaani ni fedha ambazo wizara inayohusika inahangaika sana na hali ya uchumi tunaelewa sote. Kwa hiyo, ninaomba wawe waangalifu sana katika suala hili la Mfuko wa Barabara kuhusiana na matengenezo ya barabara zenyewe.

Mhe. Spika, inaelekea hizi barabara zinafanyiwa hujuma na ushahidi upo, yaani hujuma kwa makusudi, kwa sababu Mhe. Spika sioni sababu kwamba barabara imemalizwa leo, barabara moja au kilomita moja ni 1.4 *billion*, yaani kilomita moja tu ya lami na siku ya tatu wahusika wale wa barabara imemalizwa barabara imeshawekwa geraji mafuta, *oil* yanabadilishiwa pale pale, wakati barabara moja imegharimu 1.4 *billion*.

Sasa Mhe. Waziri naomba uwe mkali kidogo pamoja na wizara yako kwa hawa Mfuko wa Barabara, tunapoidhinisha barabara hizi halafu kila baada ya kipindi kuja kufanyiwa marekebisho, inaelekea hapa kitu ambacho kinajenga hisia tofauti. Kwa hivyo, ningeliomba Mhe. Waziri kwamba hizi barabara zitizamwe zilitengenezwa lini, matengenezo yake yanahitajika lini, lakini kwa kweli katika mazingira haya hatutaweza kuisaidia na sisi kama Wawakilishi hatutaweza kuisaidia Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar katika suala zima hili la barabara.

Mhe. Spika, kwa sababu Mhe. Waziri nataka ukae siku moja au watendaji wako wa pwani na mimi kama mfanyabiashara ikiwa nitahusika basi kuwepo na sheria ya kutaifishwa gari, kwa sababu gari inatoka bandarini imepakia nondo, yaani ile nondo inakwaruza barabara mpaka mtu anafika katika eneo hilo.

Mhe. Spika, mimi nasema kile ni kitendo cha uhaini na wala si kitendo cha kawaida, kwa sababu mtu mwenye uchungu na nchi hata ikiwa Raza basi huwezi kuwa mwanahalali ukafanya jambo kama lile na halafu watu wote wakakaa kimya. Kwa hivyo, inatia uchungu sana Mhe. Spika tupo hapa kwa ajili ya kujadili kero za wananchi kwa ajili ya kuwapunguzia umasikini wananchi wetu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri kwa usikivu pamoja na watendaji wake wote katika fedha hizi tunazotoa wawe waangalifu katika barabara ambazo zinazotakiwa kufanyiwa matengenezo.

Mhe. Spika, jambo la pili nawataka wafanyabiashara nikiwemo na mimi Raza tubadilikeni na tuisaidie serikali katika kulipa kodi, kwa sababu kila tukiwa karibu *Alhamdulillah* Mhe. Spika wafanyabiashara tunapata afuweni. Lakini tubadilike angalau tuisaidie serikali yetu katika kuendeleza hizi bajeti ambazo zote zinategemea Wizara ya Fedha katika ukusanyaji wa fedha, yaani kila ukiwa ukusanyaji wa fedha mzuri basi na hizi bajeti ambazo tulizozipitisha hapa zitaweza kupata mafungu yao ya kutosha na kuweza kuziendesha na kutekeleza ile Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi ambayo ndiyo tuliomo humu ndani kupitisha bajeti zetu zote.

Jambo la tatu ambalo nataka kumuomba Mhe. Waziri, ili kuondosha hisia za wafanyabiashara Zanzibar Wizara ya Fedha kwa nia nzuri nawapongeza kutokana na msamaha wa kodi wanaotoa wa chakula kwa sababu ya Mwezi Mtukufu wa Ramadhani na sehemu ambazo wakati mwengine zitahitajika kutokana na upungufu wa chakula, ili kuwasaidia wale walaji.

Kwa hivyo, naiomba wizara inayohusika ikatoa muda mzuri wa kuwataka wafanyabiashara wote kuwapata taarifa ya msamaha kila kinachotokea katika chakula au mambo mengine, ili kusiwepo na manung'uniko kwa sababu nia ni nzuri, lakini jambo ambalo linashtukizia basi kila mmoja anaweza kujenga hoja yake binafsi ambayo sio nia ya Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Hivyo, namuomba Mhe. Waziri kutoa ushauri wangu kwamba mambo kama haya yanapotokea basi wafanyabiashara wote wapate afuweni hii, ili na sisi tupate kuisaidia nchi yetu.

Nikiendelea na mchango wangu Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri kuna maeneo atizame sana ni hii *pay as you earn*. Nadhani tukienda mule katika suala la kodi Mhe. Spika nataka nimhakikishie Mhe. Waziri katika kipindi hichi tunaweza kukusanya *over billion* na Mhe. Waziri ananifahamu nikimwambia hivyo pamoja na watendaji wake katika *pay as you earn* kwa wafanyabiashara na mambo mengine kwa jumla. Kwa kweli humu tunaweza kupata fedha za haraka haraka karibu shilingi bilioni na wataalamu wananielewa ninachosema ambacho kinafahamika.

Vile vile Mhe. Spika, nimuombe Mhe. Waziri suala zima hili la fedha zetu na mgao wetu kwa ndugu zetu Serikali hizi mbili tulizonazo, yaani Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Muungano.

Mimi nafikiri Mhe. Spika, nimuombe Mhe. Waziri imefika wakati kutokana na hali yetu ya uchumi na hapa tupo tunapiga kelele kutokana na umasikini unaotukabili taifa letu, basi nimuombe Mhe. Waziri inaelekea kuna watendaji pale Bara ninahakika wanataka kutuletea vurugu, ili tuone kila mmoja aone kwamba ugumu wa jambo lile na hatimaye tutumbukie katika mambo ambayo wakati mwengine yanatupa tabu sana Mhe. Spika.

Kwa hivyo, naweza kusema kwamba mmoja au wawili na nilitoa mfano Mhe. Spika, kuwa kuna shilingi bilioni 18 ambazo zimeidhinishwa katika kikao halali, ambapo Mhe. Waziri Mkuu ameidhinisha na kwa upande wa Serikali ya

Mapinduzi ya Zanzibar imeidhinishwa na fedha zipo tayari, isipokuwa Mwandamizi mmoja tu wa Bara amezuia fedha. *(Makofi)*

Sasa Mhe. Spika, nimuombe Mhe. Waziri kwamba tuwaombe baba zetu Rais wa Jamhuri ya Muungano, Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar tuwaombe baba zetu wakae kitako, ili haya mafungu ambayo tuliyokuwa tunayapata kwa sehemu zote tupate, kwa ajili ya kuendeleza na kutekeleza hii Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi katika kushughulikia maji, skuli madeski pamoja na mambo yote ya kilimo.

Kutokana na hali hiyo, mimi nimuombe Mhe. Waziri atendekeze *paper* nzuri na tena nataka nimpongeze Mhe. Waziri kwa sababu ninaamini watendaji waliokuwa nao wana uchungu na nchi akiwemo na yeye, tukiwemo na sisi pamoja na serikali, basi naamini Mhe. Waziri akitengeneza waraka mzuri ambao huko nyuma ilikuwa ikifanyika Mhe. Spika, kwa sababu huko nyuma kulikuwa na matatizo.

Kwa kweli nataka nimwambie Mhe. Waziri wa Fedha wakati huko nyuma awamu ya Komandoo Dkt. Salmin Amour Juma kulikuwa na matatizo kama haya yamejitokeza. Lakini nashukuru kwa sababu nilikuwa jikoni Mhe. Waziri kutokana na uaminifu wangu Mhe. Waziri wa Fedha anapofika pahala Mhe. Amina Salum Ali ulikuwa unatengenezwa waraka na kwenda kupewa Rais kumuomba Rais mwenzake wakae kitako kwa ajili ya kulimaliza. *(Makofi)*

Mhe. Spika, mambo kama haya naamini hawa Marais wetu hawaelewi mambo ya ndani yanavyofanyika, kwa sababu anaweza kuwa mtu mmoja tu mkorofi na si kila mwenye kupepesuka ni mlevi. Kwa hivyo, Mhe. Spika nimuombe Mhe. Waziri aandae kitu maalum, kwa sababu kila jambo unazungumza *terms of references* na *issue*.

Kwa maana hiyo, tukienda na *terms of references* pamoja na *issue*, basi naamini Mhe. Rais Kikwete ni msikivu, mwenye hekima, busara, Waziri Mkuu pamoja na wasaidizi wake basi jambo hili tunaweza kupunguza mambo mengi ambapo tuliyokuwa tunakwenda nayo tukapata afuweni, ili tunapokwenda huko tutakuwa tumeshapunguza mambo mengi sana ya manung'uniko yetu ya Muungano tulionao wa kihistoria. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kutokana na muda nisingelipenda uniambie dakika mbili kwa sababu ninaheshimu leo na kwa kuwa nimemaliza na wenzangu ninawaunga mkono. Hivyo, mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Uzini naiunga mkono wizara hii kwa asilimia 110, yaani naiongezea zaidi kwa uaminifu pamoja na uzalendo wa watendaji hawa na Wizara yenyewe inayohusika iliopo hapo. Kwa hiyo, nakushukuruni sana na nakutakieni mafanikio mema Wizara ya Fedha. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, nakushukuru. Kwa hivyo, hapana shaka Waheshimiwa Wajumbe wengine wangetaka kutoa mchango wao, lakini muda hauturuhusu, nikirudia sana kumuomba sana Mhe. Hamad Masoud Hamad kwa sababu na yeye aliomba na nilimtizama muda mrefu kumbe hakuwepo na baadaye ametokezea. Kwa maana hiyo, namuomba radhi sana, basi anaweza kumuandikia Mhe. Waziri baadhi ya maoni pamoja na mchango wake kwa maandishi.

Sasa nimuombe Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo aje kufanya majumuisho. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, kwanza na mimi nataka nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuja kufanya majumuisho katika Bajeti ya Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo. Wahenga wanasema "Mganga hajigangi", kwa sababu kipindi chote nimekuwa nikiwasaidia mawaziri wenzangu, basi ninaimani na leo na wao watanisaidia. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Spika, nataka niwapongeze Waheshimiwa Wajumbe wote wale waliopata nafasi ya kuchangia, waliochangia kwa kusema na wale waliopata nafasi ya kuchangia kwa maandishi. Vile vile nataka niwapongeze wale ambao hawakupata nafasi ya kuchangia, lakini walikuwa na nia nzuri ya kutaka kuchangia bajeti hii akiwemo rafiki yangu mpenzi Mhe. Hamad Masoud Hamad nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nianze kuwataja wale waliochangia kwa maandishi. Waliochangia kwa maandishi walikuwa ni watatu haya wafuatao:-

1. Mhe. Salim Abdalla Hamad.
2. Mhe. Mlinde Mbarouk Juma na
3. Mhe. Wanu Hafidh Ameir.

Mhe. Spika, waliochangia kwa kusema ni kama wafuatao:-

1. Mhe. Salmin Awadh Salmin (Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo.
2. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk.
3. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa.
4. Mhe. Mohammed Haji Khalid.
5. Mhe. Hamza Hassan Juma.
6. Mhe. Subeit Khamis Faki.
7. Mhe. Ali Salum Haji.
8. Mhe. Ismail Jussa Ladhu.
9. Mhe. Abdalla Moh'd Ali.
10. Mhe. Ali Mzee Ali.
11. Mhe. Mbarouk Wadi Mussa.
12. Mhe. Omar Ali Shehe.
13. Mhe. Asha Bakari Makame.
14. Mhe. Hija Hassan Hija.
15. Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali.

Mhe. Spika, maswali, maoni na michango niliyoipata kutoka kwa Waheshimiwa hawa yalikuwa ni 125. Kwa hivyo, nitajitahidi kadri ya uwezo wangu niweze kutoa ufafanuzi yapo mengine yamejirudia kwa Waheshimiwa, lakini kurudia kwake ni kuonesha msisitizo kwamba hili tunakuomba Mhe. Waziri kwa umuhimu wake, ndio maana baadhi ya Waheshimiwa wamekuwa wakilirudia. *(Makofi)*

Kwa hivyo, nianze kwa Mhe. Salmin Awadh Salmin (Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo

Mhe. Spika, Mwenyekiti ameuliza, ametoa ushauri katika mambo mengi kama 18 naomba kwa haraka haraka niyatolee ufafanuzi. Kwanza ametaka mafunzo kwa ajili maafisa wa mipango yasimalizikie ndani ya Wizara tu, yafike katika Mikoa na Wilaya kwa Maafisa wa Mipango. Hili nakubaliana na yeye miya kwa miya na nitalitekeleza katika mwaka huu wa fedha, mpaka maafisa mipango nao wa Wilaya na Mikoa katika kuwapatia mafunzo ili waweza kutekeleza majukumu yao tutawapatia mafunzo hayo.

Pili alilozungumzia ni suala zima la kuwapunguzia kodi wazalishaji wadogo wadogo. Nataka niseme tu kwamba tuna kodi za aina 2, kuna wale wazalishaji wakubwa tumewaweka katika VAT ambao wanatozwa asilimia 18 na wale wengine wadogo wadogo tumewaweka katika *stamp duty* ambao tunawatoza asilimia 3. Lakini bado nitalizingatia hilo ombi lake na tutaliangalia kwa kina hasa kupitia taratibu zetu na vikao vyetu vya sera za kodi. Tutalifanyia kazi na hatimaye tutaona jinsi gani ya kuweza kuwasaidia ili ule mtaji wao uweze kurudi tena faida wanayoipata na kuongeza mitaji yao.

Amesema vile vile wawekezaji kutumia vibaya fursa wanazozipata za misamaha. Hili hata mimi nilipoingia nimeliona. Nataka nikuhakikishie Mhe. Salmin Awadh, hali sasa inapungua na tutaendelea kulifanyia kazi na litakuwa zuri zaidi pale ambapo tutakapoifanyia marekebisho sheria ya ZIPA.

Mhe. Dokta Salmin Awadh Salmin, vile vile alitaka tuweke tarifa sahihi juu ya maendeleo ya mama na mtoto hasa kuanzia katika Shehia hadi taifa. Nimelipokea na tayari jana tu tumekaa na wenzangu pamoja na Kamishna ambaye anahusika na kitengo hiki, jinsi ya kuweka taarifa kuanzia katika Shehia ili ziwe taarifa sahihi na tuweze kuzitumia vizuri zaidi katika maendeleo yetu na katika mipango yetu.

Vile vile amesema utafiti wa watumishi tunaoufanya au utafiti wa watenda kazi uende sambamba na upatikanaji wa wataalamu. Kwa maana kwamba kama inaonekana kuna upungufu wa taaluma fulani katika utafiti ule basi serikali itilie mkazo katika suala zima la kuwapa mafunzo wataalamu wa maeneo yale. Tumelipokea na tayari tumeshawapelekea taarifa wenzetu wa mfuko wa elimu wanaotoa mikopo juu ya zile taaluma ambazo tunaupungufu nazo hapa Zanzibar.

Vile vile nimewaomba wenzangu kwa sababu mawizara nayo yanapesa za kutoa mafuzo za kusomesha taarifa ili wapelekewe Makatibu Wakuu, kuona kwamba ule utafiti basi unakwenda sambamba na hatua zetu za kuwasomesha wataalamu. Tulipokea sana Mhe. Salmin Awadh. Pia ameeleza kwamba bajeti zetu zitumie takwimu halisi na ziwe wazi, akasema hasa akatoa mfano takwimu za utalii. Tumelipokea na baada tu ya kumaliza bajeti yetu tutafanya mkutano wa pamoja baina ya Afisi yetu, Idara ya Takwimu na Kamisheni ya Utalii, tuweze kuona jinsi gani tutaweza kui – *prove* hizi takwimu zetu na kuweza kuzitumia katika mipango yetu na katika mambo yetu mbali mbali ya kitaifa.

Umetuwaidhi kuongeza kasi ya kampeni ya matangazo juu ya Sensa. Nataka nikuhakikishie kasi imeongezeka na itaongezeka zaidi. Ingawa tuna muda mfupi baada ya Ramadhani lakini tumepanga baada ya Ramadhani itaongezeka zaidi. Kwa sababu kuna *activities* nyengine kutokana na nature ya mfumo wetu kwa Zanzibar hatuwezi tukafanya *activities* hizo wakati wa Ramadhani. Lakini kasi imeongezeka, tumewajumuisha wasanii wengi, Makambora tayari, Bi Kidude tayari, Halikuniki tayari, wote hawa wanaitangaza Sensa.

Kwa bahati nzuri na nataka nikupongezeni Waheshimiwa nyinyi wenyewe mmekuwa mkiipongeza Sensa, kwenye majimbo yenu na hapa mmekuwa ukiishajihisha kuitangaza Sensa katika kuchangia kwenye mipango yetu ya bajeti. Nakupongezeni sana na tuendelee kusaidiana katika hili.

Vile vile ameeleza kwamba *program base budgets* ni utaratibu mpya uelezwe vizuri na kila mmoja apate kuufahamu ili apate kuutumia vizuri. Nimelipokea na tutalifanyia kazi, kwa sababu mpango huu ukifanikiwa ile *value for money* tutaanza kuiyona, ile *transparency* tutaanza kuiyona na ule uwajibikaji tutaanza kuuona.

Alitaka tumpatie tathmini katika hizi wizara 6 ambazo tumeanza nazo. Wizara 6 tumeanza nazo na ndio kwanza mwaka mmoja, tathmini unaweza kuipata hasa baada ya miaka mitatu ndio utaweza kuiona tathmini hasa. Lakini uwazi utaonekana na ule uwajibikaji kwa kutumia proramu hii utaweza kuonekana. Nataka niseme tu kwamba wazo, ushauri uliotupa tutaufanyia kazi ili kila mmoja wetu tunapozungumzia *program base budgets* aweze kufahamu tunasema nini.

Mheshimiwa amesema vile vile bado mali nyingi za serikali hazijatambuliwa na hata hizo zilizotambuliwa hazina hati miliki. Suala hili tunalimaliza lini. Nataka nieleze Mhe. Spika, suala hili limeelezwa na wajumbe wengi na hapa nataka nichukue muda kidogo nilizungumze huko mbele Wajumbe waliolizungumza nitalikuwa nalipita tu.

Daftari la mali za serikali, uwekaji wake ni endelevu, kwa sababu serikali inanunua na inauza kwa hivyo kila unaponunua na unapouza unatakiwa uli *up date* lile daftari. Lakini nataka nikuhakikishie zile Wizara sita tulizozianza nazo mali za Wizara hizo au mali walizokuwa wakizisimamia tayari tunazo kwa ukamilifu na tathmini ya mali hizo tayari imeshapatikana.

Mwaka huu tutaendelea na Wizara nyengine lakini hizo sita ambazo zilizokuwa tayari ile *up dating* itakuwa inakwenda kila mwaka wanapouza mali ya serikali inapotolewa na wao watakiwa kuitoa na wanapoingiza mali mpya na wao wanatakiwa kuingiza.

Lakini umeuliza swali la msingi Mhe. Dokta Salimin Awadh na hapa nataka nisema kwamba, baadhi ya mali za serikali ambazo tumeshazitambua bado hazina hati miliki. Mfano tuna shule, tuna vituo vyetu vya Afya. Wizara ya Elimu kwa upande wa Shule wameanza kazi nzuri za kuzitafutia hati miliki. Tumepeleka *responsibility* kwa kila Katibu Mkuu kusimamia sasa atafute hati miliki za hizi mali ambazo wanazozisimamia.

Tumeweza kupata utata mmoja tu lakini tuweza kuushughulikia, kuna baadhi ya wananchi wametoa viwanja ili ijengwe shule. Sasa tunataka kutengeneza hati kwa ajili ya shule yenyewe. Inabidi tukae na wananchi wale ili kuwafahamisha na wao watuelewe nia yetu ya kutengeneza hati. Lakini hili tumesema baadae tutakuja kukaa kwa ukamilifu baina ya sisi na wenzetu wa Wizara ya Ardhi ambao wenye dhamana ya kupima.

Mhe. Spika, inafika wakati na wao wanasema kwamba bajeti yao ni finyu ili tuweze kuona kwamba tunasaidia vipi katika kuweza kuona tunapata hati katika hizi mali za serikali. Bila ya hati tusijidanganye mali ya serikali bila ya hati, hata ya kwako bila ya hati huwezi kuuza, labda umuuzie mtu aliyekuwa hajui. Umuhimu wa kuwepo kwa hati nakubaliana na wewe Mhe. Salmin na Wajumbe wengine waliolizungumzia suala hili, tutalitekeleza kwa awamu.

Sheria ya ununuzi na uondoshaji wa mali za serikali inafaa ifanyiwe marekebisho. Hili limezungumzwa na wengi sana, Mhe. Mtando, Mhe. Dada angu, Mhe. Hamza na wengine. Nimericodi kila suala na kila ushauri uliozungumzwa ni kweli. Tumeshachukua maoni kutoka kwa taasisi mbali mbali ambazo zinazofanya manunuzi juu ya sheria ile. Tayari sasa hivi tunaye mshauri muelekezi anaifanyia kazi. Tukimaliza lengo letu katika mwaka huu wa bajeti marekebisho ya sheria hii tuyalete. Sitokuwa na uwezo Mhe. Spika, kusema kikao kipi lakini nitasema katika mwaka huo wa bajeti.

Mhe. Spika, katika kikao kijacho tayari kuna Sheria, Mwanasheria Mkuu atakuja kuzieleza tuwakuja kuzipitisha katika Kikao kijacho cha mwezi wa Oktoba na kishajaa mimi sina nafasi tena. Lakini katika mwaka huo vikao vinavyobakia tutaileta sheria hiyo ili tuweze kuipitisha hapa na tuone marekebisho yake.

Mhe. Spika, vile vile, nataka niwakaribishe Waheshimiwa Wawakilishi wote kila ambaye atakuwa na maoni juu ya sheria hii au marekebisho fulani aniletee mimi moja kwa moja au anaweza kumpatia Katibu Mkuu wangu tuka *incorporate* marekebisho yake katika marekebisho ya sheria yetu.

Limekuja wazo hapa linzishwe *journal* la *audit* ili wananchi wapate taarifa kamili. Wazo zuri, tutaliangalia na tutaweza kuangalia jinsi gani hili *journal* basi linaweza likaanzishwa. Utaongea na Waziri wa Utumishi kupitia mdhibiti na mkaguzi Mkuu wa Shughuli za Serikali ili liwe zoezi letu la pamoja. Si vibaya kuwa na *journal* na wananchi wakajua.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile ameeleza PBZ itanue mchango wake kwa jamii. Nataka niseme tu kwamba PBZ inatoa mchango kwa jamii inajenga vituo vya Afya, inasaidia katika maji, inasaidia katika shule, inasaidia vile vile katika baadhi ya vituo vya polisi. Lakini tumewataka na sisi waendelee kusaidia zaidi.

ZSSF uwekeze katika miradi mikubwa na ya kisasa. Hilo ndio lengo letu kwamba ZSSF waende katika miradi mikubwa na ya kisasa. Mkurugenzi Mtendaji wa ZSSF ni msikivu, ametusikia na yeye ana hamu hiyo. Tumpe fursa hii na tumpe muda ili aweze kuwekeza katika miradi hiyo. Na sisi tutakuwa pamoja naye katika kumsaidia.

Lakini vile vile wangine wameuliza pamoja na Mwenyekiti wangu maendeleo ya kiwanja cha Watoto, Mhe. Ali Salum vile vile ameuliza. Nataka niseme tu kwamba kiwanja kile sasa hivi ingekuwa tuko mbali, lakini baadaye tulikuja tukagundua ile *process* yote ya kutoa *tender* ilipata misukosuko kidogo ilikosewa. Kwa hivyo kwa mujibu wa sheria ya proquament kama *process* imekosewa lazima ile *process* ui – *cancel* uanze *process* mpya. Tayari tumeshatoa *tender* tunasuri hao watakaoleta *tender* zao tuje tuzifungue ili tuweze kuona kwamba nani ameweza kufanikiwa na ujenzi uwezi kuanza.

Maeneo ya uwekezaji yaimarishwe kwa kuwekewa miundombinu. Tumelipokea na sasa hivi tunataka kuelekeza nguvu zetu hasa katika maeneo yetu haya ya Fumba na Micheweni. Tumekaa muda mrefu sana, kwa hivyo hili tumelipokea, lakini vile vile tutaomba *in put* kama Waheshimiwa Wawakilishi mna ushauri wowote basi tunakaribisha ushauri wenu.

Kuwaendeleza wataalamu wa Chuo cha Fedha cha Chwaka pamoja na kuwatumia kwa tafiti mbali mbali zinazofanywa kwa taasisi zetu za Serikali. Lengo letu kuwaendeleza nimesema katika hotuba yangu, kuna walimu sita wapo wanaofanya PHD na tunataka tuziarifu Wizara zetu na taasisi zetu zote za serikali wakati wanapofanya utafiti katika sekta ambazo chuo hichi zinautaalamu nao basi watumie chuo hichi ili waweze kutusaidia.

Vile vile tumeulizwa hatua tulizofikia juu ya kuanzisha Bima ya Kiislamu (TAQAFUL). Nataka niseme tu kwamba tuko katika hatua nzuri na ndio kwa maana katika bodi ya Bima nadhani tunaye Shekhe kwa jina nadhani ni Shekhe Shamim ili atusaidie hii hali iweze kufanikisha katika kipindi kifupi. Tuko katika mazungumzo na taasisi mbali mbali ili hili suala liweze kukamilika. Litakapokamilika tu Mheshimiwa tutakuja kutoa taarifa kwa sababu tunasema kwamba hii inaweza ikawa ni *product* moja ya shughuli za Bima.

Ufuko wa barabara ujitegemee. Nataka niseme kwamba mfuko wa barabara unajitegemea wala hatuuingilii sisi. Ile fedha wanayoipata nadhani badala ya kuiandika pale kama ruzuku zile fedha ni *transfer* basi tutafanya marekebisho katika vipindi vinavyokuja.

Nilikulizwa swali la mfuko wa pamoja umefikia wapi. Hadi sasa haujaanza, nimekuwa nikilieleza suala hili mara kwa mara kwa upande wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar maoni yake yapo tayari. Lakini nina imani kwa uteuzi wa waziri mpya wa fedha, alipokuja hapa tulilizungumza suala hili. Nina imani kubwa sana waraka ataufikisha kwenye *cabinet* ya Muungano na utapata maamuzi kwa upande wao.

Hili nina imani kubwa sana kana ninavyosema na nitaendelea kusema katika kipindi kifupi tokea Mhe. Rais Dokta Jakaya Mrisho Kikwete amteuwe Waziri wa Fedha, Dokta Wiliam Mgimwa tumekutana mimi na yeye mara sita. Hii ndio ile anayosema Profesa Ali Mzee nia safi, kama nia safi ipo haya mambo tunaweza tukayafanyia kazi. Ile kuonana tu hata kama hamna la kufanya mnywe chai pamoja inatia moyo. Lakini uongozi uliopita ilikuwa shida. Lakini huyu mimi nampongeza na namuombea duwa na namuombea Mungu ampe umri mrefu aendelee kufanya kazi. Ni msikivu, tutaendelea kufanya kazi naye na sio mtu anayedharau ni mtu anayesikiliza ana anayetekeleza.

Kwa hivyo mimi nasema ndugu zangu Wawakilishi tumuunge mkono Dokta Mgimwa ili tuweze kufanya kazi naye. Bado upo uwezekano wa kukusanya mapato zaidi, nimeeleza katika hotuba yangu ya Bajeti ya Taifa. Nimewaona humu baadhi ya wawakilishi ambao mnaweza ukatusaidia kwa maoni, kwa njia, kwa muono. Tutakaa pamoja ili tusaidiane pale panapovuja tutapaziba sote. Hii kodi ni ya wananchi lazima iwasaidie wananchi na sio imsaidie mtu mmoja mmoja. Mimi ni mwenzetu na nakuombeni mnikubali kwa hili.

Mchakato wa bajeti uonyeshe matumizi ya Kasma moja kwa moja katika bajeti ijayo. Mhe. Dokta Salmin tutafanya hili kwa kupitia kwenye Kamati na tumeshatoa maelekezo tayari kwamba katika Bajeti ijayo kila Kamati ni lazima wapate *item by item*, wajue bajeti ile inafanya kazi gani. Kama kuna kifungu kitakuwa, wanazo Makatibu Wakuu wanazo MTF ni kukupeni tu mkaziona, hili si jambo la kuficha watakupeni tu, kama hawajakupeni kwenye meza *demand* watakupa tu. Hili tutalifanya nakuomba Mhe. Mwenyekiti, tusaidiane ili kuweza kulitimiza suala hili.

Mhe. Mwenyekiti, umekuja na ushauri mzuri sana, Chuo cha Chwaka kinapiga hatua. Lakini umekuwa na wasi wasi kwamba kuna tetesi huwenda kikaunganishwa na Vyuo vyengine kwa maana ya Chuo Kikuu cha Zanzibar. Ukashauri kwamba kibaki kama kilivyo. Mawazo yako mazuri na mwengine anaweza akawa na mawazo mengine mazuri. Mimi nataka niseme nasubiri hiyo ripoti ya Kamati. Pengine inaweza ikasema hayo mawazo yako kwamba hiki Chuo kibakie kisiungwe. Ikisema mawazo mengine mimi na wengine wanaotaka hichi Chuo kibakie kama Chuo peke hake tukitetee.

Kwanza kina *discipline* yake peke yake kwa maana ya aina ya masomo wanayosomesha. Sasa hivi duniani jamani Vyuo Vikuu vinakwenda kwenye *specialization*. Utasikia Vyuo Vikuu vinakwenda kwenye *specialization*, utasikia Chuo Kikuu cha *medicine*, utasikia Chuo Kikuu cha Teknologia, utasikia Chuo Kikuu cha Kilimo, hiki kama tunataka basi kibakie Chuo Kikuu cha Fedha. Lakini nasema sitaki nii – *pre empty* ripoti ya Kamati, wacha Kamati ije na ripoti yake, halafu na sisi tuna hoja za kukiacha chuo kiendelee tutatetea.

Tena nawaomba sana Waheshimiwa Wajumbe Wawakilishi waliokuwa hawajafika Chwaka wafike *is a beautifully and marvelous*, ukiitazama dakhalia ilivyojengwa na pesa silizotumika *you could see value for money*. Nendeni na kama kuna mtu anataka kwenda Chwaka hana gari aje anambie miye nitampa gari yangu aende. Tukijenga hoja tujenge hoja nzuri zaidi. Maana yake unajenga hoja baada ya kuona.

Shirika la Bima linafanya kazi nzuri na linafanya faida. Mimi nakubaliana na wewe mwenyekiti na tayari nimeshawambia watu wa bima kwa sababu unatengeneza faida sasa na mimi serikali nataka gawiwo langu anipe. Kwa hiyo tutakaa na Shirika la Bima ili tuweze kuona gawiwo tunaweza kulipata na sisi.

Ujenzi wa Ofisi Pemba, hatujasita lile jengo lililoanguka liko kwa msuluhishi sasa hivi. Mwanasheria Mkuu amefanya kazi nzuri, ameshampatia msuluhishi. Nini serikali ina *demand* inataka kwenye jengo lile. Utaratibu wa kuendelea na kujenga jengo jengine tayari tumeshapata kiwanja Gombani, Wizara tatu tutajengo jengo moja ili tukae pamoja. Wizara ya Ajira, Wizara ya Wanawake na Watoto na Afisi ya Rais Fedha. Tutajenga jengo moja tutakaa pamoja kama wenzetu wengine wamejenga jengo moja Utumishi nadhani na Makamo wa Kwanza wa Rais watakuwa pamoja. Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi anawajua mwenyewe. Bado nia yetu ya kujenga Pemba ipo na katika bajeti hii tunazo pesa kwa ajili ya kuanza ujenzi.

Mhe. Mshimba ametaka kujua katika ripoti yangu au katika hotuba yangu ameeleza kwamba 4.5 hakuiyona. Imo Mheshimiwa kwamba kuna gawiwo la JBS, lile nililolipata ni asilimia 4.5. Kuna gawiwo la BOT lile nililolipata ni

asilimia 4.5 limo na katika hotuba yangu imo na wala usiwe na wasi wasi chini na Komandoo mimi utapata tu haki yako.

Ameuliza je, tunaipata kwa ukamilifu. Nyengine JBS tunaipata zaidi ya makisio ambayo tumeyaweka. Kwa sababu tumesimamia tukaona kwamba add tunayoipata ni *amount* hii, kwa hivyo tutapata zaidi.

Umewapongeza sana ZRB na mimi nawapongeza kwa niaba yao. Na umetaka kodi wanazokusanya TRA sasa zipelekwe ZRB. Wazo sio baya lakini hizi kodi TRA wanazozikusanya nimesema mimi wakati mmoja najibu maswali, zipo kwa mujibu wa Katiba. Sasa tunayo fursa nzuri ya kurekebisha Katiba yetu. Hii ndio tumepewa fursa ya kurekebisha katiba, turekebisheni Katiba baadaye tukiambua kwamba zikusanywe huku zitakusanywa baada ya Katiba kurekebishwa.

Umeeleza pacenteji ya mfuko wa barabara ipandishwe ili iweze kufanya kazi vizuri zaidi. Sasa hivi kila lita moja ya mafuta tunatoza shilingi mia inakwenda katika mfuko wa barabara. Tukirekebisha maana yake tukiongeza kidogo kwa wakati huu maana yake unamwambia mwananchi ndio ailipie hiyo. Mimi nasema wazo sio baya Mhe. Mshimba kila inapotaka kujitegemea lazima wewe mwenyewe utafute kodi. Nasema tupe muda tutaliangalia kwa siku za usoni, ili hichi chombo kiwe kina mapato mazuri na kuweza kufanya kazi vizuri sana.

Umeizungumzia barabara yako ya Kinduni. Basi Kamanda Gavu yupo, Mhe. Rashid Seif yupo wamekusikia na watakwenda kuiangalia barabara yako ya Kinduni na kuangalia utararibu mpya.

Mheshimiwa umeniuliza kuhusu habari ya Hoteli ya Venta watu wanadai fedha zao. Pamoja na Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa kauliza swali hilo. Nataka niseme tu kwamba kulkuwa kuna Kamati iliundwa chini ya Mhe. Makamo wa Pili wa Rais na Afisi yake ilikuwa ina wajibu wa kutoa maelezo ya kina juu ya hatua tuliyofikia. Lakini kwa kifupi tu kwamba Mhe. Mwanasheria Mkuu ameifanyia kazi nzuri na ameshatoa mapendekezo nini kifanyike. Tumepata habari kwamba muwekezaji anakuja, basi atakapokuja ofisi zetu hizi tatu, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo ambayo ndiyo inayomlea ZIPA, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais na Afisi ya Mwanasheria Mkuu, tutakaa ili tuweze kuona nini tunafanya kulingana na mapendekezo ambayo yametolewa na Mhe. Mwanasheria Mkuu.

Lengo letu sisi kama Serikali hawa wananchi wanaodai walipwe. Katika eneo hili hakuna *compromise* walipwe na sisi tutalisimamia hilo ili kuweza kuona kwamba madai ya wananchi yanafanikiwa. Suala la muwekezaji amekubaliana na vijana kujenga uwanja wa mpira lakini muwekezaji anapiga chenga. Hapa tatizo moja tu vijana wetu hawa wamekubaliana na muwekezaji wa awali, sasa kuna muwekezaji mwengine, lakini ZIPA tumewapa kazi hiyo, wanalisimamia, wanaliratibu, likishakufikia pahala pazuri tutakupatia maelezo zaidi.

Suala jengine ambalo limeulizwa na Mhe. Mshimba na hili ametaka majibu ya kina si hivyo buti leo itafanya kazi. Wawekezaji kufutiwa ovyo ardhi. Hata na mimi hili silipendi lazima niseme ule ukweli. Na hili kuna *loophole* katika sheria yetu uya ZIPA hakuna *time limit* ambayo inamuambia muwekezaji kwamba ukipewa ardhi katika kipindi hiki uweke *investment* zako. Muwekezaji anakaa na ardhi ile na wengine sio wawekezaji wazuri ni speculaters anaanza kutafuta na yeye miaka 10, 20. Lakini hii haimfanyi Waziri asifate sheria, kuna sheria na taratibu zimewekwa zimepitishwa ndani ya Baraza hili za kufuta ardhi. Mimi nitazungumza sana na mawaziri wenye dhamana ya ardhi wakifuta wafate sheria.

Kwa hivyo Mhe. Mshimba kama hili wewe hulipendi na mimi silipendi, tufute ardhi kwa mujibu wa sheria. Sheria ya ZSSF iletwe kwenye marekebisho hii italetwa na hii ninaweza nikakuahidi kikao cha januari inakuja tutaifanyia marekebisho kwa sababu hii imeshawiva tayari.

Oktoba nimeshindwa kupata muda kwa sababu kuna sheria nyingi muhimu lakini hii itakuja kwenye kikao cha januari tukijaaliwa. Ulitaka vile vile nikueleze wale ambao wanochelewa kuwasilisha michango yao kama taasisi na kama michango yao kama taasisi na michango ya watumishi wao. Sheria ina-*provide penalty* nitamkumbusha mimi mkurugenzi mtendaji kwamba atoe adhabu kwa wanaochelewa. ZSSF watumie wataalam wa ujenzi kutoka serikalini kusaidia katika miradi yao ya ujenzi hili tayari ninalifanyia kazi lakini tumewataka walifanyie kazi *official*. Sio kumteua mtaalam pale wakafanya kazi nae tunataka wawaandikie Idara kama ni wasimamizi wawe wanasimamia.

Kuna suala jengine hili lilikuwa ni zito kidogo Mhe. Mshimba alitaka ajira PBZ zisitolewe kwa upendeleo, na mimi ninawaambia sitoi ajira kwa upendeleo. Ajira zinapotolewa zinatakiwa zitangazwe na kila mmoja anatakiwa aombe maombi yake na kama kuna usajili basi wafanyiwe usajili ili kila mmoja aonekane uwezo wake.

Kuna usajili wa aina mbili, usajili wa kuandika kuna masuala unaulizwa ya kujibu na usajili ya *verbal* unaulizana na yule anayekuuliza maswali moja kwa moja, anakuangalia jinsi unavyojibu maswali, anakuangalia jinsi unavyo-*master* lugha kama lugha ya Kiswahili, lugha ya kingereza, kichina inategemeana na jinsi ambavyo anataka kukuweka hiyo nafasi ya ajira. Kwa hivyo haya yote unapofanikiwa hakuna sababu kwa nini tena wasikupe ajira.

Kwa hivyo mimi nitazungumza nao zaidi na nitalisimamia zaidi na ninakushukuru umetoa ushauri PBZ watuandalie basi semina katika majibu yetu ili kuelimisha wananchi wetu juu ya uwezeshaji. Nimezungumza na PBZ wao wanasema ukeshakuwaandaa tu watu wako wewe waandae tu watatoa wataalam watakuja kufanya semina. Sasa hapo kama kuna vitafunio mwakilishi utaviweka hapo.

Mhe. Mahmoud kwanza amepongeza sana fedha kwa ajili ya meli na mimi nakushukuru sana tumpongeze sana Mhe. Rais kwa agizo lake. Lakini vile vile umetaka nikupatie ufafanuzi wa kila Wizara, nina ufafanuzi hapa, nikianza kuusoma Wizara moja moja nitachukua muda. Kuna wizara moja moja, taasisi zinazojitegemea moja moja, amount nitakazochukua lakini nataka nikwambie tu kwamba ili kuonesha mfano taasisi niliyotoa pesa kidogo nimetoa milioni mia moja na ishirini na sita ndio niliyotoa kidogo. Hii taasisi niliyotoa pesa kidogo sitaki niitaje kwa sababu mtaionea huruma.

Taasisi niliyotoa pesa nyingi ili kuonesha mfano nimetoa bilioni nne kutoka Wizara ya Fedha kuonesha mfano jambo letu la dharura limejitokeza lazima sote tushirikiane katika kulitekeleza yaani agizo la Rais, agizo la Rais hutakiwi tena kumwambia mzee hili haliwezekani, hii mzee hivi mzee hivi lazima utafute mbinu za kuweza kulitekeleza. Tutalitekeleza bwana wala usiwe na hofu, na wanaoendesha magari ya kubeba watalii wanatakiwa kukata vibali maalum, nimekusikia na nimekufaham, tutakaa pamoja na wenzetu wa utalii. Haya magari yana leseni sasa hivi vibali angalau wenzetu wa utalii watwambie kama viko ndani ya sheria tuliyoipitisha hapa basi tutaangalia utaratibu mwengine, hili tupe muda tufanye kazi kwa sababu hili ni la kufanyiwa kazi si la papo kwa papo tutazungumza na wenzetu wa Kamisheni ya Utalii.

Umetaka vile vile kupata maelezo juu ya hoteli ya Mpapindi na venta, venta nimeeleza. Mpapindi tatizo lao ni ardhi, wale walipopewa lile eneo kipindi hicho wale ni wastaafu wazungu nadhani wanatoka sijui Afrika Kusini au Europe wamejenga pale muda huo wote kulikuwa hakuna maelezo juu ya ile ardhi. Sasa imeibuka kwamba ile ardhi ni ya wananchi, tutalifanyia kazi tuweze kujua hasa chimbuko lake ni nini, ili haya matatizo yaondoke.

Mimi ninamshukuru sana Mhe. Makam wa Pili wa Rais, Mhe. Makamo wa Pili wa Rais sasa hivi amevamia matatizo haya ya ardhi. Hayo matatizo ya ardhi anataka yaishe. Lakini na Mhe. Rais kila anapokwenda kwenye ziara zake akikuta kuna tatizo la ardhi anaambiwa Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya mtalimaliza wenyewe hili. Sasa hapa kama hii ardhi imetolewa bila ya kujua kwamba hii ardhi ya watu basi tukishirikiana na Afisi ya Makamo wa Rais na Wizara ya Ardhi tupe muda kidogo tulifanyie kazi.

Sababu za msingi za kutokutumika soko la Dar es Salaam kwa magari yetu hili limepigiwa kelele sana Mhe. Hamza ni shahidi tulikuwa pamoja na wafanya biashara na nimelieleza kwamba tukimaliza bajeti hii inshaalla na Mhe. Mgimwa akesha kurudi kutoka Dodoma tarehe 16 wanafunga bajeti kule kwa sababu wanarudi Dar es Salaam basi baada ya sikukuu Dar es Salaam sio mbali. Mimi nitakwenda nitakaa na taasisi hizi tu-table matatizo yetu, tuonesha evidence juu ya matatizo haya. Sasa tukifika hapo wenzetu kama hawajatusikiliza sasa tunajua kwamba hakuna ile nia njema anayoizungumza brother wangu pale Ali Mzee lakini ule ukweli tutakuwa tumeshakaa na wenzetu tumeshalizungumza pamoja. Kwa hivyo ninakuomba Mheshimiwa tusatahmilie.

Mheshimiwa umetaka kujua *exemption* iliyotolewa ya mwaka 2011/2012 na faida iliyopatikana baada ya kutoa huo msamaha. Nimejibu katika suala langu moja nililijibu tarehe 9/7/2012 na leo ni tarehe 9/8/2012 na Mhe. Mwakilishi wa Chonga aliuliza swali la ziada nikamjibu kwa maandishi. Lakini kwa faida yako na faida ya wengine nasema hivi:

Mwaka 2011/2012 tulitoa misamaha 234 misamaha hiyo tuliitoa kwa wawekezaji, taasisi za serikali, kampuni ya watu binafsi, miradi ya washirika ya maendeleo mashirika ya umma na taasisi za kidini. Misamaha 234 misamaha

hiyo tuliyoitoa samani ya vitu vilivyoingia ndani ya uchumi wa vitu vya Zanzibar ilikuwa ni zaidi ya bilioni mia tatu na moja, na msamaha tulioutoa ulikuwa ni bilioni 22.01. Na katika msamaha huu tulioutoa asilimia 51 umekwenda kwa wawekezaji kwa maana wawekezaji walipata bilioni 11 nyengine milioni 11 zimekwenda kwa taasisi nyengine. Sasa ile bilioni 301 ndio iliyoingia katika uchumi wetu kwa kupitia vifaa mbali mbali. Kwa hivyo hiyo ndio ambayo faida tuliyoipata.

Umeeleza vile vile kupambana na magendo ya mafuta, magendo ya mafuta tumeiwekea mkakati maalum kwa kushirikiana na vikosi vyetu vya SMZ na vikosi vyetu vya muungano. Kwanza mkakati wetu mkubwa atakayetoa taarifa asilimia ishirini ya pesa zitakazopatikana baada ya magendo kukamatwa anapewa yeye. Na mkakati wetu wa pili ni kushirikiana hivi vikosi vyetu na ZRB inawasaidia inawewezesha ili waweze kufatilia kwa karibu zaidi. Kwa hivyo sisi tutapambana nayo mpaka magendo ya mafuta yaondoke, lakini kama unavyomuelewa mwanaadam, mwanaadam siku zote yeye samahani amekuwa kama guruguru ukizipa huku anazibua huku, lakini tutajitahidi kufanya hiyo kazi.

Mfuko wa barabara umeelezwa nishaujibu kwa nini mpaka leo hatujaweza kutoa risiti pale ZRB wameshaanza kutumia mfumo wa electronic mfumo wa risiti. Sasa kuna taasisi za kodi zinakutana Nairobi ili kulizungumzia suala hili la Afrika Mashariki. Matokeo ya Mkutano wao tutakuja kuona jinsi gani twende na sisi katika suala la utoaji wa risiti. Ni suala gumu sana kwa sababu kwanza ni yule anayenunua na yule anauza, mmoja lazima akerwe ndio risiti itoke. Mmoja akikerwa ndio risiti itatpla. Kama wote hawakerwi basi risiti haitoki. Tutajitahidi hata kutumia askari kanzu kuwaweka kwenye maduka na utaweza kumuona mtu yupo pale ukafikiri huyu mtu anataka kununua kumbe anaangalia risiti kama zinatoka atakamata hapo hapo nae, tunajitahidi kuweka mikakati kama hiy.

Ulitaka kujua kwa nini ATM mara nyingi hazifanyi kazi. ATM inaendeshwa na taasisi nyingi sana sio taasisi za kibenki tu, ile ni ATM ya benki lakini kuna watu maalum wanaoweka zile *switch*, switch ikiwa haifanyi kazi ATM nayo itakuwa haifanyi kazi. ATM mashine ikiwa haifanyi kazi ile ni *electronic* inawezekana ikawa haifanyi kazi na ile itakuwa haifanyi kazi. ATM yenyewe kama haina pesa itakuwa haifanyi kazi hivyo hivyo. La msingi ni kwamba tutawaomba wenzetu wa mabenki wenye ATM wawe wanazikagua mara kwa mara ATM zao hasa pale ambapo ulipoeleza *during the week end and during the* sikukuu pesa iwepo ya kutosha. Na kwenye ATM za PBZ sikukuu hii zitakuwa zipo pesa za kutosha tu wala usiwe na wasiwasi.

Lakini nataka niwashauri ndugu zangu ambao hawana ATM ya PBZ ni vyema ukawa na ATM ya PBZ kwa sababu PBZ wamejiunga katika Umoja, Umoja una mabenki 15. Kwa hivyo kama ya PBZ haifanyi kazi unakwenda katika benki nyengine unaweze ku-draw na ukaweza kupata pesa zako bila ya matatizo. Lakini vile vile tumewataka PBZ, waingie katika visa na katika *master card* ili iweze kusaidia kuchukua kwenye benki yoyote yenye visa na wametuahidi kwamba mwaka huu hiyo *process* itakuwa tayari.

Mhe. Mohammed Haji Khalid umeeleza kuhudu habari ZSSF nimeshalieleza, lakini vile vile umetaka kujua kwamba kwa nini hatuwapi pesa za wakati wanapokuwa hawana kibarua. Hapa nataka niseme kwa kifupi tu kwamba lengo la mswada ule kuanzisha ZSSF mfuko wa hifadhi ya jamii ni kumuwezesha mwananchi wa kawaida ili awe na matumizi wakati anastaafu. Tukisema leo ana miaka 30 kaajiriwa kiwana kime-*colapse* yeye hana kazi tumrejeshee pesa zake lile lengo litakuwa silo la ule mswada. Na lengo la serikali hatutaki tuje kuwa na wazee omba omba wazee ambao wamefanya kazi lakini baadae wanaomba. Ndio dwa maaba tukasema kwanba hizi pesa wacha tuziweke ili zije zimsaidie wakati akifika muda wa kustaafu.

Wenzetu Tanzania Bara kisa kilichopelekea Bunge kupiga kelele ni kwamba wanataka kifungu hicho kirejeshwe kwa maana kwamba hizi pesa zije ziwasaidie sasa hawa wazee. Sio mtu anadondoka kazini anakwenda kuzichukua. Lakini ninachokisema mimi ni kwamba sheria tumeipitisha ndani ya Baraza hili na mimi nitaileta tena sheria hii ya ZSSF kwa marekebisho kama Baraza wanataka lengo hili tuondokane nalo watatwambia. Lakini tukiondokana na lengo hili ule mtazamo mzima wa mfuko tumeshaupoteza. Kwa sababu mfuko huu sio SACCOS Kama unaweka unakwenda kuzichukua unapotaka huu si SACCOS. Huu una malengo maalum kwa hivyo tuutazameni bado tunao muda nitakapoileta ile sheria mtanambia mimi ni mtumishi wetu tu mtanambia hilo tuliondoshe tulirudishe. Lakini mimi nataka nitoe ule muono wangu na maoni yangu juu ya hili.

Uwanja wa watoto nimeshazungumzia pongezi kwa kupata meli sawa tunashukuru. Ameomba vile vile mishahara kwa wafanyakazi katika mwezi huu mtukufu wa ramadhan na sikukuu nimeombwa vile vile na dada yangu Mhe.

Asha Bakari nasema basi Waziri wa Utumishi yupo hapa, yeye atasema anataka vipi, mimi ninamsikiliza yeye, yeye ndie mtoaji mishahara.

Mhe. Hamza amesema kuhusu habari ya benki imekabiliwa na hujuma sasa. Nasema kama unavyoiona Mhe. Hamza na mimi ninaiona lakini nataka nikuhakikishie nitakuwa muangalifu sana kuiangalia Benki ya Watu wa Zanzibar ili isije ikaporomoka. Na ile kesi ambayo uliieleza kesi hiyo bado ipo na inaendelea haijafutwa, hatuwezi tukaiachie hii achievement iliyopatikana kwenye PBZ halafu ukaanza kuiona PBZ inayumba. Tusaidiane na mimi ni msimamizi wa ile Benki kama Wizara lakini wana *management* yao, wana bodi yao huwa siwaingilii. Wao walipoona kwamba kuna watumishi wamechota fedha zao, wamewaita watumishi hao wakaona walipe zile fedha halafu wawafukuze ni uamuzi wao si uamuzi wa wizara yangu. Na kwa sababu wana management yao na bodi yao, kama wanaona wawatimue halafu warudishe pesa yao sawa, lakini hatutakubali kuona benki hii inayumba tena. Sasa hivi benki hii iko katika top ten hatuwezi tukaiwachia ikayumba tena, lazima tuisaidie.

Magari yaliyozuiwa na TRA nimeeleza tayari kule Dar es Salaam, ZSSF nimeeleza vile vile kuchangia kurudisha. Mhe. Hamza vile vile umepongeza kuhusu habari ya meli, lakini ume-put more emphasis kwamba Shirika hili lifanyiwe ukarabati upya. Wakati Mhe. Omar anawasilisha ripoti yake kamati ya PAC tafuteni *Hansard* yangu muisome nilisema, mashirika haya ya serikali tuliyonayo manane tutayafanyia kazi ili tuone yepi yanaweza kujiendesha kibiashara yaliyokuwa hayawezi kwenda tuyafunge. Hili ni shirika moja linaweza kujiendesha kibiashara lakini mpaka tulifanyie kazi, tulitoe *engine* yote, tuikarabati upya halafu tuseme sasa hii tunakukabidhini meli na Mwenyezi Mungu ametupenda kutengeneza meli mpya. Maana yake meli tunayokuja nayo ni mpya tumetengenezesha kiwandani itachukua miezi kumi na mbili mpaka miezi 18 kipindi hiki tutalikarabati shirika la meli, ili meli inapokuja inakabidhiwa shirika jipya. Hatuwezi tukaja tukalikabidhi meli shirika hili hili liliopo sasa hivi hapana.

Umeeleza kuhusu habari ya kampuni ya savana nimelisikia tutalifanyia kazi muda mfupi tutalifanyia kazi kwa sababu wanaoendesha kiwanda hiki ninawafaham sana zile zote ulizozieleza taarifa na nimezipokea nimeziandika zote.

Mhe. Subeit masuala ya leseni kutolewa katika taasisi zaidi ya moja tutalifanyia kazi ili tuweze kuona jinsi gani tutakavyoweza ku- *synchronize* hizo leseni. Umeeleza vile vile kigezo gani kimetumika katika 4.5, tulipoanzia 4.5 ilikuwa ni kwa ajili ya BOT tu na wamekuja wenzetu hawa wa IMF Shirika la Fedha Duniani, wakaangalia ukubwa wa Zanzibar, wakaangalia idadi ya watu, wakaangalia umasikini, wakaangalia vigezo vingi. Wakasema jamani hebu tuanzieni na 4.5 kupata gawiyo lenu la BOT lakini hatma baadae muweze kwenda na ku-*review* baada ya kwisha kukamilisha hizo taratibu zenu.

Lakini sasa mimi ninafikiri wakati umefika kila pahala ambapo mahesabu yapo basi tuyaangalie mahesabu halafu tuwe na asilimia ambayo ni muafaka 4.5 imeshapitwa na wakati miaka mingi tena. Umeeleza kwamba kodi za magari zimepanda kuna mengine Mhe. Subeit lazima tustahmiliane. Maana na mimi nilikuwa najaribu kukata hicho hicho kitambaa nikashone koti, kwa hivyo nimekatakata humo humo kidogo nimepeleka kule lakini mambo yetu ni kweli lakini tustahmiliane kidogo tutaandaa utaratibu mzuri tu, tutazungumza na wenzetu wa ZRB kuona jinsi gani wataweza ku-fecilitate suala hili ili lisiwe mzigomkubwa sana kwa wananchi wetu.

Wafanyabiashara wa magari kutokuuza Dar es Salaam imezungumzwa kuhusu riba za benki, riba za benki hata mimi ninasema ni kubwa sana. Na ndio maana tunawashawishi wananchi wetu na mimi naendelea tena kuwashawishi wananchi tuanzisheni saccoss tuanzisheni *community bank*, tukisha kuanzisha sacoss kule kwenye sacoss yetu sisi wenyewe tutasema jamani hizi pesa zetu tunaweka kwa ushirikiano lakini tunakopeshana kwa asilimia tatu. Tukianzisha hilo haya matatizo yatakuwa yamepungua. Ninakuomba sana Mhe. Subeit tuanzishe SACCOS kule Micheweni.

Mhe. Ali Salum, pesa za wananchi zitumike kwa umakini kabisa mimi nakubaliana na wewe zitumike kwa umakini, mwakani umesema tutumie fedha zetu kwa kutafuta umeme wetu, tutajitahidi tuutafute umeme wetu, kama kwa pesa zetu ama kwa pesa za wafadhili kwa sababu tumeona umeme tunauhitajia.

Kufanya utafiti wa kutosha katika vyanzo vyetu vya mapato ili tuweze kujua hizo kodi tunazotoza zinalingana na vyanzo vyenyewe. Wahasibu kukaa muda mrefu umelizungumza wewe, limezungumzwa na Mhe. Mtando limezungumzwa na Mhe. Omar Ali Shehe, limezungumzwa na Mhe. Asha Bakari. Nimeshamwambia Mhasibu

Mkuu ukikaa sana pahala unazoea na kama kuna watu wananuka na wewe utanuka, hebu wahasibu wakuu wasikae zaidi ya miaka miwili. Kuna wahasibu wakuu wa Wizara tatu nimeshampa Mhasibu Mkuu nimeshamwambia hawa waondoshe wameshakaa sana. Narudia kuna wahasibu wakuu wa wizara tatu nimeshampa Mhasibu Mkuu nimemwambia wamekaa sana hawa wawaondoshe. Nina imani Mhasibu Mkuu somo yangu vile vile ni msikivu atawaondoa, atawapeleka wizara nyengine au taasisi nyengine waendelee na majukumu yao.

Alisema wakaguzi wa ndani wanafanya kazi kufuatana na matakwa ya mabosi wao. Mimi ninasema tu kwamba usifanye kazi kutokana na matakwa ya bosi, ufanye kazi kwa mujibu wa matakwa ya maadili ya kazi. Ukifanya kazi kwa ajili ya matakwa ya bosi hamtafanya kazi. Lakini mkifanya kazi kwa ajili ya maadili ya kazi yenyewe mtafanya kazi. Mkaguzi wa ndani anapaswa kukagua hesabu kumsaidia katibu mkuu huyu ni *first hand information* wa katibu mkuu juu ya hesabu zetu za ndani. Na kama hao wakaguzi wa ndani wanafanya kazi vizuri, mimi nasema yule mkaguzi wa nje angekuwa na kazi chache tu.

Na mimi naungana na pale Mhe. Jussa aliposema kwa nini hawa hawawi na mkuu wao, wacha tuliangalie hilo tutamshauri Makamo wa Pili wa Rais ili tumshauri vile vile Mhe. Rais na Makamo wa Kwanza tulione hili. Na kama hili tumeshalikubali tumekubaliana basi katika kipindi kifupi tunaweza kuanzisha hiyo taasisi kwa sababu nchi nyingi wameanzisha hiyo taasisi, hawa hawana pahala pa kuripoti. Mimi nimekutana nao wengine wanasema tunampelekea Katibu Mkuu taarifa hatupati feed back kwa sababu katibu mkuu na yeye ana mambo mengi. Mimi nasema hilo wazo si baya zuri tutaliangalia na tutalifanyia kazi.

Gari kutembea usiku wakati haina namba nasema hivi gari kutembea usiku, kutembea mchana, kutembea alfajiri madhali haina namba ni kosa. Sasa kama kuna yadi za magari wanatoa magari yao kutembea usiku bila ya namba nawaomba sana wasifanye, lakini nataka niwatahadharishe, Mhe. Mazrui yupo ukikamata gari inatembea bila ya namba na ukipata uthibitisho imetoka katika yadi fulani ifungie leseni tu. Hatuwezi tukaleyana hivi *simple* ifungie leseni tu. Kwa sababu huu si utaratibu mzuri namumba sana Mhe. Mazrui tushirikiane na Idara ya Leseni nayo tutashirikiana nayo ili kufanikisha suala hili.

Mhe. Ismail Jusa ulisema hili suala la meli lisiwe la dharura tu tuangalie hasa bajeti zetu kila mwaka kulingana na vifungu vyetu tunavyojipangia. Nimelipokea kwa mikono miwili na nitalifanyia kazi. Umeeleza tuangalie kununua meli mbili ndogo za kiasi badala ya kubwa moja lengo letu ni kuwa na meli mbili, lakini tumesema tuanzie na hii moja ni meli ya kisasa itakayopakia abiria 1000, itakayoweza kuchukua mzigo wa tani 100, ni meli ya kisasa ambayo itakuwa ina na sehemu ya kuwekea maiti, itakuwa ina chumba cha daktari, itakuwa ina *first class* na *VIP*, hukatazwi wewe ukitaka kuingia *VIP* utakata tiketi ya huko hukatazwi ni meli ya kisasa kabisa tunataka wananchi wetu wapate fursa za kutumia matunda ya Serikali yao ya Mapinduzi.

Bado mpaka sasa hivi hatujaamua tunaijenga wapi, tunajaribu kutazama mjenzi mzuri tukishakupata tu taarifa wananchi watapata, wataelezwa inajengwa wapi na kwa muda gani na hiyo meli inagharimu kiasi gani. Hivi sasa taarifa tulizonazo meli inaweza ikatugharimu kati ya US$ 12 mpaka 15 milioni, lakini bado mpaka tukishamaliza ule mchoro wa meli ndio tutaweza kujua.

Kuimarisha mfumo wa udhibiti wa ndani nimelieleza na umesema Sheria ya *Public Finance Act* tuifanyie marekebisho nayo vile vile tutaiangalia tumelipokea Mhe. Ismail Jussa. Pia Mhe. Jussa umesema kwamba kuna mambo mengi ndani ya sheria hiyo hayafai sasa hivi kuwepo, nakubaliana na wewe kwa sababu ni ya muda mrefu na lazima ifanyiwe marekebisho. Tutaifanyia marekebisho tukisaidiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu.

Ofisi ya Mkaguzi nimeeleza halafu vile vile umeuliza kuna watu wanaomchimba Meneja wa *PBZ*. Mimi nasema hawa watu wanaomchimba Meneja wa *PBZ* wasimchimbe, mwenye mamlaka ya mwisho ya meneja yule ni Rais, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ndio mwenye mamlaka ya mwisho ya uteuzi na Rais atakuja kuninong'oneza mimi kwenye sikio waziri mwenye dhamana ya ile benki, wasimchimbe kijana anafanya kazi vizuri na tunaiona benki tumsubiri astaafu kwa mujibu wa sheria au tuone utendaji wake umeaza kudhorota pale tutatoa mapendekezo ya kumuondoa, lakini kwa sasa hivi wasimchombe bure wamuache afanya kazi zake.

Mapato ya *ZRB* yanaongezeka mwaka hadi mwaka, nakubaliana na wewe Mhe. Jussa. Watendaji wanafuja fedha za umma kupitia manunuzi. Nataka niseme hapa pana kazi mbili kubwa, moja ni ile kuifanyia sheria ya manunuzi marekebisho.

Mhe. Spika: Wajumbe wanaotoka nje wakumbuke kurudi tena si muda mkubwa ujao ili tuje tumalize shughuli hii. Nawaomba sana Waheshimiwa Wajumbe Mheshimiwa endelea.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Moja ni kuifanyia marekebisho sheria ya manunuzi lakini moja ku *strengthen* ile *procurement management unit* ya kila wizara ziwe na nguvu kidogo, ziwe na utaalamu kidogo, ili huu ubadhirifu katika upande wa manunuzi basi usiwepo. Mhe. Jussa nimekufahamu vizuri sana na tutajitahidi sana.

Lakini vile vile umesisitiza kama sheria yetu inaruhusu twende katika ule utaratibu wa *bulk procurement*, umetumia neno kupitia *agent* lakini utaratibu ni kwamba ni *bulk procurement.* Kama serikali inataka kununua kompyuta 20 basi tuzinunue kwa pamoja halafu tuzigawe kwa wizara zetu na taasisi zetu badala ya kuwa huyu ananunua mbili, huyu moja, huyu tatu, huyu nne tutalitafakari hilo na tuone tunalifanyia kazi vipi. Na linawezekana kule Tanzania Bara wanalifanya na wamefanikiwa vizuri sana.

Idara ya Uratibu wa shughuli za SMZ haina haja ya kuwepo. Mimi nataka nimshauri tu ndugu yangu, rafiki yangu, swahibu wangu Mhe. Jussa hii idara muhimu sana. Siku moja nitakuomba twende Dar es Salaam mimi na wewe tuanze hapa kwanza uwasikilize ile *external finance*, halatu twende Dar es Salaam mimi na wewe uwasikilize na wale ina kazi nyingi sana. Kwa kweli wana kazi nyingi sana na mimi nakuomba tuwape nafasi hii ili watekeleze majukumu yao, lakini baadae Mhe. Jussa nitakuletea *silent report* ili uone majukumu wanayoyafanya *in detail*.

Hapa nimeeleza kwenye hotuba kwa kifupi kwa sababu ya wakati, lakini nitakuletea *in detail* hasa uone hii halafu nitakuwekea na *external finance* halafu utaona *contrast* na *similarities* itakusaidia. Mimi nakuomba sana hii idara acha iendelee bado na hasa ilivyokuwa inaongozwa na mwana mma shababi acha iendelee.

Pia umezungumza jambo zuri sana tuwatazame wazee katika pencheni zao, viwango vidogo. Hili Mhe. Rais ameshatoa agizo mwaka jana tumeongeza viwango vya pencheni kwa wazee hawa na ametupa maelekezo kila hali itakapoturuhusu hawa wazee nao tuwaangalie tupandishe viwango vyao vya pencheni. Tume ya pamoja ya fedha nimeshaisema.

Utumishi wa *BoT* hauna Mzanzibari kwa hivyo haina sura ya Muungano, kuna Mzanzibari mmoja tu, hizi ndio zile *listed* kero za Muungano. Mimi ninamfahamu sana swahibu yangu hapa Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora wanayazungumza haya utumishi katika taasisi za Muungano, *at least* kuwe kuna zile taasisi za Muungano basi ziwe zina sura ya Muungano. Hili ni kweli, na hilo ulilolisema ni sahihi kabisa waziri wamepewa *role* kubwa ya kuisimamia wizara. Ni kweli na umenisaidia kuwakumbusha mawaziri wenzangu kwamba *role* ya kuisimamia wizara wanayo kikatiba. Katibu Mkuu amewekewa utendaji wenye *role* ya kuisimamia unayo kikatiba usije ukafika pahala ukamkuta mfanyakazi pale hafagii ukachukua *role* ya kumfukuza kazi huna *role* hiyo, manaake tunajisahau na sisi mawaziri, huna *roll* hiyo ya kumfukuza mwite Katibu wako Mkuu umpe maelekezo. Kwa hivyo, hiyo *roll* ya kuisimamia wizara tunayo na kwa mujibu wa katiba. Kwa hivyo tuzisimamie wizara zetu ili faida iweze kupatikana.

Mhe. Abdalla Mohammed Ali alitaka kuelewa eneo la Bwawani, mwenyewe hayupo halafu akija anapiga buti, mimi buti Mhe. Spika, kwa maeneo ambayo nimeshajibu sitajibu tena. Eneo la Bwawani tayari kuna mambo mawili pale, kwanza kuna hoteli ile hoteli iko chini ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo. Kwa mujibu wa mgawano wa taasisi zetu ile hoteli imewekwa chini ya Wizara ya Habari, lakini serikali imepitisha maamuzi kwamba eneo zima pamoja na hoteli yake pafanyiwe *development* kubwa sana. Kwa hivyo, wametakiwa *ZIPA* wasimamie hiyo *development* na ndio maana ukaona na *ZIPA* wapo na hivi sasa wapo wawekezaji ambao wanakaribishwa kuleta mapendekezo yao juu ya watakavyoliendeleza lile eneo la Bwawani eneo zima sio hoteli tu, eneo zima mpaka kwenye Msikiti kule kote.

Kwa hivyo, tutakapofanikiwa kuwapata wawekezaji hawa tayari wapo wengine wameshajitokeza lakini tunaona bado kidogo tunataka tupate wengine zaidi ili tuweze kufanya *comparative analysis* nzuri zaidi, tukishakufanikiwa kuwapata hawa tutakuja tu kutoa taarifa hapa tumempata mwekezaji gani na ana-*develop* anafanya kitu gani. Lakini lengo letu ni kwamba pale pahala papendeze kidogo sio tujenge kijihoteli kimoja au nyumba moja tunataka papendeze kidogo ili hata jioni Waheshimiwa Wawakilishi mnapotaka kwenda kutembea badala ya kwenda Forodhani muwe mna eneo jengine la kwenda vile vile. Tunataka eneo hilo liwepo pale Bwawani kwa hivyo, Bwawani ni hivyo.

Vile vile aliuliza kuhusu habari ya msaada wa mchele, msaada wa mchele unaratibiwa na Wizara ya Kilimo. Wenzetu wa Japan wametupatia *metric tonnes* 1,200 za mchele na hizo zimeuzwa thamani ya shilinsi 832 milioni. Lakini wenzetu hawa wanazielekeza katiak *irrigation*, kwa hivyo kwanza watakapozipata zile pesa watazielekeza huko katika umwagiliaji ambao Mhe. Abdalla Mohamed alitaka kujua zinaelekezwa wapi.

Amesema pia *ZSSF* ifanyiwe marekebisho. Nakubaliana na wewe tutaifanyia marekebisho. Amesema kwamba wawekezaji tunachelewesha kuwapa misamaha yao ya kodi. Mimi nadhani na wawekezaji na wao wenyewe wanachelewa ku-*submit document* zao. Kwa sababu unaposafirisha mzigo wako mpaka mzigo unafika Zanzibar mwezi mzima Waziri wa Fedha utamkosa kukaa ofisi mwezi mzima?

Mhe. Spika: Samahani Mhe. Waziri, Waheshimiwa Wanadhim wa pande zote mbili nisaidieni kuwachunga Waheshimiwa Wajumbe warudi ndani. Nakushukuru.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Kwa hivyo mimi nasema kwamba walete *document* zao mapema zaidi ili tuweze kuwasaidia.

Mhe. Ali Mzee Ali nashukuru umezungumzia suala la nia njema na umewaomba Waheshimiwa Wawakilishi wanisaidie na mimi nashukuru sana nakuombeni mnisaidie ili yale matatizo ya Muungano basi yanayonihusu mimi tuweze kusaidiana kuweza kuyatatua na yale yanayowahusu wenzangu basi tusaidiane nao tuweze kuyatatua.

Mhe. Ali Mzee vile vile umesema *BoT* haina sura ya Muungano. Hili halipingiki kwa sababu linaonekana ndani ya macho yetu nakubaliana na wewe. Sasa tutajitahidi tuzungumze na wenzetu angalau sura ya kimuungano basi iwe na mwelekeo.

Suala la ununuzi wa meli nakushukuru umetoa histotia nzuri sana na mimi nimeipokea, na umetupongeza sana kwa hili hususan Mhe. Rais. *ZMA* umesema ina matatizo inafaa kurekebishwa na mimi nasema kila penye matatizo ni vyema pakarekebishwa. Kama tatizo ni mfumo au tatizo ni sheria basi ni vyema tukarekebisha.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa Mtandao umenionesha kianzio kizuri cha kodi, Mhe. Mtando wewe una buti nyingi unapaswa kunisikia. Umenionesha kianzio cha kodi nitakifanyia kazi ili kila mmoja anayevuna ndani ya nchi hii aweze kulipa kodi.

Pia umetaka kuelewa kuhusu habari ya mishahara ya Wahasibu, ile ilikuwa ni uamuzi wa serikali kutokana na unyeti wa maeneo wanayofanyia kazi. Tumekubaliana wao tuwape mshahara kulingana na maeneo yao wanayofanyia kazi, lakini yule anayepewa mshahara ni mhasibu *by qualification*, kama wapo wahasibu ambao wamepewa mishahara hiyo hawajafikia hizo *qualification* zinazohitajika za uhasibu mkuu nakuomba Mhe. Mtando tushirikiane na mimi nakuhakikishia tutalirekebisha. Si vibaya wahasibu kuwapa mshahara kidogo wasivutikevutike na mambo mengine, lakini wawe na zile sifa. Lakini pia huyu hata ukimuondoa ukimpeleka popote pale bado atabakia kuwa ni Mhasibu Mkuu lakini si Mhasibu Mkuu wa wizara na ndio maana tukasema kwamba tutengeneze utaratibu mzuri hawa wahasibu wetu angalau na wao wawe na mishahara ambayo inaridhisha. Wale walioko Pemba sio wahasibu wakuu wala si wasaidizi wa wahasibu wakuu wale, lakini vile vile tutaangalia.

Sasa hivi wenzetu wa utumishi hawa wanaangalia mtu miaka yake ambayo amefanya kazi na *qualification* zake ili kuweza kuona jinsi gani mtakavyoweza kupitana katika hiyo miaka ya kufanyia kazi. Lakini lile ulilolizungumza nakubaliana na wewe, haiwezekani leo mtu anarudi skuli leo halafu kesho unamzawadia Mhasibu Mkuu, hii bwana nitazungumza mimi na Mhasibu Mkuu wangu wa Serikali, uteuzi huu angalau basi apate uzoefu wa miaka mitatu, lakini leo Mhasibu Mkuu hii tutazungumza kwa sababu anakuwa haja-*gain experience*. Hili tutazungumza tuweze kulifanyia kazi kwa pamoja, lakini kama una majina ambayo unataka kunisaidia nakuomba sana nisaidie.

Ulizungumia pia sheria ya uhakikimali tuifanyie marekebisho, hili nimelikubali sasa hivi tunayo *consult* tunaifanyia kazi na ulisema kwamba uhakiki mali itenganishwe na eneo la mitaji ya umma. Ndani ya muundo wa ile idara kuna divisheni, hizi ni divisheni mbili tofauti, ndani ya muundo hizi ni divisheni mbili tofauti na zinafanya kazi tofauti. Sasa umenipa kazi moja ya kuzifuatilia kwa karibu ili niweze kuona kwamba wanafanya kazi inavyotakiwa na Mhe. Mtando au kwa mujibu wa sheria? Hiyo umenipa kazi na nitaifuatilia ili niweze kuona, lakini wana divisheni mbili tofauti. Kwa hivyo hawapaswi wao kulalamika lazima wafanye kazi kama ni divisheni mbili tofauti.

Vile vile ulitaka nikuelezee *performance report* imewasilishwa kwa Mdhibiti na Mkaguzi. Kwa kifupi mimi nimekaa miaka miwili, kwanza umesema mwenyewe kwamba ninatakiwa nikabidhiwe mimi waziri mimi sijakabidhiwa. Hii ni kwa sababu walikuwa wana watendaji wachache lakini sasa tumeshaiwezesha hii *department* kuwa na watendaji wa kutosha na nimeeleza katika ripoti yangu ya bajeti kwamba kuanzia mwaka huu watatoa hiyo ripoti sasa.

Mhe. Omar Ali Shehe somu yangu lini sheria ya *procurement* na ile ya fedha zitaletwa kwa marekebisho. Nadhani Mheshimiwa somu yangu nimekusaidia huna haja ya kupiga buti hapa.

Mashirika ya Umma hayafanyi hesabu. Kwanza hili ni kosa, kama shirika la umma halifungi hesabu ni kosa, lakini hapa tunatofautiana pahala pamoja tu, kuna baadhi ya Mashirika ya Umma mwaka wao ni kuanzia Januari mpaka Disemba hawaendi na huu utaratibu wa kiserikali kwamba kuanzia Julai mpaka Juni. Sasa tunapokwenda sisi tunakuta hesabu zao hazijafika kumbe ule muda wao au kalenda yao ya kufunga hesabu ni tofauti. Lakini umenisaidia nitayatafuta mashirika yangu yote niwaulize na kila mmoja aniletee hesabu zake pale kama kafunga au hakufunga nitaziona na kama hakufunga basi huyu kiongozi itabidi tuzungumze nae tuweze kufahamishana adhabu za kutokufunga hesabu za mashirika. Kwa hivyo, hilo tumelipokea Mheshimiwa.

Kuwahamisha wahasibu nimeshalisema hilo, *fixed asset register* nimelieleza Mheshimiwa na mimi nakubaliana na wewe ni muhimu sana kuwa nalo na hili kama nilivyosema *is a continues process* kila baada ya muda tutakuwa tunalirekebisha. Umezungumzia uuzaji wa mali chakavu nao vile vile una taratibu zake huuzi tu mali ya serikali kuna taratibu zake. Nitawasisitiza wenzangu Mhasibu Mkuu awe anazungumza na hawa watu wetu ili wafuate hizi taratibu za kuuza mali chakavu na kunakuwa na *register* yake vile vile ya mali chakavu ambazo umeziondoa.

Uimarishaji wa mfumo wa ulipaji kodi kulipia mahala pamoja na kupitia benki. Hili Mhe. Omar nataka niseme tu kwamba, kwa upande wetu hapa tunataka kodi zote za serikali zilipwe na zilipwe kwa ukamilifu na zilipwe kupitia benki. Lakini inaonekana Mhe. Omar una mawazo mazuri sana katika eneo hili, mimi nitakuomba sana pengine kabla hujenda zako Pemba kwenye jimbo ukawasalimie wapiga kura tupate japo robo saa mimi na wewe tuzungumze kuhusu hili ili nigeme mawazo yako, ili niweze kuyafanyia kazi najua baada ya sikukuu utakuja halafu tutakaa zaidi mimi na wewe ili uweze kutusaidia. Lazima tugeme mawazo ya kila mtu katika kutekeleza shughuli zetu.

Format ya kuandaa bajeti. Mimi nakubaliana na wewe kabisa na nililisema hili kwamba *format* yetu lazima iwe moja baina ya Pemba na Unguja haiwezekani hapa ikawa tuna *format* nyengine na Pemba nyengine, vifungu vinakuwa havina *consistence*, huwezi ukaviona huku utekelezaji wa vifungu hivi kwa Pemba vinafanya kazi gani, au idara hizi kwa Pemba zinafanya kazi gani na tayari nimeshamwambia Kamishna wangu wa Bajeti baada ya kikao hiki cha Baraza na sikukuu ataunda timu ya kupitia hili buku letu na kutoa mapendekezo. Kwa sababu ndani ya buku hili kuna vifungu vyengine sasa hivi hata yale majina hayafai tena, tuweke majina kwa mujibu wa hali halisi, tuweke vifungu kwa mujibu wa hali halisi, tayari nimeshampa hiyo kazi na ninaamini chini ya usimamizi wa Katibu Mkuu watafanya kazi na watalifanikisha *Inshaallah*.

Kamati ya *PAC* mapendekezo yake kutokufanyiwa kazi. Mimi nataka nikuhakikishie Mhe. Omar mapendekezo uliyoyatoa kwenye kamati yako mimi nimeyafanyia kazi na hatua yangu ya kwanza nilikutana na Wahasibu Wakuu wa serikali hii wote, nikakutana na *Internal Auditors* wote nikakaanao tukazungumzia na wale wasimamizi wa *procurement* tukaizungumzia ripoti yako na tumepeana mkakati. Ripoti hii atakayoiwasilisha Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora tutaiangalia kwa pamoja na kila wizara itaeleza kwa nini ule upotevu umetokea, ndio jukumu letu sasa. Nimenong'ona na Mhe. Waziri wa Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwamba kipindi hiki anaiwasilisha, anai-*table* ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi ili tuje tuifanyie kazi.

Mhe. Omar pia umeomba mishahara kwa ajili ya sikukuu. Mimi nadhani hata na mimi nautaka nikipata si vibaya.

Mhe. Asha Bakari Makame Idara ya Uhakiki Mali ni muhimu. Nakubaliana na wewe dada yangu hii idara ni muhimu sana na itabidi tuifanyie kazi ili iweze kutekeleza majukumu yake. Kuna watumishi ambao alikuahidi Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi bado hawajalipwa eria zao. Sasa nasema hivi, Mhe. Asha Bakari alilitupa suala kwangu na akasema kama sijampa majibu atapiga buti nzuri hapa leo. Mimi nataka nikuhakikishie Mhe. Waziri kwa kauli yake anasema washalipwa lakini na mimi nitathibitisha leo hii nitalifuatilia ili

niweze kupata uhakika kama washalipwa au bado, kama hawajalipwa basi tutalisimamia ili waweze kulipwa pesa zao.

Msamaha kuhusiana na mama wajawazito. Kama alivyoahidi Mhe. Rais tutahakikisha kwamba Wizara ya Afya inapata fedha mapema zaidi. Vile vile na wewe umetaka kuhusu habari ya mshahara kwa watumishi. Benki ya Kinamama iharakishwe, kuna kamati nadhani imeundwa inaliangalia hilo jinsi ya kuweza kuanzisha hiyo benki au kuanzisha *community benk* kwa ajili ya kinamama, tutalifanyia kazi na tuweze kutoa majibu kwa haraka zaidi.

Mhe. Hija Hassan Hija sheria ya *ZSSF* irekebishwe, ndugu yangu tutairekebisha kwa nguvu zetu zote. Umeshauri shilingi 150 milioni za JKU ziondoke zende kununuliwa meli. Mhe. Hija mkutano wetu wa mwanzo tulikubaliana tuunde kamati ndogo tukafanye kazi tuweze kujiridhisha. Kamati ile tumeshaiunda ina wajumbe kutoka Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, wajumbe kutoka Ofisi yangu na itakuwa na wajumbe kama hatujawateuwa kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu. Watafanya kazi tutajiridhisha tukishajiridhisha kwamba hizi pesa hazina kazi sasa tena mwanawazimu unampa rungu, tutaziondoa tu hatuna ujanja, tutaziondoa tutazipeleka kwengine kama sio kwenye meli basi tutapeleka kwengine lakini wewe poa tujiridhishe kwanza. Pengine zina kazi tutaziacha zifanye kazi wala usitaharuki.

Ubadhirifu wa fedha za umma ndani ya wizara. Hili tutalisimamia mawaziri wenzangu tupo kwa pamoja na Makatibu Wakuu tutalisimamia kwa pamoja ili huu ubadhirifu basi usiwepo.

Kuna wachache wanaotaka kuihujumu *PBZ* nimelieleza hili tutalisimamia ili benki yetu isiweze kuhujumiwa. Wafanyakazi wanne wameachishwa kazi PBZ kwa makosa gani? Hili umetaka mimi nikueleze na umenambia kwamba wizara imeeleza kwa sababu kuna upotevu pale wenyewe *management* na bodi imekaa imeona ni kuwaachisha lakini wakati huo huo imetaka walipe zile pesa. Kwa hivyo, hii wizara haitii mkono kule.

Pia umeipongeza sana Bima hasa kwa kutanua huduma zao Tanzania Bara na Zanzibar. Na mimi nimepokea pongezi zako na wewe mwenyewe ni shuhuda umeangalia na umeona katika Bima na mimi nawaombea dua sana Shirika la Bima wafanye kazi vizuri zaidi. Sasa hivi katika mashirika ambayo yana mwelekeo ni mawili, Bima a *PBZ*, lakini mashirika mengine mawili yanaweza yakafanya kazi vizuri vile vile, Shirika la Umeme na Shirika la Bandari na haya tutayafanyia kazi nayo yafanye kazi vizuri zaidi ili yasiwe yanachukua pesa kutoka serikalini au kupata misamaha ya kodi ili wao wawe wanalipa.

Mhe. Mohamedraza Mohammedali usimamizi wa ujenzi wa barabara mimi nakubaliana nae kabisa. Serikali inapojenga barabara wananchi wasivuruge hizi barabara, hii barabara ambayo tumeijenga hapa inayokwenda Mazizini na Fumba hapa Wizara ya Elimu tu sijui kuna chombo gani kile kimekwenda kishachimba ile barabara, mkitembea hapo Wizara ya Elimu mkikatisha tayari kuna chombo kimeingia yale meno yake kimeichimba ile barabara. Sasa wananchi nao waangalie, serikali inapojenga barabara tushirikiane kuzitunza hizi barabara vyenginevyo tutakuwa kila baada ya muda serikali inatafuta pesa kwa ajili ya ujenzi wa barabara.

Ameeleza mfano aliyouona gari imepakia ndondo na nondo zile zinaburutika zinakwaruza barabara, sasa huu si mfano mzuri hata kidogo. Mimi nawaomba sana wananchi na sisi wasimamizi wa wananchi tutakapoiona gari inafanya kama hivyo tuisimamishe tuwaambie huu si mfano mzuri pandisha nondo juu zivute zile nondo juu zisiwe zinaning'inia.

Pia amewaomba wafanyabiashara wasaidie serikali kwa kulipa kodi halali na mimi naomba vile vile, wafanyabiashara nawashukuru sana, nawapongeza sana tusaidiane katika kulipa kodi ili serikali yetu iweze kutekeleza majukumu yake.

Ametaka tunapotoa misamaha basi tuwaarifu wafanyabiashara wote ili na wao waweze kujiandaa badala ya kutoa barua tu. Sawa tumelipokea na tutaliangalia ugumu wake na wepesi wake. Amesema kwamba tunaweza kukusanya *Payee* kwa kiwango kikubwa zaidi basi tutaliangalia hili na tutalifanyia kazi ili tuweze kukusanya *Payee* kwa kiwango kikubwa zaidi. Lengo langu mimi ni kukusanya mapato kwa wingi zaidi, kama kuna Mwakilishi anaweza akanisaidia jinsi ya kuweza kukusanya mapato mengi zaidi mawazo yake nayakaribisha.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo na ufafanuzi huo nataka niseme tu kwamba nimejitahidi kujibu masuala karibu yote niliyoulizwa na Waheshimiwa Wawakilishi. Lakini kama kuna suala ambalo Mheshimiwa sijampatia jibu

namuomba radhi sana sio nia yangu ni kwa sababu ya muda. Hapa tulipo Mhe. Spika, ameshaniongeza dakika tano tayari.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe nichukue nafasi kwanza kumshukuru Mhe. Waziri aliniomba nimpe muda kama saa moja na nusu na kwa kweli ndio niliompa tena juu ya alama bila hata kuzidisha hata dakika moja. Nichukue nafasi hii kukushukuru sana na sasa basi Waheshimiwa Wajumbe niwahoji wale wanaokubaliana na Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara ya Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo wanyanyue mikono. Wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, kwa kuwa Baraza limejadili na kuikubali Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, sasa naomba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Matumizi ili kuvipitisha vifungu vya matumizi vya Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo.

KAMATI YA MATUMIZI

FUNGU 19 AFISI YA RAIS FEDHA, UCHUMI NA MIPANGO YA MAENDELEO

Kifungu 0202 Idara ya Kodi za Ndani	shs.39, 654,000,000/=
Kifungu 0203 Idara ya Forodha	shs.67, 077,000,000/=
Kifungu 0401	

Mhe. Ali Salum Haji: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, mimi nishukuru kwa dhati leo buti hakuna kali lakini kuna mambo ya faida ndogo ndogo tu naomba kwa Mhe. Waziri atusaidie.

Wakati nikichangia juu ya suala la Uwanja wa Watoto majibu ya Mhe. Waziri ameniambia kwamba tender za mwanzo zilikuwa zina matatizo. Baadae imebidi wamekaa waitishe tender upya. Mimi ninataka anisaidie tu kipindi cha kukabidhiwa na kuitisha tender ya mwanzo mpaka kuhisi kuna hayo matatizo madogo madogo kulikuwa kuna muda gani na hii hatua ya pili ni muda gani na anategemea lini hizo tender zitamaliza ili ule uwanja uweze kufanya kazi.

Mhe. Mwenyekiti, ninauliza hivi kwa sababu za msingi sana. Kama tutatembelea viwanja vyetu vya Mnazi Mmoja, tukiangalia kadhia au hatari za biashara za watu wanaokwenda pale jinsi ya hatua zinavyopikwa vyakula na hatua za watu wanavyotembea kwa kustarehe Mwenyezi Mungu atuepushe na majanga lakini otherwise tunaweza tukaja tukalia kilio chengine.

Mhe. Mwenyekiti, naomba ufafanuzi zaidi kidogo.

Mhe. Mwenyekiti: Hivi ni pahala pake kwenye mapato au kwenye uendeshaji. Mimi ninadhani ni kwenye uendeshaji huko.

Mhe. Ali Salum subiri kwenye uendeshaji.

Mhe. Ali Salum Haji: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa ninataka kujua kidogo kwenye fungu hili la 142219 mapato ya Uhamiaji, nilikuwa ninataka kujua ukaguzi wake huu unafanywa na nani juu ya kujiridhisha mapato hayo tunayokusanya.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, kwanza ninamshukuru sana Mhe. Mtando wakati anachangia hili suala hakulichangia.

Lakini kwa faida tu nitamsaidia. Sisi pale afisini tunavitengo ambavyo vinachunguza mapato ya uhamiaji na huwa vinafanya kazi hiyo kila kipindi ili kuweza kuona mapato yaliyokusanywa kupitia uhamiaji na PBZ walichokipokea na idadi ya wahamiaji ambao walioingia kwa mujibu wa visa zao. Kwa hivyo tunakuwa tunafanya na huwa tunachunguza lakini hivi sasa tumeona kwamba badala ya kuchunguza kwa kutumia macho na mikono tu, sasa tunataka kuweka njia ya electronics tuweze kujua mapato halisi yanayokusanywa pale ndio hayo yanayotolewa na watalii wenyewe.

Mhe. Mwenyekiti: Hivi kama Mjumbe hakuchangia sasa anahoja kweli ya kuuliza. Ninadhani itoshe hayo maelezo yaliyotolewa.

Kifungu 0401 Idara ya Mipango, Sera na Utafiti shs.3,518,000,000/=
Kifungu 0701 Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali shs.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, nilipochangia nilimuomba Mhe. Waziri kutusaidia kuhusu hili suala la 4.5 la mapato kuhusu misaada na kibajeti.

Lakini mheshimiwa ninamshukuru sana kawa muwazi kweli kweli na kanieleza vizuri na sote Baraza kila mmoja kafarijika, kapata yale maelezo ninamshukuru.

Lakini sasa mimi nimesimama kwa ajili ya kumwambia Mhe. Waziri kama tumeelewa kuwa makusudio ya hii 4.5 ilikuwa ni suala la gawio la Benki Kuu kama alivyotueleza yeye mwenyewe.

Lakini sasa wenzetu wameifanya katika mote kila sehemu ya mapato ya Zanzibar kutokana na muungano basi wanaifanya ni 4.5. Sasa ninamuomba Mhe. Waziri kama hili ndilo basi sasa yeye awe ni meneja mkuu wa kuongoza hii timu ya kudai mapato yetu kwa sababu tushadhulumika muda mkubwa, sasa aione kama Wazanzibari nao wanataka wapewe haki zao.

Kwa hivyo hili baada ya kulikuwa na kusudio maalum, humu mwengine tusikubali kwenda hivi kwa sababu ni maonevu. Kwa hivyo nimesimama kumwambia Mhe. Waziri ninamshukuru sana lakini aongoze sasa timu kutudaia haki zetu.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri kuna ombi hilo.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, kwa kazi aliyonipa Mhe. Subeit nimeikubali ya kuongoza na nitaiongoza vizuri sana.

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Mwenyekiti, katika kuchangia kwangu, maana yake ninatizama vifungu hapa nimeshababaika, lakini bora nizuie fungu hili.

Katika kuchangia kwangu nilisema kwamba kuna mafao ya Baraza la Miji: Mkoani, Chake-Chake na Wete hawajalipwa arrears zao na baadhi ya wafanyakazi.

Sasa nimepiga simu sasa hivi maana yake niliposema hivyo Mhe. Waziri Mwinyihaji kasema wameshalipwa. Nimetoka nje Mhe. Mwenyekiti, wewe shahidi hapa kwenda kupiga simu, maana mimi sisemi neno lililokuwa si la uhakika.

Wamesema kwamba wametiliwa pesa za matumizi ndio walizotiliwa, kama wamefanya hivyo watalipa arrears za pesa za matumizi walitiliwa Baraza la Mji. Kwa hivyo Mhe. Waziri ninataka unihakikishie Ramadhani hii jamani tusitese watu, wale watu wana familia hizi fedha zingewafaa zamani.

Halafu kuna wafanyakazi wa Wizara ya Kilimo Mhe. Waziri wamekuja hapa wameambiwa hayo mafaili yao hayaonekani hasa, maana bora nitumie fungu hili hili la Pemba. Wapo hapa mwezi mmoja na nusu yanatafutwa mafaili na mafaili hayajatimia Wizara ya Kilimo watu hawa hawapati kiinua mgongo chao.

Mhe. Waziri kwa ninavyokujua pamoja na watendaji wako tafadhali ninakuomba ninawaombea hawa wafanyakazi jamani walipwe viinua mgongo vyao na mafao pamoja na Vikosi vya SMZ walizokatiwa pesa zao.

Jamani tukisema maneno humu tunasema kwa uhakika, nimetoka hivi sasa ninasema tena kupiga simu Pemba. Ninakuomba sana Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, ninakushukuru sana na mimi kama alivyosema Mhe. Asha Bakari Makame kwamba yeye kapiga simu Pemba na mimi nimepiga simu vile vile.

Hakika Mhe. Mwenyekiti, wafanyakazi waliolipwa wamelipwa kuna baadhi tu hawakulipwa na nitazieleza sababu zenyewe, lakini ukweli wamelipwa. Kwa hivyo hatusemi uwongo tuaminiane Ramadhani hii, kama anavyosema tuaminiane na mimi ninasema tuaminiane.

Wamelipwa Mhe. Mwenyekiti, lakini tatizo lililotokezea zile pesa zilizopelekwa zimetiwa kwenye OC. Sasa wale kidogo kukawa na confusion; wao walifikiri labda zingekwenda separate. Kwa hivyo wale wa Halmashauri wamelipwa Mhe. Mwenyekiti, ni juzi tarehe 2 mwezi wa Agosti, mwaka huu shilingi milioni mbili, laki saba na arobaini na nane elfu mia mbili na arobaini na nane arrears zao makatibu.

Sasa kwa confusion hiyo wale wafanyakazi ambao ni wachache tu wa Mabaraza ya Miji, wao hawakulipwa kwa kweli. Sasa labda hao pengine ndio katika hao anaowasemea Mhe. Asha. Lakini kwamba hilo zoezi halikufanyika si kweli, wamelipwa kama nilivyotoa hizo takwimu na hilo tutalishughulikia kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha limalizike hakuna tatizo, sote tunawatakia mema wenzetu Mhe. Mwenyekiti. Ahsante.

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Mwenyekiti, kakiri mwenyewe waziri hapa kwamba Mabaraza ya Miji hawajalipwa na hawa ndio ninaowasemea. Hawa ndio niliosimama nikawasemea na pesa wametiliwa kwenye kama alivyosema mwenyewe kwenye hiyo OC sijui ndio nini, mimi si mhasibu wala sijui.

Ni kwamba waliolipwa si niliwatetea mimi, kuna baadhi ambao kama alivyosema mwenyewe wamelipwa lakini hawa sasa hivi Mhe. Mwenyekiti, mimi nimetoka kwanza, halafu akatoka na yeye.

Naomba sana. Mimi sitokuwa mbishi hapa ushanifahamu lakini ninaomba sana. Naomba pia mikato ya vikosi vyetu vya SMZ, nakuomba Mhe. Waziri hawa watu wanafanya kazi ngumu mno jamani. Katika vikosi ambavyo vinafanya kazi ni vikosi vyetu vya SMZ vinafanya kazi katika hali ngumu Mhe. Mwenyekiti.

Kwenye karafuu mbali, magendo wanauza roho zao hawa. Kwa hivyo ninakuomba sana Mhe. Waziri kwa sababu ni hapa hapa nipakamate na Wizara ya Kilimo kuna nini, hawa wafanyakazi wa Wizara ya Kilimo hata mafaili yao hayaonekani kuna nini.

Nakuomba Mhe. Waziri mimi sitozuia fungu, najua ninakuamini sana unaposema utatenda basi utatenda, lakini wajibu wangu ni lazima nitetee watu ambao wanatakiwa kupata haki zao.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, mimi naona Mhe. Dada yangu hapa Asha Bakari na Mhe. Mwinyihaji wanafika pahala wanakubaliana kwamba hao wenzetu wa Baraza la Miji Pemba hawajalipwa, hilo ndilo la msingi ambalo wanakubaliana.

Kwa maelezo ya Mhe. Waziri mwenyewe na maelezo ya Mhe. Asha wote wamekwenda nje wamepiga simu, lakini wamewapigia simu watu tofauti. Sasa kila mmoja amempigia simu alichokipokea alichokitumia lakini imeonekana kwamba hapa hapa kati kwenye Baraza la Miji wamekubaliana.

Sasa mimi ninataka niseme tu kwamba kwa sababu serikali inafanya kazi collective, serikali haifanyi kazi mmoja mmoja. Ninataka niseme tu kwamba Mhe. Asha Bakari ameona hili atuachie, mimi nitafanya jitihada zangu tutakaa na Mhe. Waziri mwenzangu tuone sasa tunasaidiaje hili kuliondoa, kwa sababu kama binadamu kama mfanyakazi anadai pesa yake si vizuri serikali ikawa inadaiwa pesa ndogo ndogo kama hizi shilingi laki moja au mbili haipendezi. Kwa kweli haipendezi.

Kwa hivyo mimi ninasema tu kwamba hili la wafanyakazi wa Miji tutakaa na Mhe. Waziri ikiwezekana hata leo tukimaliza kikao chetu inshaallah saa tisa, nitamuomba Mhe. Waziri tukae mimi na yeye, hatuna muda wa kulichelewesha.

Lakini na hili la vikosi ninadhani Mhe. Waziri wa Utumishi ameshalitolea maelekezo kwamba vikosi wale wasikatwe fedha zao, ameshalitolea maelekezo na ninadhani hivi sasa wacha tuli-monitor tuliangalie kama ule utekelezaji wa Mhe. Waziri wa Utumishi kwamba unafuatwa, kama haifuatwi basi tutasisitiza ufuatwe. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, naomba nilitie mkazo majibu ya Mhe. Waziri wa Nchi Fedha kuhusu suala la Mhe. Asha Bakari Makame juu ya mikato ya watumishi wa vikosi vya SMZ.

Baada ya kutoa kauli ile hapa ndani ya Baraza la Wawakilishi, chombo kinachohusika na masuala ya utumishi nacho ni Kamisheni ya Utumishi wa Umma. Kimekutana na Tume ya Utumishi Idara Maalum na kufanya mazungumzo juu ya kadhia hii, na wameshakubaliana kwamba suala hilo litapita mara moja.

Tume ya Utumishi ya Idara Maalum kwa mujibu wa sheria ndio yenye mamlaka ya kusimamia masuala haya ya watumishi wa Idara Maalum lakini chini ya usimamizi wa Kamisheni ya Utumishi wa Umma.

Kwa msingi huo Tume ya Idara ya Maalum imeshakaa na wakuu wa vikosi vyote na kuwaelezea taratibu za maslahi ya mtumishi kwamba hayaruhusiwi kukatwa kinyume na utaratibu wa ridhaa yake mwenyewe. Kwa hivyo suala hili ninafikiri serikali imelichukulia hatua na ninadhani Mhe. Asha aridhike na majibu tuliyompa kwa sababu sisi tukipokea ushauri hapa na maelekezo, basi kama serikali tunakwenda kufanyia kazi. Ahsante sana.

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Mwenyekiti, ninawaamini sana Mawaziri; ninamuamini sana Waziri wa Fedha kwa sababu ni mtu ambaye akisema kitu anakifuatilia na anakitekeleza na ni uungwana ulivyo. Hiyo ndio kupenda kazi yako. Kama mtu huipendi kazi yako basi maisha atafeli. Lakini kama unaipenda kazi yako hupati shida. Hilo moja.

Lakini la pili, ninamuheshimu sana Mhe. Haji Omar Kheir na yeye ni mmoja ambaye ukimpa masuala anayafuatilia lakini ninataka kusema hivi, wahakikishe ahadi hizi wanazozichukua hapa wanatupa feed back. Hilo moja.

La pili kwa utawala bora Mhe. Haji Omar Kheir atwambie yale makato yao, maana yake watu walikuwa hata mishahara yao hawaijui vikosi wanapokea tu. Hiyo ninakwambia uhakika hawajui. Kwa hivyo ninataka atwambie ilikuwaje kuwaje huko mbele ya safari. Hapa kwa sababu ninakuaminini Waheshimiwa Mawaziri tuendelee.

Mhe. Mwenyekiti: Tutaendelea baada ya taarifa hii.

Kwa sababu hili jambo limetokezea hapa Barazani, mimi nimepata barua kwamba zoezi hili la kukatwa limeshasitishwa rasmi. Sasa uhakika kama hiyo ni maandishi tu, utendaji haupo hilo ninawaachia Waheshimiwa Waziri kama alivyosema Mhe. Mjumbe.

Lakini mimi barua ninayo nimenakiliwa kuthibitishiwa kwamba amri au maelekezo yaliyotoka ndani ya Baraza hili yameshafanyiwa kazi na mikato hiyo kwa askari wetu imesitishwa rasmi.

Tuendelee.

Kifungu 0701 Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali shs.86, 803,000,000/=

Kifungu 1310

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, mimi kidogo nilikuwa ninataka ufafanuzi kutoka kwa Mhe. Waziri juu ya hii ukodishwaji wa mashamba wa mipira, malipo ya nyumba Africa House na malipo ya Depot, maana nikiangalia hapa katika makusanyo ya mwaka 2009/2010 kwenye mashamba ya mipira ilikuwa karibu milioni mia mbili na sita lakini makisio ambayo yapo hivi sasa ni milioni mia moja na arobaini.

Nikija kwenye malipo ya nyumba, kwenye mwaka 2009/2010 kuna milioni mia moja na thamanini na tatu lakini mwaka huu 2012/2013 ni milioni tisa sita lakini kwenye malipo ya depot mwaka 2009/2010 kulikuwa kuna milioni karibuni milioni mia mbili na sitini na saba lakini makisio ya mwaka huu yanaonekana ni milioni mia mbili kumi na nane.

Nilikuwa ninataka kujua kushuka kwa mapato haya kunatokana na nini.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, kidogo ninataka nimsaidie tu Mhe. Mtando. Haya mashamba ya mpira uzalishaji wake unaenda kama karafuu.

Kuna msimu una zao kubwa na wenyewe wanaelewa kwamba msimu huu mazao yatakuwa makubwa. Kwa hivyo tunaweza tukakodi kwa this amount. Msimu huu bei yake itakuwa hii tunaweza tukakodi kwa this amount.

Watu wanaangalia bei ya mpira nje, wanaangalia kiwango cha uzalishaji, halafu wanakuja wanasema msimu huu bei itakuwa hii nje, msimu huu production itakuwa hivi, kwa hivyo tutakodi kwa kiwango hiki.

Hivyo kutokana na hali hiyo ndio unakuta hizi bei zinatofautiana.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, ninasikitika sana Mhe. Waziri amenijibu moja tu hapa yapo matatu, baada ya mashamba ya mipira kulikuwa na malipo ya nyumba ya Africa House na depot nazo pia yanakodishwa kwa msimu sijui.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, malipo ya nyumba za Africa House, hapa sisi tunakodisha kwa dola na tunapokodisha kwa dola inategemeana na exchange rate wakati ule ambapo tunakuja kui-convert na kuweka hapa.

Utaona trend yake haipo sawa kwa sababu ile inflation ya dola na shilingi yetu. Kwa hivyo ndio hizo sababu za msingi tu hapo basi.

Mhe. Mwenyekiti: Na kwenye depot

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, na kwenye depot ni hali kama hiyo kwa sababu depot ya Unguja tunaikodisha kwa dola lakini depot ya Pemba tunaikodisha kwa shilingi. Kwa hivyo tunapovunja zile pesa vile vile inakuwa tofauti inaonekana.

Akifuatilia Mhe. Mtando ataweza kuona kwamba the average exchange rate ya mwaka jana na mwaka huu zipo tofauti, akichukua ile ya mwaka mzima halafu akaweza kuitafuta average yake ataona ipo tofauti.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Mwenyekiti, mimi ninapata shaka kidogo naona sijaridhika na majibu ya Mhe. Waziri katika hili, kwa sababu ukiangalia hii anayoizungumzia exchange rate kwa mwaka huu 2009/2010 kama imeweza kupatikana milioni mia moja na thamanini na tatu kwenye haya malipo ya nyumba ya Africa House.

Sasa mwaka huu bila shaka hata hiyo kodi itakuwa imepanda zaidi na dola zitakuwa nyingi zaidi, ninafikiri haikufika hata milioni mia ni milioni tisini na sita. Ndio ninataka kuona ule utofauti. Maana hii ni tofauti kubwa sana karibu ya milioni tisini kama utatizama kwa ghafla, basi exchange rate iende kwenye milioni tisini.

Hebu atusaidie kidogo hapo ufafanuzi zaidi.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mtando ninachotaka kumueleza hata akenda akitazama ile exchange rate, kuna wakati fulani exchange rate ilifika dola moja kwa shilingi elfu moja mia nane naa.

Na kuna wakati fulani exchange rate imeshuka mpaka imefika dola elfu moja na mia nne. Leo tunazungumzia exchange rate dola elfu moja mia tano na hamsini. Sasa ukizichukua dola laki moja ambayo unayokodisha, ukizi-plus na hiyo exchange rate iliyokuwepo hapo, utaona kwamba definitely kwa elfu moja na mia nane zitakuwa ni nyingi zaidi shilingi kuliko hii elfu moja na mia nne au elfu moja na mia tano.

Hiki ndicho ninachomwambia Mhe. Mtando, hakuna utata katika hili ni exchange rate tu.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri pamoja na maelezo yake hayo, mimi sijaridhika sana lakini ningemuomba labda nilifuatilie zaidi akanioneshe ule mfumo mzima ambao alioutumia zile rate zilivyo na bei ambayo wanakodishwa anapatia utaratibu huo, hakuna tatizo katika hili mimi ninaweza nikamruhusu Mhe. Mwenyekiti, tuendelee lakini akubaliane na hilo.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri anakuomba mushirikiane ili kufuatilia suala hilo.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, mimi ninamkaribisha sana leo jioni aje tufutari pamoja nitampa maelezo yote ili yawe ya moto moto sitaki nisubiri mpaka kesho, leo aje tutafutari nyumbani nitampa maelezo yote.

Kifungu 1301 Idara ya Uhakiki Mali na Mitaji ya Umma - shs.454, 400,000/=
Kifungu 1901 Bodi ya Mapato Tawi la Pemba shs.6, 982,272,000/=
Kifungu 2203 Bodi ya Mapato Afisi Kuu shs.138, 961,728,000/=
Jumla ya Fungu **shs.343,450,400.000/=**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote

Kifungu 0301 Afisi Kuu Pemba

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa ufafanuzi mbali mbali alioweza kuutoa hususan katika zile hoja ambazo nimezieleza na kwa kiasi fulani nimeridhika sana nazo, na ninamuamini sana juu namna anavyojibu masuala.

Isipokuwa kuna moja tu nililizungumza wakati nilipokuwa nikitoa mchango wangu pengine amesahau kunipa ufafanuzi. Nilizungumzia juu ya ujenzi wa Afisi Kuu ya Wizara ya Fedha Pemba ambayo kwa kweli nilisema kwamba ujenzi huu unahitajika, kwa sababu bado mahitaji ya afisi hii yanaonekana yapo kwa kule Pemba, na ukizingatia kwamba ule ujenzi wa mwanzo umeharibika.

Sasa sikuona humu kwenye maelezo juu ya namna ujenzi ule utakavyojengwa katika kipindi hiki. Sasa naomba unipatie ufafanuzi ili niweze kujua juu ya ujenzi wa Afisi ya Wizara ya Fedha Pemba.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, mimi ninawaamini Waheshimiwa Waheshimiwa Wawakilishi wote na hasa ninapokuwa na mwenyekiti wangu kama huyu Doctor Salmin ninamuamini sana.

Hili nililieleza Mhe. Mwenyekiti, lakini ninadhani inawezekana Mhe. Mwakilishi alikuwa ametoka kidogo au ninadhani anafanya consultation na Mhe. Panya, lakini nitamuongezea kidogo kwa faida yake.

Nimesema kwamba kwa upande wa Pemba tumepata kiwanja Gombani na kwa mujibu wa programu zetu mtaalamu elekezi tayari yupo kuangalia michoro ya aina gani na tutajenga jengo ambalo tutalitumia wizara tatu; afisi yangu, ajira na wanawake na watoto kulingana na ile idadi ya watumishi wetu tulionao, tumeona tutumie wizara tatu.

Nimeeleza vile vile kwamba pesa katika bajeti hii tunazo kwa ajili ya kuanzisha ujenzi wa jengo hilo. Nimeeleza Mhe. Salmini. Ahsante sana.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, ninadhani kipindi kile ulichonituma nikatafute wajumbe ndicho kilichokuwa nimejibiwa.

Lakini jengine Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli tunapata shida kweli katika chombo chetu hiki kuwasikia Waheshimiwa Mawaziri wanapotoa ufafanuzi juu ya mambo. Mhe. Waziri anaweza kutoa ufafanuzi lakini ukawa husikii na ndio maana unaona wakati mwengine Waheshimiwa Wajumbe wanalala hapa kusikiliza kwenye microphone kwa sababu tunakuwa hatusikii chochote mpaka unainama hivi, jambo ambalo halipendezi kwa Wajumbe wako kuonekana kwamba wanalala.

Sasa ningeomba sana Baraza lako tukufu lichukue hatua ili kuona kwamba jambo hili linapatia ufumbuzi ama kama alivyozungumza Mhe. Hamza tutafutiwe zile za kuwekea masikioni, badala ya Mjumbe kuinama atakuwa anasikia yeye mwenyewe moja kwa moja.

Kwa kweli tunapata shida. Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Mhe. Mwenyekiti: Ni kweli mheshimiwa nilimtuma na hiyo kazi mara tukimaliza shughuli hii watendaji wetu watafuatilia hili tatizo ambalo limo ndani ya ukumbi wetu.

Kifungu 0301 Afisi Kuu Pemba shs.962, 751,000/=
Kifungu 0401

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, ninakushukuru kunikubalia na mimi kwa niaba ya wananchi wetu kupata ufafanuzi zaidi ya Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri alipokuwa akitoa ufafanuzi wa michango yangu mingi nimeridhika sana. Hii hoja ambayo ninayoizungumza hivi sasa kuhusu wizi uliofanyika kwa mara nyengine tena Benki ya Watu wa Zanzibar.

Lakini nilisikitika sana Mhe. Waziri pale aliposema kwamba yeye linamkera na atasimamia, lakini bado kuna chombo ambacho kipo chini yake ambacho chenye maamuzi kuhusu wafanyakazi hawa.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, hapa Barazani haji mwenyekiti wa bodi wala wajumbe wa bodi, hapa yupo Mhe. Waziri. Tatizo jengine linalojitokeza kwamba hizi taasisi zinazojitegemea kwamba yale maamuzi yao, vile vyombo vinakuwa vina maamuzi ya moja kwa moja. Kwa hivyo wakati mwengine Waziri hata kama anataka kufanya maamuzi anakuwa anapata wakati mgumu.

Sasa mimi sijaridhika na hayo maamuzi yaliyotolewa na hicho chombo ambacho kipo chini yake, kwamba wafanyakazi hawa wameshathibitishwa kuwa kweli walichota hizi pesa. Lakini hivi sasa wanaambiwa waandike barua ili ya kuweza kuomba kuacha kazi.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, huu ndio utaratibu wa serikali kweli. Maana yake itakuwa mtu anaiba halafu atakuwa anaambiwa aandike barua. Mimi ninadhani kuna sheria nyingi ambazo za kuwaadhibu watu kama hawa. Lakini hata hiki chombo kinachosimamia ambacho Mhe. Waziri kipo chini yake kama wanafanya maamuzi ambayo yanakwenda kinyume cha sheria, mimi ninafikiri afanye maamuzi magumu.

Mhe. Mwenyekiti, umefika wakati hivi sasa lazima pesa ya umma kila ilipo ilindwe hata kama ipo chini ya mivuli mitatu tuilinde. Haiwezekani watu wameshatafuna pesa halafu unawaambie aandikeni barua ya kujiuzulu sio wajiozulu ati wanaambiwa waache kazi. Ina maana mtu ukimwambia aandike barua ya kuacha kazi *ofcourse* ina maana haki zake nyengine itabidi umlipe. Sasa mimi naomba maelezo ya ziada ili nipate kuachia hili fungu, ahsante.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, mimi nadhani Mhe. Hamza Hassan anataka kusikia jambo moja tu kwamba nifuatilie hii kesi kwa kina zaidi, niweze kuijua kwa kina zaidi, niweze kuyasoma maamuzi ya bodi na *management* dhidi ya watu hawa, halafu kama kuna kitu ambacho

hakiowani na upatikanaji wa fedha zilizopotea, basi hapo mimi nifanye *intervention* ili fedha zilizopotea nihakikishe kwamba zinarudishwa.

Kwa hivyo, mimi nataka nimuhakikishie tu Mhe. Hamza Hassan kwamba anipe muda huo na mimi niweze kulifanyia kazi kwa kina, niweze kuona hayo maamuzi yao yote, halafu kama ni waziri mwenye dhamana basi na mimi nitaangalia kwa mujibu wa sheria nini cha kufanya, lakini namuahidi Mhe. Hamza Hassan Juma kwamba nitakachokifanya mimi kwanza ni ku-*recover* ile fedha ambayo imepotea, ndio muhimu kwangu ku-*recover* ile fedha ambayo imepotea. Sio kutoa pesa nyengine za kuwapa wao kwa sababu tu anaacha kazi kwamba wanataka kustaafu, hilo halitoingia kwanza tutaangalia sheria na taratibu ili tuweze ku-*recover* hizo pesa. Lakini namuomba anipe muda ili niweze kulifanyia kazi.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, kama kuna chuo ambacho cha kuvunja hoja, basi nadhani Mhe. Waziri ana *PhD*. Kwa sababu anakuwa maridhia, lakini fungu liache lipite.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, mimi hoja yangu inakuja hapa kwamba chombo chetu hiki ni lazima kiwe kina-*consistence* katika maamuzi. Mhe. Mwenyekiti, tuna ushahidi kwamba kuna wafanyakazi wa Benki ya Watu wa Zanzibar wamefika mpaka kufungwa kwa ajili ya mambo ya udokozi na wengine Mhe. Mwenyekiti, wala yale makosa hawakuyatenda wao. Makosa yalifanywa na watendaji wengine, lakini kwa kuwa yule aliyekuwepo pale kuwa ndio *responsible* kwa siku ile, basi akachukuliwa hatua, mtu kafungwa na sasa hivi kaachishwa kazi.

Sasa ikiwa wengine wanachukuliwa hatua za kisheria baada ya kufanya ubadhirifu na wengine wanabembelezwa bembelezwa. Mimi nadhani Mhe. Mwenyekiti, tutakuwa hatuwatendei haki watu wetu na tutaendelea kuibiwa. Tutaendelea kuibiwa mpaka ifike pahala siku moja kuwe hakuna kitu benki ile itangaziwe kuwa imefilisika. Mhe. Mwenyekiti, leo wanaiba kidogo kidogo lakini kesho watakuja kuezua.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, hayo yalikuwa ni mawazo yangu ambapo siridhiki na matendo ambayo yanafanyika katika usimamizi wa Benki ya Watu wa Zanzibar. Lakini kwa kuwa Mhe. Waziri ameniambia nimpe muda, sawa nitampa muda na mimi kwa shingo upande fungu naliachia, lakini bado huko mbele nitakuja kuhitaji maelezo ya kina ni hatua gani ambazo alizozichukua. Mhe. Mwenyekiti nashukuru.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nilipokuwa nachangia hoja zangu zote Mhe. Waziri amekwishakutoa ufafanuzi namshukuru kwa hilo. Ametaka nimwachie muda ili aweze kuja kunijibu kwa ufasaha zaidi nakubali. Lakini kuna moja hili la hizi pesa bilioni 17. Tulikuwa tunaomba utupatie ufafanuzi kwa sababu sisi ndio wasimamizi, bila ya kuwa na maelekezo yake basi tutashindwa namna ya kuziendeleza huko mbele. Naomba maelekezo zaidi.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, huyu Mhe. Mahmoud ni Shemegi yangu halisi hasa, sio wa mchezo mchezo. Wakati nilipokuwa naeleza bilioni 17.166 kwa ajili ya meli, nilieleza nimezitoa katika taasisi za serikali katika bajeti ya mwaka huu wa 2012/13. Katika *circulation* yangu ya mwanzo nilitoa hii, ili waone wawakilishi mafungu mbali mbali niliyokata na *percentage* yake. Lakini aliniomba nitowe maelezo juu ya kila wizara. Wakati nafanya majumuisho nilisema kwamba nimetayarisha kila wizara na kila taasisi, lakini kwa sababu orodha ni ndefu, nikataja kwamba taasisi niliyoitaja pesa kidogo ilikuwa ni milioni 126. Lakini taasisi ambayo tumeikata pesa nyingi kuonesha mfano, ilikuwa ni wizara yangu mimi ninayoisimamia, nikasema nimetoa bilioni 4. Lakini nikasema nisipoteze muda kusoma moja baada ya moja, maana yake kiambatisho ni kikubwa sana. Sasa kama yeye anahitajia *copy*, nadhani baadae naweza nikaifanya hiyo kazi nikawapa *copy* au nitaileta Barazani na kuiwasilisha kwako ili uwagaiye kwa sababu sio siri katika hili, hizi ni pesa ambazo tunazikata tutaziwasilisha kwako ili uwagaiye Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nafikiri hoja yangu imejibika shida yetu tupate *copy,* ili tuweze kuweka kumbukumbu nzuri na ufuatiliaji mzuri katika utendaji wetu. Ahsante Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti. Mhe. Mwenyekiti, na mimi nitakuwa sitendi haki kama sikuungana na wenzangu wote kwa kumpongeza Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, kwa jinsi alivyokuwa makini, mahiri na alijikita katika hoja zilizoulizwa katika kutoa ufafanuzi wake. Nawaomba na Waheshimiwa Mawaziri wengine wote wafuate mfano wa Mhe. Waziri wa Nchi

Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, kwa sababu wakifanya hivyo, nafikiri hata zile buti zitapungua. Leo naona ajabu hapa kwamba wizara kama hii kubwa, lakini buti zenyewe za kiasi kiasi tu.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo, katika mchango wangu nataka nimuhakikishie Mhe. Omar Yussuf Mzee asishtuke sana leo nafikiri nitakuwa na buti mbili tu, baada ya hii na nyengine moja basi.

Mhe. Mwenyekiti, katika mchango wangu nilizungumzia suala la pencheni. Nashukuru katika majibu yake na wewe Mhe. Mwenyekiti, ni shahidi nilikuwa nikimsikiliza kwa kina wakati alipokuwa akijibu hoja zangu. Nashukuru kajibu kwa maana ya kama sera, kuwa Mhe. Rais kaagiza kwamba malipo haya ya pencheni yaangaliwe. Lakini kama atakumbuka katika mchango wangu ulijikita katika sehemu mbili. Mara nyngine huwa nasema haraka Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu ya ule muda huwa nataka niseme hoja zangu zote nilizokuwa nazo nizimalize. Kwa hivyo, labda ile moja ilimpita.

Mhe. Mwenyekiti, nilizungumzia pia suala la *calculation* za pencheni yenyewe, kabla ya yale mapitio na nikatoa mfano hasa wa mtu maarufu hapa Zanzibar, Maalim Abofu kwamba kuna mfano wa mtu. Labda hili nieleweke, naomba kidogo uniruhusu dakika mbili tu nilitolee mfano, kwamba kuna mtu ambaye mshahara wake aliomaliza nao ni tofauti na mwenzake ambaye viwango vyao wa kutumikia havikupishana sana, lakini ukija kutizama pencheni wanayolipwa haipishani sana na ili nieleweke Mhe. Mwenyekiti, natoa mfano wa huyu niliyemtaja Maalim Abofu. Mhe. Mwenyekiti, huyu kafanyakazi kwa miaka 31 katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, mshahara aliyomalizia, ameacha kazi mwaka 1985 kwa maana ya kustaafu, alikuwa anapata mshahara wa shilingi 4,600. Pensheni anayoipata hivi sasa kwa kufanyakazi miaka 32 akiwa ameacha mshahara wa shilingi 4,600, mshahara wake wa mwisho, anapata shilingi 41,730 kwa mwezi.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, kuna mwengine ambaye yeye naomba nimstiri jina lake, katowa ulinganisho tu, kwa sababu yeye itakuwa sio vizuri, huyu kwa sababu ni mwathirika ndio nikamtolea mfano. Huyu mwenzake yeye kastaafu mwaka 1988 baada ya kuitumikia nchi yetu kwa miaka 31 na alipoacha kazi mshahara wake wa mwisho ulikuwa anapata shilingi 800. Itazame shilingi 800 Mhe. Mwenyekiti, na kule shilingi 4,600. Huyu pensheni yake ni shilingi 41,700. Sasa huyu ambaye katumikia miaka 32 ambaye kawacha kazi mshahara wake wa mwisho ni shilingi 4,600, yeye anapokea shilingi 41,730. Huyu ambaye kawacha kazi akiwa anapata mshahara wa shilingi 800 kwa kufanyakazi miaka 31 anapata shilingi 41,700 tofauti ni shilingi 30 Mhe. Mwenyekiti.

Kwa hivyo, nasema tatizo liko sio tu katika kuliangalia kwa jumla kwa maana viwango viko kidogo, lakini hata ule utekelezaji wenyewe una matatizo makubwa. Mbali ya mambo mengine sitaki kupoteza muda wako, lakini ukitizama hata hii *breakdown* aliyokuwa kapewa Maalim Abofu, katiliwa mshahara humu kama ndio mshahara wake wa mwisho ambao sio mshahara aliokuwa akiupata. Kwa hivyo, hata hizi *calculation* zake zina matatizo. Kwa hivyo, nilikuwa naomba hili Mhe. Waziri alitazame kwa kina, awataze kuna upotevu mkubwa sana, kuna watu wanadhulumiwa sana katika sehemu hizi Mhe. Mwenyekiti, na kuna watu mimi naamini wananufaika na mipango hii ambayo inafanyika katika wizara yake.

Kwa hivyo, nilikuwa naomba suala hili Mhe. Mwenyekiti, walitazame kwa kina kabla hiyo *policy* ya Rais iliyotaka kwamba kuangaliwe viwango kwa jumla yake, hili hivi sasa wanaopata viwango hivi ili tupate kupata uwiano na kupatikane haki katika masuala haya. Nilikuwa naomba kauli ya waziri katika hili Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, mimi nimemfahamu sana Mhe. Ismail Jussal Ladhu. Lakini nataka niseme tu wakati unatayarisha kiinua mgongo cha mtumishi baada ya kustaafu, kuna *parameters* mbili ambazo ni muhimu sana. Moja ni mshahara wake wa mwisho, lakini la pili muda aliofanyakazi katika utumishi wa umma. Mshahara wake wa mwisho na muda aliofanyakazi. Sasa matarajio ni kwamba aliyefanyakazi miaka mingi na akawa anapata mshahara mkubwa, kiinua mgongo chake ni matarajio twabaan itakuwa kubwa. Lakini kama kuna tatizo hapo la ki-*formula*, mimi namuomba sana Mhe. Ismail Jussa basi nalo vile vile nitaliangalia kwa sababu amekuwa *very specific* amekuwa ya Maalim Abofu na ya mtu mwengine ambaye amekuhifadhi, basi nitamuomba sana basi baadae anipe hizo taarifa ili *very specific* tuweze kuziangalia. Pengine hao wawili ambao amewataja yeye, inawezekana pengine wapo wengi, lakini hawajijui, basi tuweze kurekebisha matatizo hayo kama yapo na kama yapo basi tuweze kuona ni jinsi gani tutakavyoweza kuchukua hatua haraka iwezekanavyo.

Namuomba tu Mhe. Jussa kwamba tutakapomaliza basi hizi taarifa anipatie ili tuanze kuzifanyia kazi, kwa sababu sasa hivi sitoweza kutoa jibu la haraka haraka, kwa sababu hiyo *formula* ambayo ameizungumza hapo sijaiona iliyotumika. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Mjumbe akishanipatia hizo taarifa tunaweza tukalifanyia kazi kwa ujumla.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru na nimeshaifikisha bahasha mbele hapo, apewe Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, ili alifuatilie baada ya kumaliza kazi hii hapa. Lakini kama alivyosema mwenyewe. Hii mimi nimetoa mfano, lakini naamini mambo kama haya yapo mengine Mhe. Mwenyekiti, na sisi kama chombo hatuji hapa kumtetea mtu mmoja mmoja, maana hatutowamaliza, hii nimetoa kama mfano tu kwa sababu huyu amekuja kwangu. Nilikuwa naomba kama chombo cha wananchi kwa ujumla wake, hii aichukulie kama ni *custody* moja, lakini baadae akae na idara yake inayohusika waliangalie kwa kina ili wazee wetu waliotumia umri wao mwingi kuitumikia nchi hii Mhe. Mwenyekiti.

Hata sisi leo tumo humu, mafanikio waliyoyapata ni kwa sababu kuna watu walifanyakazi ndio tukafika hapa. Kwa hivyo, nilikuwa naomba hawa wote kwa jumla niipongeze na serikali, aliyetuambia mapema kwamba kamshauri Mhe. Rais na Mhe. Rais katoa agizo kwamba waangalie viwango vya viinua mgongo. Nalipongeza sana, lakini na hili la hivi sasa pia katika masuala ya malipo walitizame kwa kina ili wazee wetu hawa wapate kuishi vizuri kama wanavyoishi watu wengine.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo nasema nashukuru tuendelee.

Kifungu 0401 Idara ya Mipango Sera na Utafiti Shs.404, 731,000

Kifungu 0701 Idara ya Muhasibu Mkuu wa Serikali Shs.2, 782,787,000

Kifungu 0801-Idara ya Uratibu wa Shughuli za SMZ Dar es Salaam-Shs. 258,275,000

Kifungu 0901 Idara ya Fedha za Nje Shs. 206,688,000

Kifungu 1001 Idara ya Mipango na Maendeleo ya Watendakazi Shs.188, 466,000

Kifungu 1101 Idara ya Mipango ya Kitaifa Maendeleo ya Sekta na Kupunguza Umaskini Shs. 397,354,000

Kifungu 1301

Mhe. Ali Salum Haji: Ahsante Mhe. Mwenyekiti. Mhe. Mwenyekiti, nishukuru kwa kupata fursa hii kwa mara nyengine baada ya kwenda mchomo kwa mara ya mwanzo. Mhe. Mwenyekiti, wakati nachangia mjadala huu nilizungumzia suala la mali yetu au mali ya wananchi wa Zanzibar kiwanja cha kufurahisha watoto na nikaeleza wasi wasi wangu kwamba taasisi ya ZSSF ina pewa nyingi, wamekabidhiwa muda mrefu lakini hatujui nini kinaendelea. Lakini nimshukuru Mhe. Waziri amejaribu kuelezea vizuri tu na alichokielezea yeye ni tatizo lililojitokeze kwenye masuala ya *tender* kwa nilivyomfahamu mimi, kwamba wameamua kuitisha tenda nyengine.

Mhe. Mwenyekiti, mimi hofu yangu ni muda mrefu sana na mara nyingi tunajaribu kutoa indhari kwa maslahi ya wananchi wa Zanzibar. Tulikuwa tunatoa indhari muda mrefu katika suala la meli mpaka janga likatokezea, na hapa hofu yetu ipo kwa wananchi wetu. Watoto wanapokwenda skukuuni Mnazi Mmoja Mhe. Mwenyekiti, mazingira yanatisha, na Mwenyezi Mungu apishilie mbali moto. Pale siku hizi watu wana mabiashara mengi ya chipsi, Mwenyezi usije ukazuka moto pale ni hatari sana.

Kwa hivyo, nataka Mhe. Waziri anisaidie maelezo, huu muda waliopewa mpaka kuitisha *tender* ulikuwa ni muda gani na huu muda ambao wameamua kutisha *tender* kwa mara ya pili tutegemee muda gani kwa hii tenda kumalizika na kiwanja kile kikaweza kujengwa. Mhe. Mwenyekiti, naomba kukaa.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, *concern* ya Mhe. Ali Salum Haji ninaiona hasa kwa upande wa utulivu wa watoto wetu kupata eneo la kuchezea. Nataka nimwambie tu kwamba kikawaida hasa unapoitisha *tender* mpaka ule utaratibu wote unapomalizika, kwa kawaida unatumia miezi

sita. Sisi tulipoitisha *tender* ile ya mwanzo hatukufika miezi sita baadae tukajakugundua kwamba ule mchakato kwa mujibu wa sheria ya *procurement* haukuwa sahihi na tungeweza kulazimisha kwamba yule aliyeshindwa apewe, basi wale wengine wangeweza kuishitaki serikali na kuipeleka mahakamani. Kwa sababu tulipoiona sheria ni kweli na hatukuona sisi watu wa ZSSF, tuliwaita wenzetu wataalamu kutoka kitengo cha uhakiki mali, kuja kuufuata ule mchakato mzima wa *tender*, wamegundua kwamba mchakato ulikosewa, kulikuwa kuna *elements* pale zimekiukwa. Kwa hivyo, wakaishauri serikali kwamba iitishe *tender* mpya. Sisi kama ni serikali tulipoiangalia ile sheria na ule mchakato, katibu mkuu wangu akaniandikia barua ya kuniambia kwamba tuna-*nullify tender* hii, kwa hivyo tunaomba tuitishe mchakato mpya. Sisi bila kupinga kwa sababu hatukutaka kuvunja ile sheria na wale hawakukosea kwa sababu kuwa walifanya makusudi ni kibinadamu. Tulivyoona hicho, tukasema sasa tuitishe *tender* mpya, tukaitisha *tender* mpya. Nadhani hatutofika miezi sita tutakuwa tumeshapata mkandarasi.

Mhe. Mwenyekiti, jana nimezungumza na Katibu Mkuu, nimezungumza na Mkurugenzi Mtendaji wa ZSSF tumekubaliana kwamba tui-*speed* ile *tender process* tusiwe tunapeana muda mrefu ili tuweze kupata mchakato. Nadhani katika kipindi cha miezi mitatu au minne tutakuwa tumeshapata mkandarasi. Sasa hivi tuko *very carefull* katika ile *process* nzima ili uanze kujengwa.

Mhe. Ali Salum Haji: Ahsante Mhe. Mwenyekiti. Mhe. Mwenyekiti, kama wanavyosema wenzangu waziri wetu mashaallahu Mwenyezi Mungu amzidishie Inshaallah. Nimeridhika tuendelee.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nimesimama katika *vote* hii ya Idara ya Uhakiki Mali na Mitaji ya Umma, kwa sababu nikisoma katika kitabu cha bajeti kimesema idara hii miongoni mwa jukumu lake ni kusimamia mali za serikali zikihusisha ununuzi, utunzwaji na uondoaji wake. Mali hizo ni pamoja na majengo, vifaa, mitambo, mashamba na zana mbali mbali na pia jukumu la kusimamia mitaji hii sera ya uwekezaji wa rasilimali katika mashirika na kampuni za umma na binafsi.

Mhe. Mwenyekiti, nimesimama hapa kwa sababu katika mchango wangu nilizungumzia suala la meli au ununuzi wa meli, nikatoa ushauri. Nashukuru Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, katika ufafanuzi wake kaupokea ushauri na ulikuwa ni ushauri kwamba ni haki yake. Nimesimama kwa sababu moja tu Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nasema tulizungumzia hapa juu ya suala zima la kwamba utaratibu wa ununuzi wa meli hii uonekana kwamba pia uko wazi. Mhe. Waziri pia katika majibu yake hilo kaligusia.

Kwa hivyo, nimesimama tu niseme sijui kama manunuzi ya meli hii kama yatasimamiwa na Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, kwa kupitia idara hii au mwengine yeyote, lakini kwa sababu hawa wenye dhamana kwa mujibu wa hotuba yake mwenyewe Mhe. Waziri basi tuhakikishiwe kwamba utaratibu wa *tender*, isiwe suala la mazingira namna meli hii inavyonunuliwa kama kumetokezea maafa, kwa hivyo kuna dharura watu wakatafuta ujanja hapa wa kutengeneza pesa binafsi mifukoni mwao.

Kwa hivyo, nilikuwa nataka utaratibu mzima wa *tender* katika suala zima la kuipata meli hii, uwekwe wazi Mhe. Mwenyekiti, ili wananchi na wajumbe wa Baraza la Wawakilishi waridhike. Fedha iliyotajwa takriban milioni 17 sio fedha kidogo Mhe. Mwenyekiti, ni fedha nyingi ambayo inakwenda pale ni fedha ya walipa kodi. Kwa hivyo, nilikuwa naomba utaratibu wake uwekwe wazi ili tujuwe kila mmoja aridhike. Nilikuwa naomba utaratibu wake uwekwe wazi ili tujuwe kila mmoja aridhike. Nilikuwa naomba kauli ya waziri katika hilo na baadae tuendelee Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, nataka nimuhakikishie tu Mhe. Ismail Jussa kwamba utaratibu wa sheria ya *procurement* utafuatwa na bila ya pingamizi, lakini katika ujenzi wa meli mpya utaratibu wake hautakuwa kama ile unakwenda kununua compyuta au unakwenda kununua pasi. Kwa sababu ukisema tu kwamba unataka kununua meli mpya, basi watakuja mpaka hawa *middleman*, kwamba mimi naweza kukuletea meli mpya, ukajikuta meli ambayo inakugharimu wewe dola milioni 12, *middleman* na yeye akatia zake dola milioni tatu, basi ikakugharimu dola milioni 15. Sisi tunataka kwenda kwenye *source*, tunataka kumtafuta kwanza mchoraji *naval architect* tumpate yule atakayechora meli tunayoitaka kwa matakwa yetu. Tukishakumpata *naval architect* akatuchorea, basi tutatafuta mjenzi *qualifier ship builders* wale wanaojenga ile meli.

Mhe. Mwenyekiti, sasa ukisema tutangaze kama hivi tunavyotangaza, basi anaweza akajitokeza mtu kama Omar Yussuf, akakuambia mimi nakuja naleta *tender* yangu na mimi naleta *order* hiyo, basi akawaletea meli mkaja mkawa mmeliwa. Sasa utaratibu wa sheria ya *procurement* tutaufuata, lakini tutaufuata kwa misingi kwamba tunataka tuone ile *volue for money* na tunataka kwenda kwenye *source*, hatutaki *middleman*. Sisi sasa hivi tuna utaalamu, Wazanzibari tumesoma, tunaelewa jinsi ya kwenda huko. Kwa hivyo, hii nilikuwa nataka ifahamike kwa tunavyokwenda.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru tena kwa majibu yake Mhe. Waziri fasaha, *straight the point* anayoitoa Mhe. Waziri. Kwa hivyo, nimuombe tu, kwa sababu katueleza na tumeelewa kitaalamu kwamba utaratibu wake huu hautakuwa rahisi kwenye kutangaza *tender* kama vinavyonunua vyombo vyengine. Lakini kasema vinakwenda mtengenezaji kwa maana ya *builder* basi niombe tu kwa sababu chombo hiki ndio chombo kinachosimamia serikali na ndicho chombo kinachosimamia fedha za walipa kodi, basi angalau labda mwakilishi mmoja kwa kupitia kamati ya *PAC* katika *process* hizi za kumpata na kufuatilia ujengaji na gharama zake, ashirikishwe ili turidhike na nadhani huyu akiridhika yeye kwa niaba yetu sisi, basi itakuwa katuletea taarifa tumeridhika hapa kwamba fedha hizi zinakwenda kutumika vizuri na zitafanyakazi ambayo imekusudiwa. Baada ya hayo Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru nasema tuendelee ahsante.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka niseme kwamba wazo la Mhe. Ismail Jussa sio baya, lakini nikishakumtia mwakilishi wa PAC kwenye kamati yangu ya kutafuta meli, likiharibika basi kamati nzima ile haina uwezo tena ya kusema kwamba ilikuwa nje. Mimi namuomba sana Mhe. Jussa aniwachie serikali nifanye kazi, kamati iwe ni *watchdog*. Tukija tukiharibikiwa kamati sasa inatukamata shuka, inasema sasa nyinyi mmefanya sivyo.

Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Jussa aturuhusu kamati ikae nje, kwa sababu ukiniambia nimchukuwe mwakilishi, nitamwambia somo yangu njoo. Ataingia mule ndani Mhe. Omar Ali Shehe mule ndani, na mimi nitamchukua Mwenyekiti, nimuingize ndani mule, ikiharibika basi Kamati ya PAC hamna tena maneno. Mhe. Jussa mimi nakuomba sana tuiwache kamati ya PAC iwe ni *watchdog*, serikali iendelee kuifanya hiyo kazi. Lakini nataka aniamini, mimi ninajitahidi sana kila *step* tunayokwenda najitahidi tusivunje sheria, nataka aniamini na aturuhusu tuendelee.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri anajua kama kuna watu ambao wanamuamini basi mmoja ni mimi, analijua hilo. Lakini hili nazungumza kwa sababu kutakuwa na watendaji ambao watakuwa wanasimamia, kwa sababu kaomba nimuachie na baadae kamati ije ifanye kazi yake iliopo ya kusimamia matumizi kwa maana ya *watchdog*, namkubalia na namuachia apumuwe. Ahsante sana

Kifungu 1301-Idara ya Uhakiki Mali na Mitaji ya Umma-Shs. 359,012,000

Kifungu 1901 Idara ya Uendeshaji

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, watani wangu wananiambia mbona wewe uko kimpya au kuna chochote. Nawaambia sina chochote, nilikuwa namuachia jamaa yangu apumuwe. Mhe. Mwenyekiti, nilivyochangia kwenye hotuba hii nilizungumzia PBZ kwa aina mbili ya mchango wangu. Moja ni ile ambayo Mhe. Hamza Hassan amezungumza, na sitaki nirejee tena kwa mujibu wa kanuni.

Lakini hoja yangu nyengine inasema kuwa kunataarifa kwamba kuna baadhi ya watendaji wanajaribu kuchezea mashine za ATM na hata huu uwizi ambao umefanyika ambao orodha ninao, sitaki nitaje majina, kwa sababu Mhe. Waziri majina anayajua mwenyewe. Wamefanikiwa kutoa fedha ndani ya benki kuna watu ambao wamejaribu kuchongesha kadi na sisi sote hapa kila mtu ana mia mbili, mia tatu, mia nne kwenye account yake na benki ni taasisi muhimu sana katika nchi, ukiigusa. Wachilia mbali mimi ninayeweka shilingi mia tano kwa mwaka, kuna watu wanaweka fedha nyingi kwa ajili ya biashara. Sasa Mhe. Waziri hebu aniambie kwenye idara hii ya utumishi, atafanye vipi ili kusafisha katika benki kwa watendaji ambao sio waaminifu ambao wanadiriki kuchonga hata ATM kadi na kuwapa watu wa nje kuweza kutoa fedha kwa ajili ya wizi, ili wawekezaji wetu na wananchi wetu ambao wanaweka fedha katika benki yetu basi wawe na imani kwamba benki yetu ni salama.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, nilimuona Mhe. Hija Hassan kanyamaza kimya, hata hiyo buti aliyopiga ilikuwa haina nguvu, haina afya. Kwa hivyo, nimefarajika sana kwamba amenielewe vizuri sana majumuisho niliyokuwa natoa leo.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, kwa hili anachonitaka Mhe. Hija Hassan nisimamie katika kuchekecha hawa watumishi tulionao, ili tuweze kuwachunguza wale ambao tunawaelewa kwamba hawa wana matatizo, basi tuweze kuepusha ili matatizo yale yasijekujitokeza katika fedha ambazo ni mali za watu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka nimuhakikishie kwamba hii hoja imekuwa nzito leo hapa, wiki ijayo tutakaa na uongozi pale ofisini Katibu Mkuu, Katibu Mtendaji wa Tume pamoja na uongozi wa PBZ, ili tuone tunafanya nini juu ya watumishi ambao wana mwenendo huo, ili tuweze kusafisha nyumba yetu mapema ndio lengo analolitaka

Kwa hivyo, kama tutagundua watumishi hawa wapo, basi badala ya kuwaweka katika maeneo ya fedha tutawaweka kwenye maeneo mengi kwa ajili ya kumaliza muda wao wa ajira. Mhe. Mwenyekiti, hili nimemfahamu Mhe. Mjumbe na tutalifanyiakazi. *(Makofi)*

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, tuendelee kwa sababu namuamini, lakini ukiangalia haya majina ya watu waliohusika, basi mwananchi wa kawaida anapata picha, kwamba hili jina la mtoto wa Hija ndio maana hata kesi haipo. Kwa hivyo, Mhe. Waziri sisi tunakuamini, lakini tunakuomba uendelee kuwatumikia wazanzibari kwa imani na kwamba benki ni mali ya watu wa Zanzibar. Mhe. Mwenyekiti, tuendelee. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri, mimi niliwaomba Waheshimiwa Wajumbe wasipige buti sana wakaniharibia mabao yangu haya. Kwa hiyo, wamepiga kwa mujibu wa maelekezo niliyotoa, lakini sio kwamba haikuwa na nguvu na wengine naomba wafanye hivyo wasiniharibie hizi meza zangu. Haya tunaendelea.

Kifungu 1901	–	Idara ya Uendeshaji na Utumishi	11,246,720,000/=
Kifungu 2101	–	Idara ya Ukuzaji Uchumi	335,578,000/=
Kifungu 2201	–	Idara ya Bajeti	5,553,838,000/=
Kifungu 2202	–	Chuo cha Uongozi wa Fedha	1,641,000,000/=
Kifungu 2203	–	Boti ya Mapato Afisi Kuu	7,297,000,000/=
Kifungu 2204	–	Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali Sh	1,330,000,000/=
Kifungu 2205	–	Mfuko wa Barabara	6,320,000,000/=
Kifungu 2206	–	Mamlaka ya Uwekezaji Vitega Uchumi Zanzibar Sh	300,000,000/=
		Jumla ya Fungu	**39,584,000,000/=**

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 19 – OFISI YA RAIS, FEDHA, UCHUMI NA MIPANGO YA MAENDELEO

Kifungu 0401	–	Idara ya Mipango, Sera na Utafiti	20,504,691,000/=
Kifungu 0701	–	Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali	2,527,308,000/=
Kifungu 0901	–	Idara ya Fedha za Nje	1,382,000,000/=
Kifungu 1001	–	Idara ya Mipango na Maendeleo ya Watendakazi	1,437,743,000/=
Kifungu 1101	–	Idara ya Mipango ya Kitaifa na Maendeleo ya Sekta na Kupunguza Umasikini	2,550,989,000/=
Kifungu 1301	–	Idara ya Uhakiki Mali na Mitaji ya Umma	6,000,000,000/=
Kifungu 2101	–	Idara ya Ukuzaji Uchumi	150,000,000/=
Kifungu 2201	–	Idara ya Bajeti	3,800,000,000/=
		Jumla ya Fungu	**38,350,761,000/=**

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 45 – MFUKO MKUU WA SERIKALI

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, tuweke nidhamu.

Kifungu 9101	–	Mfuko Mkuu wa Serikali	52,824,000,000/=
		Jumla ya Fungu	**52,824,000,000/=**

(Kijifungu kilichotajwa hapo juu kimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, ilivyokuwa Kamati ya Matumizi imejadili na kupitisha Makadirio ya Fedha ya (OR), Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo bila ya mabadiliko. Sasa naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako liyakubali makadirio hayo. Naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, niwahoji wale wanaokubali makadirio hayo wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika: Katibu tunaendelea.

Katibu: Mswada wa Sheria ya Kuidhinisha Makisio na Matumizi ya Serikali kusomwa kwa mara ya pili.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, kwa mara nyengine tena naomba nitimize wajibu wa Kikatiba chini ya kifungu Nam. 106, unaomtaka Waziri mwenye dhamana ya fedha kuwasilisha katika Baraza hili la Wawakilishi, Mswada kwa ajili ya kuidhinisha matumizi ya Serikali kila mwaka unapoanza.

Kwa heshima kubwa naomba sasa kwa ruhusa yako niwasilishe mapendekezo ya Mswada wa Sheria ya Kuidhinisha Makisio na Matumizi ya Shilingi 648,943,798/= kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali kwa mwaka wa fedha unaishia siku ya tarehe 30 Juni, 2013 na kuruhusu utoaji na uhaulishaji wa fedha hizo pamoja na mambo yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, napenda nianze kwa kukushukuru kwa dhati wewe binafsi na Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza lako Tukufu kwa mashirikiano makubwa, ambayo kwanza yalituwezesha sisi Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kuandaa na kuiwasilisha Bajeti ya Serikali, ambayo ilipitishwa awali na Baraza lako Tukufu.

Pili katika kuchangia bajeti za wizara zote za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na hatimaye kumalizia na Bajeti ya Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo.

Mhe. Spika, kuidhinishwa kwa bajeti za Wizara zote hizo, kunapelekea mswada huu mfupi wa Makisio na Matumizi, ambao unadhamiria kutoa uwezo kwa Serikali kutumia kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina jumla ya shilingi bilioni 648,943,798,000/=. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 307,797,136,000/= kwa ajili ya kazi za kawaida na shilingi bilioni 341,146,612,000/= kwa ajili ya kazi za maendeleo.

Mhe. Spika, kupitishwa kwa mswada huu kutaiwezesha pia serikali kukopa ndani na nje fedha kwa ajili ya matumizi ndani ya mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2013. Kiasi cha fedha kilichoainishwa kwa ajili hiyo ni kama kinavyoongozwa na masharti ya kifungu cha 4.1 cha mswada huu.

Mhe. Spika, mswada huu una vifungu vinane. Kifungu cha kwanza kinazungumzia jina fupi, kifungu cha pili kinazungumzia utoaji wa shilingi bilioni 648,943,798,000/= kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali.

Mhe. Spika, kifungu cha tatu kinazungumzia makisio ya fedha zilizokubalika, kifungu cha nne chenye vifungu vidogo vinne kinazungumzia uwezo wa kukopa wa Waziri mwenye dhamana ya fedha. Kifungu cha tano chenye vifungu vidogo vitatu kinazungumzia uwezo wa Waziri katika maombi ya ziada, kwa lengo la kukabili matumizi mengine ya dharura itakapotokea mahitaji.

Kifungu cha sita kinazungumzia marejesho ya mkopo na riba, kifungu cha saba kinazungumzia kukubaliwa kwa mpango wa maendeleo na kifungu cha mwisho cha nane kinazungumzia kukubaliwa kwa fedha zilizopitishwa kwa matumizi ya maendeleo.

Mhe. Spika, mswada huu ni mfupi kama nilivyosema hapo awali. Kwa hivyo, naomba kwa idhini yako na Waheshimiwa Wajumbe kuweza kuujadili na hatimaye kuupitisha, ili iwe Sheria ya Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2012/2013. Mhe. Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, hoja imeungwa mkono, ikimaanisha sasa tuijadili. Ninao wachangiaji watatu, nashukuru nadhani wanatosha sana na Mhe. Hija Hassan Hija wa nne. Kwa hiyo, nitangulie kumuomba Mhe. Ismail Jussa Ladhu na baadaye Mhe. Abdalla Juma Abdalla kuchangia.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii kuwa mchangiaji wa mwanzo katika mjadala wa Mswada huu wa Sheria ya Kuidhinisha Makisio na Matumizi ya Serikali kwa maana ya *Appropriation Bill*.

Nimpongeze tena Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwa hatua yake ya kuwasilisha mswada huu ambao Mhe. Spika hiyo maana yake ni kwamba tayari tumefanya kazi kubwa ya kupitisha mafungu ya wizara mbali mbali.

Mhe. Spika, mimi naomba bila ya kupoteza wakati nizungumzie maeneo machache kuhusiana na mswada huu kwa maana ya maudhui na pengine kidogo katika vifungu kimoja au viwili.

Mhe. Spika, katika maudhui nilikuwa nasema fedha hizi bila ya shaka zimeidhinishwa na Wajumbe wa Baraza hili na tayari mafungu ya wizara mbali mbali hivi sasa tunakamilisha utaratibu wa kisheria tu, kwa mujibu wa matakwa ya Katiba yetu ya Zanzibar kifungu cha 106.

Lakini Mhe. Spika, kulikuwa na maeneo ambayo mimi naomba kidogo niyachangie. Moja Mhe. Spika, mswada huu katika kifungu cha tano kama ilivyo kawaida miswada hii inampa idhini Mhe. Waziri anayehusika na masuala ya fedha kuhaulisha vifungu na pale ambapo uhaulishaji huo utajumuisha ongezeko la bajeti kwa bajeti ya ziada, basi kuja kupata idhini ya Baraza ikibidi hata baada ya kuchukua hatua ikiwa hatua zenyewe ni za dharura.

Mhe. Spika, mchango wangu nataka kumuomba Mhe. Waziri, kwamba alitazame sana suala hili si kwa maana ya yeye kutekeleza madaraka haya na kwa wale watakaokuwa wamekasimu madaraka yake. Lakini juu ya kufuatwa taratibu za fedha katika uhaulishaji wa vifungu katika wizara mbali mbali na taasisi nyengine ambazo yeye anazisimamia kama Waziri mwenye dhamana ya fedha.

Mhe. Spika, nalisema hili kwa sababu tunao ushahidi na hapa si mahala pake kwa hivi sasa na wala sitaki kurefusha mjadala huu, lakini tunao ushahidi kwamba katika wizara mbali mbali Makatibu Wakuu wakeshaidhinishiwa fedha

hudhani zile ni miliki yao na wanaweza kufanya wanavyotaka. Taratibu za uhaulishaji wa vifungu kwa mujibu wa Sheria zetu za Fedha hazifuatwi katika wizara na taasisi nyingi Mhe. Spika. *(Makofi)*

Kwa kweli si hilo tu Mhe. Spika, kuna mifano ya wizara na taasisi ambazo kwa kuendekeza mno safari na hili tumelisema sana Mhe. Spika, kwamba safari imekuwa ndio *priority* ya watendaji wetu pamoja na wakubwa wetu wa Serikali, kinachokimbiliwa nini ni posho ya safari Mhe. Spika.

Sasa mara nyengine inapokuwa *priority* safari watendaji wanaingia kuhaulisha hata vifungu vya *Capital Expenditure* katika kugharamia safari, ambao si utaratibu kabisa Mhe. Spika, lakini watendaji wetu na wala sitaki kutaja mifano hivi sasa, lakini iko mingi tena naamini hata Mhe. Waziri anaifahamu.

Kwa hiyo, nilikuwa naomba asimamie sana suala la sheria hizi katika kusimamia uhaulishaji wa fedha, ambapo madaraka amepewa yeye kwa jumla katika kifungu cha tano cha mswada huu.

Vile vile katika kutokupoteza muda kuna baadhi ya mambo nilikuwa nimeshayasema na ninashukuru ameyakubali katika suala la kuanzishwa *Office of Internal Auditor General* kwa Zanzibar, ili kudhibiti matumizi ya fedha zetu, badala ya kuwa Mhasibu Mkuu akawa yeye ndiye mtumiaji na halafu huyo akang'ang'ania kila pendekezo likipelekwa kazi yake kulitia chini ya meza, kwa sababu anajua litamuathiri yeye. Mhe. Spika, namshukuru Mhe. Waziri wakati wa kujibu hoja zetu alilikubali na kusema kwamba atalifanyiakazi na baadaye kurudi kwetu.

Mhe. Spika, kwa haraka haraka la jumla katika maudhui nimuombe Mhe. Waziri wakati wa asubuhi nilipokuwa nikichangia bajeti ya wizara yake, nilizungumzia Mhe. Spika Sheria yetu hii ya *Public Finance Act* na nilimuomba ayatizame tena, kwa sababu huko ambako tulinakili sana wao wenyewe wanaifanyia mapitio.

Lakini wakati bado haijafanyiwa mapitio basi sheria hii ni valid inatumika na sheria hii imempa dhamana kubwa sana Waziri wa Fedha au Waziri mwenye kushughulikia masuala ya fedha katika kusimamia *Public Finance*. Mhe. Spika, tukiangalia katika kifungu cha 9 cha *Public Finance Act* kimempa Waziri madaraka ya kuweka adhabu kwa watu ambao watakuwa wanakiuka sheria hii.

Vile vile kifungu cha 9(3) Mhe. Spika kuna hoja ilitolewa hapa wakati tulipokuwa tukipitisha vifungu juu ya suala la wale watu nafikiri aliitoa Mhe. Ali Salum Haji, watu ambao wanaotumia fedha, Mhe. Spika samahani nadhani alitoa Mhe. Hamza Hassan Juma alizungumza hoja ya watu wanaotumia fedha isivyo halali na halafu baadaye wanaambiwa waandike barua za kuwajibika. *(Makofi)*

Lakini Sheria ya *Public Finance* Mhe. Spika kifungu cha 9(3) kimempa madaraka Waziri wa Fedha kuagiza kwamba panapotokea upotevu wa fedha au matumizi mabaya, basi kumtaka aliyehusika kulipa fedha ile kabla hatua nyengine za kisheria. Sasa nadhani vifungu hivi vimempa madaraka mazuri tu Mhe. Waziri katika kusimamia *Public Finance* na avitumie. *(Makofi)*

Mhe. Spika, la mwisho katika sheria kifungu cha 11 cha *Public Finance Act*. Kifungu hichi kimetoa nafasi kwa waziri kuanzisha *Special Funds*, sasa sijui hii *Special Funds* ni pamoja na hili Mhe. Waziri atakapokuja atanisaidia, ni pamoja na yale mashirika au taasisi ambazo tunazipa ruzuku, kwa sababu zile moja kwa moja huwa haziwajibiki hapa.

Sasa ukitizama kifungu cha 11 kimetaka *Special Funds* zitakazoanzishwa, bado mahesabu yake na hata idhini ya matumizi yake yaje yaombwe katika Baraza la Wawakilishi kwa taarifa rasmi kabisa.

Mhe. Spika, asubuhi nilichangia na wala sina haja ya kupoteza muda kifungu cha 23 kinazungumzia pia, kwamba fedha za maendeleo zinapokuwa hazikutumika, basi katika mwaka unaofuata wa fedha inabidi zije ziripotiwe katika Baraza la Wawakilishi.

Sasa naomba Mhe. Spika, wakati tunapitisha Mswada huu wa *Appropriation Bill* ambao sina wasi wasi kwamba utapita, basi Mhe. Waziri aangalie kwa kina maeneo hayo, ili pale inapobidi aitumie vizuri *Public Finance Act* wakati tunasubiri kui-*review*, tuhakikishe kwamba tunadhibiti vizuri fedha za wananchi wetu.

Mhe. Spika, jengine ambalo naomba tena walichangia watu wengine hapa, kwamba katika matumizi au kupanga bajeti tumekuwa hatuzingatii sana hii *MTF* wala *Strategic Plan* za Wizara. Mhe. Waziri ametuambiwa wanayo na kuanzia mwakani atahakikisha kwamba kila kamati inapatiwa.

Mhe. Spika, mimi nasema kwa mwaka huu wa fedha wakati tunapitisha Sheria hii ya *Appropriation*, basi Idara yake ya Bajeti ipewe uwezo pamoja na meno ya kusimamia, kwamba haya matumizi tunayoidhinisha hapa yende kwa mujibu wa vifungu tulivyoviidhinisha Mhe. Spika na yazingatie hiyo *Medium Term Expenditure Framework (MTEF)*, lakini pia vizingatie *Strategic Plan*, yaani Mipango Mikakati ya Wizara na isiwe kila mtu anatumia anavyotaka yeye.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo na nimesisitiza suala la kuwaimarisha Wakaguzi wa Ndani nadhani hilo amelizungumza vizuri Mhe. Waziri. Kwa hivyo, sasa naomba nigusie moja tu, ili akija Mhe. Waziri naomba anisaidie katika mswada wenyewe. Mhe. Spika, kifungu cha 5(3) anaomba kunukuu kidogo.

Kifungu cha 5(3) cha Mswada kinaeleza hivi:-

> "Waziri mwenye dhamana na mambo ya fedha anaweza kukasimu uwezo wake alionao chini ya kifungu hichi kwa afisa yeyote kwa mujibu wa masharti atakayoona yanafaa".

Mhe. Spika, ukitizama Katiba imemtaja Waziri, lakini sheria tukipitisha huwa zinampa madaraka waziri kukasimu madaraka yake haya ambayo Katiba imempa yeye.

Sasa naomba kwa faida yetu akija atusaidie kwamba je, anapokasimu madaraka haya huwa yanatumika vipi hasa ukizingatia ile *enabling provision* imo ndani ya Katiba ambayo imemtaja waziri ndiye anayewajibika katika chombo hichi. Kwa hivyo, nilitaka hili akja aje atusaidie.

Jengine katika mswada huu Mhe. Spika, kuhusiana na jaduweli ambalo kidogo mimi limenitanza naomba wakati atakapokuja aje anisaidie. Jaduweli Nam. 1 kuna vifungu nikiviangalia nikivilingalisha na vifungu mbali mbali ambavyo vilikuwemo kwenye Kitabu cha Makadirio naona kuna mabadiliko na wala sitaki kupoteza muda kwa kusoma kifungu kimoja kimoja, ili na wenzangu wapate kuchangia.

Kwa hivyo, Mhe. Spika nimuombe Mhe. Waziri aangalie Vote Nam. 8 ambayo ni Ofisi ya Rais Baraza la Mapinduzi naona kuna tofatui na kile ambacho kilikuwemo humu na kile ambacho kimo kwenye jaduweli hili. Vile vile nimeona tofauti pia kwenye *Vote* 15 Ofisi ya Mwanasheria Mkuu na hii yote ni katika matumizi ya kawaida.

Sambamba na hilo nimeona tofauti na hata kama ni ndogo ni fedha za walipakodi Mhe. Spika katika *Vote* 24 Wizara ya Afya, pia nimeona tofauti katika *Vote* 25 Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati, nimeona tofauti ndogo katika *Vote* 28 Wizara ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto.

Tofauti nyengine pia katika *Vote* 29 Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo, nimeona tofatui ndogo katika Mkoa wa Mji Magharibi *Vote* 37, nimeona tofauti ndogo katika Mkoa wa Kusini Pemba *Vote* 40, nimeona tofauti katika *Vote* 41 Mkoa wa Kaskazini Pemba. Vile vile nimeona tofauti katika Wizara ya Nchi, (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora *Vote* 44, nimeona tofauti katika Mfuko Mkuu wa Serikali *Vote* 45 na nimeona tofauti katika Kamisheni ya Utumishi *Vote* 47.

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri wakati atakapokuja atusaidie, kwa sababu sisi tumepitisha vifungu hapa vya vizara au mafungu ya jumla ya wizara mbali mbali, lakini tunaona tofauti kidogo hata kama ni shilingi milioni 1,000,000/= au 2,000,000/= na sehemu nyengine ni zaidi kidogo kwa mfano Kamisheni ya Utumishi wa Umma.

Kwa hivyo, ni vyema atusaidie na iko moja sikuihoji kwa sababu tuliamua kuipunguza katika Ofisi ya Rais kwa maana Ofisi ya *Diaspora* zile shilingi milioni 40,000,000/=, lakini kwengine nako kumeondoshwa na wakati sikumbuki kama tulikata eneo jengine lolote katika Baraza hili. Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri wakati atakapokuja anisaidie.

Baada ya kusema hayo, Mhe. Spika, naomba niseme nampongeza tena Mhe. Waziri, namtakia kila la heri pamoja na watendaji wake katika kusimamia hili na ninaiunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Mhe. Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, tunakushukuru. Sasa tumsikilize Mhe. Abdalla Juma Abdalla na baadaye Mhe. Hamza Hassan Juma.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Mhe. Spika, ahsante kwa ruhusa yako naomba nitoe mawazo yangu mawili matatu katika Mswada huu wa makisio ya Bajeti.

Kwanza Mhe. Spika, mimi nilikuwa na wazo kwamba utaratibu tunaotumia hapa Barazani kwetu huwa tunapitisha Bajeti Kuu ya Serikali kwanza na tukeshapitisha ile na kuikubali baadaye ndio tunakwenda kwenye Bajeti za Sekta.

Sasa kuna kitu kinanipa tabu kidogo kwamba kule kwenye Bajeti Kuu ya Serikali nimekubali na kwa sababu nimekubali ile maana yake nimekubali sekta zote. Lakini je, itakapofika hapa nikaja kwenye Bajeti za Sekta nikakataa kupitisha Bajeti ya Wizara fulani, wakati kule mwanzo nimeshakubali na hapa nakataa.

Kwa hivyo, nilikuwa na wazo kama ni hivyo ama tupitishe Bajeti Kuu ya Serikali tu ile kubwa na halafu tukae kwa sababu sekta zote zimo mule au tuanze kupitisha Bajeti za Sekta tuzikubali kwanza na halafu ndio tukapitisha Bajeti Kuu ya Serikali, wazo hili naomba sana watu wa bajeti waliangalie. *(Makofi)*

Jambo la pili ni kifungu cha 3 cha mswada huu Mhe. Spika, naomba nikinukuu kidogo.

Kifungu cha 3 cha mswada kinaeleza hivi:-

> "Kiasi cha fedha kilichotolewa chini ya kifungu cha 2 cha sheria hii kitatumika kwa matumizi yale tu na kima kile kile tu kilichoelezwa katika jadweli ya sheria hii".

Mhe. Spika, sisi tunapitisha vifungu hapa na unatuhoji kwamba tumekubali, tunasema hapa ndio. Lakini tukeshapitisha watendaji wanafanya *reallocation* na tumejaribu sana mimi pamoja na Kamati yangu ya *PAC* kusema kwamba hii *reallocation* haina uhalali, lakini wametetea sana. Sasa kifungu hichi leo kinatoa uwazi kwamba vile tulivyokisia na kupitisha vile vifungu vya matumizi, basi vitumike vile vile, hivyo uhalali wa *reallocation* uko wapi? Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri wakati atakapokuja atueleze.

Vile vile kwenye ukurasa wa 224 kuna fungu 32 kuna fedha za kawaida shilingi bilioni 3,099,000,000/= na fedha za maendeleo hamna. Fungu 34 kuna shilingi bilioni 3,784,000,000/=, Mhe. Spika bahati mbaya sana taasisi hizi tulipokuwa tukipitisha Bajeti ya Sekta taasisi hizi mimi sikuziona zinasomeka Kikisi cha Zimamoto na Kikiso cha Valantia. Sasa mimi nitakuwa mgumu kidogo kupitisha hii kwa sababu hayakuwemo haya. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Spika, jambo jengine nilikuwa najaribu kuangalia taaswira ya bajeti yetu na hii iko ukurasa wa 229 kwenye jaduweli mwisho mwisho. Mhe. Spika, bajeti ya kawaida ni shilingi bilioni 307.7, na bajeti ya maendeleo ni 341.15 bilioni. Lakini hii bajeti ya maendeleo ukiiangalia kati ya hizo bilioni 341.15 basi mchango wa serikali ni bilioni 47.9 pekee, zilizobakia zote ama ni ruzuku au mikopo.

Mhe. Spika, bilioni 47.9 ni sawa sawa na kusema asilimia 14 tu ya bajeti ya maendeleo ndio ambayo inachangiwa na serikali. Taswira hii si nzuri inaonekana serikali yetu bado iko nyuma sana katika masuala haya ya bajeti, *at least* ingelikuwa angalau nusu kwa nunu. Nusu tunagharimia wenyewe na nusu tunaomba ruzuku ingelikuwa afadhali. Lakini 40% ni hali mbaya sana, huu ni ufukara wala si umasikini huu.

Mimi nafikiri Mhe. Waziri na wala si yeye tu pamoja na wizara zote na watendaji wote tufanye bidii ili kuondokana na taswira hii ambayo kwa kweli hairidhishi. Mimi nafikiri kwanza watendaji wetu wafanye kazi kwa bidii sana. Isiwe kazi ya kufanywa siku moja inafanywa wiki nzima, itawakuwa hatuwezi kuinua uchumi wetu.

Pili watendaji na hasa wale wanaoshughulikia mambo ya fedha, Wahasibu, washikafedha, keshia, kwa kweli wanatakiwa wawe waaminifu katika kiwango cha juu. Wasijaribu kudokoa dokoa pesa za walipa kodi tutakuwa

hatwendi pahali. Hili nilikuwa unamuomba sana Waziri wa Fedha kwamba yeye ndiye anayehusika na wizara yake na hawa wahasibu.

Mhe. Spika, pesa nyingi sana zinavuja kupitia watu hawa Wahasibu, wamefika pahali sasa hivi wanaota kibri. Maana yake sisi kama PAC tunakwenda na tunakwenda sisi baada ya kupita Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuangalia mahesabu, lakini bado tukiondoka wanasema hawa hata wafanye nini tutawaibia na hawagundui na hatugundui kweli. Nilikuwa naomba sana Mhe. Waziri awatolee macho sana wahasibu hawa pamoja na Mhasibu wake Mkuu wajitahidi kuangalia wahasibu hawadokoi pesa za watu mbona hatwendi mbele, hatari sana Mhe. Spika.

Halafu nilikuwa namuomba sana Mhe. Rais zikija taarifa za ubadhilifu Mheshimiwa achukue hatua. Zimepita kamati teule hapa zimetoa taarifa zao mpaka leo hatujaona hatua yoyote mpaka leo, hatumfundishi wala hatumuingilii katika kazi zake lakini asipochukua hatua Mhe. Raisi hawa watendaji wanaota kibri wanaendelea kuiba, wameshaona hakuna linalofanyika.

Mwisho Mhe. Spika, tunavianzio vya kodi vingi, mimi si mtaalamu lakini wataalamu wetu wanasema ikiwa vianzio vyetu vya mapato tutavisimamia vizuri, vina uwezo vya kutuzalishia milioni hamsini kwa mwezi, usimamizi utakapokuwa mzuri kwa mwezi mmoja vianzia hivi vinaweza vikatutolea bilioni 50. Sasa tukifika hapo hali hii ya 40% itaondoka. Nilikuwa naomba sana Mhe. Waziri na taasisi zake za ukushanyaji wajitahidi kusimamia masuala haya, tufike pahali tuondokane na taswira hii ambayo kwa kweli ni aibu kubwa.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja mia juu ya mia.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe kazi hii mmeshaifanya kwa hiyo kazi ilibaki ni ndogo sana. Ninawachangiaji watatu waliobaki ambao michango yao wameipa taarifa kwamba sio mirefu. Muda wetu unakaribia kwisha, nimuombe Mhe. Waziri atuongezee muda kwa kuwaomba Waheshimiwa wajumbe.

KUONGEZA MUDA WA BARAZA

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwa kuwa muda uliyombele yetu hautoshi kumaliza shughuli iliyombele yetu. Hivyo naliomba Baraza lako tukufu ikubali kuridhia kuweka kanuni kando ya muda ili tuweze kumaliza shughuli zetu za leo na hasa kumpa nafasi Waziri wa Fedha kuyajumuisha yote yaliyo mbele yake. Naomba Baraza lako tukufu liridhie tuendelee mpaka pale tutakapomaliza shughuli zetu.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

(Hoja ilitolewa Iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, nakushukuru na mimi nitoe mchango wangu katika hoja hii ya Mswada wa kuruhusu Mhe. Waziri kumruhusu kuweza kutumia fedha.

Mhe. Spika, mimi kwa mara nyengine nataka nimpongeze sana Mhe. Waziri na nadhani katika Waziri aliyeonesha mfano nadhani tokea kuanzishwa Baraza la Wawakilishi yeye ni wa mwanzo. Kwa kuweza kusikiliza michango ya wajumbe na ndani ya mwezi mmoja akaweza kusikiliza michango ya wajumbe katika suala zima la uokoaji wa fedha akaweza kulifanyia kazi. Nadhani Mheshimiwa tunakuweka katika *record* katika Waziri wa mwanzo wewe nafikiri tokea kuanzishwa Baraza hili utakuwa ni wa mwanzo.

Mhe. Spika, kwa kuokoa muda nataka niende haraka haraka katika hili Bando Kitita alotuletea Mhe. Waziri nimejaribu kuangalia baadhi ya mafungu kwa mfano kifungu 68003 ukurasa wa 226 hapa Mhe. Waziri kuna fedha ambazo zimeekwa na Mfuko wa Serikali. Lakini kuna fedha ambazo katika mchango wa wahisani hatukuziona katika Chuo cha Hoteli na Utalii.

Mhe. Spika, namuomba sana Mhe. Waziri katika jitihada zake ajaribu kuangalia Chuo kile tukiangalie katika jicho la huruma. Fedha tulizozitenga kwa kweli ni fedha chache kwa kuimarisha Chuo hichi cha Hoteli na Utalii. Nilikuwa namuomba Mhe. Waziri kwa kushirikiana na Mhe. Waziri wa Habari kwa anaeshughulikia masuala ya

utalii katika hizo mbio zao katika mafungu tuliyoyapitisha basi waweze kuhangaika ili Chuo hiki kiweze kupatia fedha vile vile.

Vile vile Mhe. Spika, katika kumsaidia tena Mhe. Waziri katika kukusanya fedha kwa uhakika bado tunamuomba na tunamsisitiza kwamba bado tunaachane na huu utaratibu wa kulipa pesa mkononi na bado tunahisi tukiweza kufanya malipo kwa njia ya benki nadhani Mhe. Waziri mfuko wake utazidi kutuna. Hili nilikuwa najaribu kutoa ushauri ili mapato yetu yaweze kuwa mazuri zaidi.

Mhe. Spika, nilikuwa nataka nizungumzie kuna hili fungu la Shirika la Umeme ambapo pia kuna ruzuku vile vile. Hivi sasa namuomba sana Mhe. Waziri hili suala ajaribu kulifanyia kazi. Sisi hivi karibuni tulikaa na watu wa ZECO baada ya kuona tunawasakama sana, tunawasema sana, viwango vya bei vimekuwa vikubwa, walitupa jawabu ambalo tunahisi Mhe. Waziri wa Fedha anaweza akatusaidia hili vile vile.

Sasa hivi ukiwaangalia wananchi wa Unguja kwa kweli wanabeba mzigo wa kuwalipia bili ya umeme mpaka na wananchi wa Pemba. Ukiangalai gharama za umeme wa Pemba kwa kweli ni kubwa, lakini gharama za matumizi kwa umeme kwa upande wa Unguja gharama hizi kwa kweli zinakuwa ni ndogo.

Mhe. Spika, nadhani tujaribu kuangalia Mhe. Waziri safari kuna fedha tulizitenga katika Mfuko Mkuu wa Serikali, tukazigawa katika maeneo mbali mbali katika mazingira, katika upande wa misitu na kupanda miti na vitu vyengine. Mimi nadhani katika Bajeti ya mwakani tujaribu kuangalia sisi tutajitahidi kumsaidia kuibua vianzio vyengine vya fedha. Lakini tujaribu kuangalia kuwapunguzia wananchi mzigo *at list* kuangalia kama kuna uwezekano kutoa ruzuku ambayo itaweza kuwapunguzia wananchi wa kisiwa cha Unguja ambao kuwa umeme pengine hawatumii wao.

Mhe. Spika, hii walifanya kama ni *over role budget* wakafanya kwamba miundombinu yote iliyokuwepo Zanzibar ya Unguja na Pemba, wakajaribu kuangalia ile gharama halafu wakatoa *percentage*. Ina maana ile *percentage* ndio tunagaiwa mafungu mafungu. Matokezeo yake wenzetu kule ile hasabu yao kwa kila *unit* walisema karibu 335 kwa upande wa Unguja karibu kama 220. Sasa hiyo unapokuja katika mahesabu inabidi tunalipa *flat rate* kwa pamoja.

Hili linachangiwa na mzigo mkubwa tunaopewa wa kulipishwa bili na TANESCO na wao kumbe wanaangalia kama tunavyofanya hapa Unguja ile miundomibinu yote iloyowahi kuwa Kigoma, Tanga, Morogoro, wapi inachanganywa pamoja halafu wanaweka kawiyo ndio inaletwa kwa Zanzibar. Utakuta kwa upande wa Zanzibar bado sisi tunalipishwa kama mteja wa kawaida. Wakati sisi Zanzibar ni mteja mkubwa. Tulikuwa tunatakiwa tupatiwe gawiwo ambalo lililokuwa ni dogo. Hiki ni kitu ambacho mpaka sasa hivi hakifanyiki na naomba hata katika vikao vyenu vya kero za Muungano hili vile vile mjaribu kulizungumza.

Mhe. Spika, jengine kuna fedha hapa zimetengwa katika yale mafunguo yaliyotengwa kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali kwa kusaidia kupanda miti na masuala ya mazingira. Mhe. Spika, mimi nataka nikwambie inawezekana Kamati yako ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuna maeneo tukaamua tusende kabisa. Kwa sababu haionekana *impact* ya Kamati kwenda katika yale maeneo. Natoa mfano:

Mhe. Spika, leo serikali fedha inatenga, fedha hizi ilikuwa zitumike kwa ajili ya madawati kuwasaidia vijana wetu kupata vikalio, fedha hizi zinakwenda kutolewa katika uhifadhi wa mazingira. Mheshimiwa kuna taasisi zinakiuka sheria za mazingira, tunakwenda kuna baadhi ya mahoteli zimejengwa makuta ndani ya Bahari. Sisi tumetoa agizo kupitia Idara ya Mazingira na hata kabla ya kwenda sisi Idara ya Mazingira walikwisha kutoa barua ya kusimamisha.

Mheshimiwa hivi juzi nimepata barua hapa nimeletewa kwamba ile amri ya Idara ya Mazingira imepuunzwa, ile amri ya Halmashauri imepuuzwa. Sasa hivi huyo muwekezaji anafanya jeuri baada ya kuambiwa yeye asimamishe jengo avunje yeye anaendelea na ujenzi.

Mhe. Spika, sasa sisi itakuwa tunapoteza muda, tunapoteza fedha za wananchi kwenda katika maeneo ambayo kuwa tunaambiwa yamevunja sheria. Huku serikali inatenga fedha nyengine kwa ajili ya kwenda kuhifadhi mazingira. Kwa hiyo tunaruhusu watu waharibu mazingira halafu tunatenga fedha kwa ajili ya kuhifadhi mazingira. Mimi nafikiri Mhe. Spika, hili litakuwa sio jambo sahihi. Lakini kama alivyosema mwenzangu kwa kuwa hii bajeti tumeshapitisha, lakini laiti kama ingelikuwa hatujapitisha mimi fungu hili la uhifadhi wa mazingira ningeomba bora

tukaliacha, watu tuwaachie tu waendelee kuharibu mazingira mpaka siku moja tukishakuzama basi itakuja kuwa ndio tulivyotaka.

Mhe. Spika, hili nilikuwa nalizungumza ili ujue kwamba Kamati zako tunapokwenda kufanya kazi yale maelekezo yake hayaheshimiwi. Bora ingelikuwa hayaheshimiwi na serikali lakini na muwekezaji, ambae katoka kwao kaja hapa anaharibu mazingira kwa makusudi. Mimi nafikiri Mhe. Spika, kwa kweli kitendo hiki hakipendezi kabisa.

Mhe. Spika, nataka nimalizie kwa kusema kwamba tulimuomba Mhe. Waziri kwamba katika suala zima la misamaha ya kodi. Katika misamaha ya kodi mimi niliwahi kuwa Mjumbe Kamati ya PAC kwa muda wa miezi kama miwili mitatu halafu baadaye nikapata nafasi nyengine sikuendelea. Moja katika eneo ambalo tunaloambiwa serikali zetu za Kiafrika pamoja na kwamba tunakaribisha uwekezaji lakini katika eneo ambalo fedha nyingi za umma zinakosa maeleezo mazuri katika suala zima la misamaha ya ko.

Mhe. Waziri nadhani pengine labda hili pengine hakujitayarisha lakini tunamuomba wakati mwengine anapokuja kutuletea taarifa zake za Wizara basi angalau tupate ile misamaha yaliyotolewa. Na sisi Mhe. Waziri hatumlazimishi lazima aandike kwenye kitabu. Wakati mwengine kuna baadhi ya mambo mengine hayatakiwi kila kitu kiwe *public*, lakini basi angalau Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tuje tupatiwe copy ya wale waliopewa ile misamaha ya kodi ili kuweza kujua kufatilia. Kuna wengine tunaambiwa wamepewa misahama ya kodi lakini wanaitumia vibaya, lakini tukipata ile orodha tutapata kujua huyu kapata msamaha wa kodi na je, ameutumia vizuri ule msamaha wake wa kodi alioupata au ameutumia pengine kwa maslahi yake binafsi au kwa watu wengine..

Mhe. Spika, nadhani kwa kumalizia kabisa kabisa nilikuwa nataka nijue tulipopeleka umeme Pemba Mhe. Waziri kipindi kile Waziri wa Nishati, alitueleza kwamba serikali kila mwezi ilikuwa ina fidia karibu milioni 800 kwa ajili ya kununua ile *IDO*. Tulitegemea baada ya kupatikana umeme Pemba ina maana zile fedha zingeliweza kuokolewa zikasaidia katika matumizi mengine. Ndio maana nilikasema ule mzigo ambao wanabebeshwa wananchi wa Unguja ambao matumizi yametumika Pemba kwa nini ule utaratibu wa serikali, zile zilizokuwa zikitumika kwenye *IDO* ile milioni 800, hatuoni kama serikali ingeliendelea na utaratibu ule, kuliko kuwabebesha mzigo wananchi wengine ambao hawakutumia bajeti ile.

Mhe. Waziri ananiangalia kwa sababu hilo suala lilipotajwa yeye alikuwa hayupo kipindi hicho, ilikuwa katika Wizara ya Nishati ya awamu ya sita wao ndio waliosema kwamba tukitia umeme Pemba tutaokoa karibu shilingi milioni 800 kwa kila mwezi. Inaonesha kuwa zile fedha hazikuokolewa. Kwa hivyo, kama hazikuokolewa basi zirudi tena ili ziende zikafidie lile pengo ili bei ya umeme kwa upande wa Unguja vile vile iweze kupungua.

Mhe. Spika, juzi wafanyabiashara walikaa wakasema kutokana na ongezeko la bei ya umeme kwa kweli wanafanya kazi katika mazingira magumu, biashara inakuwa haina faida kwa kweli inakuwa ni mzigo mkubwa. Tunashukuru kwa kumsikia Mhe. Waziri anatafuta umeme mbadala, tunamuomba aendelee na jitihada hizo, lakini bado mzigo kwa wananchi tunaomba serikali iangalie namna yoyote ya kuweza kuwapunguzia wananchi bei ya umeme.

Mhe. Spika, nakushukuru ahsante sana naunga mkono hoja.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, mimi nina maeneo mawili kwenye Mswada huu naomba niseme kwa ufupi ili nitoe nafasi kwa Mhe. Waziri kuweza kufanya majumuisho.

Mchango wangu wa mwanzo ni kifungu cha pili cha sheria hii cha Utoaji wa Shilingi bilioni 648. 9 ambazo tumeziidhinisha hapa katika mahitajio ya matumizi ya mwaka huu.

Mhe. Spika, mimi naunga mkono kwamba tuitoe hii fedha lakini katika utoaji wa fedha hii kusiwe na Wizara mama na wizara baba. Kwa maana kwamba mwisho wa mwaka tunapokwenda sisi Wajumbe wako kuna Wizara zinafikia asilimia 90 au asilimia 100 lakini kuna wizara zinafikia asilimia 60 mpaka 70. Kwa kweli mipango ya Wizara husika inakuwa haifanyiki kutokana na fedha ndogo. Mhe. Waziri kwa hivyo tutoe fedha hii kwa maana ya kuzingatia mahitajio ya kila Wizara kwa kile walichokiomba, kusiwe na upendeleo kwenye utoaji wa fedha hii.

Hoja ya pili kwenye Mswada huu Mhe. Spika, kifungu cha 8 kwamba fedha zilizokubaliwa kwa mujibu wa kifungu cha pili cha sheria hii zimeidhinishiwa kwa matumizi ya maendeleo yaliyokusudiwa.

Mhe. Spika, kila fedha ambayo tumeipanga basi iende kule kulikokusudiwa. Mwaka juzi tulitenga fedha mradi wa barabara ya Kiwani lakini hatimaye ikatolea fedha hile ikaja Unguja bila hata taarifa kwa wananchi. Sidhani kama Mhe. Waziri aliombwa na akatoa idhini. Kwa hivyo fedha itolewe kwa yale maeneo ambayo tumayaidhinisha vyengivyo kuwa sababu za msingi ambazo Waziri Sheria imeruhusu kufanya *real question* kwenye Mswada huu.

Mhe. Spika, naunga mkono hoja.

Mhe. Asha Bakari Makame: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi sitokuwa na mengi kwa sababu mengi yameshazungumzwa, lakini nimuombe Mhe. Waziri kwamba ahakikishe tunasaidia sana Wizara, fedha ambazo zimepangiwa zifike kwa wakati. Hii nakuombe dua wewe na watendaji wako ili muwe na uwezo wa kuzitafuta fedha hizi, ili mambo yote yaende sambamba kwa mujibu wa bajeti tulivyoipanga. Hilo moja.

La pili nitamuomba Mhe. Waziri kuna hii Idara ya Bajeti, tutakuwa wizi wa fadhila kama Idara hii hatukuipongeza, kwa sababu ni Idara ambayo ndio inajipinda migongo, tunakuwa nao wakati wa kupitisha bajeti hapa. Mimi sina uhakika nisiseme neno nililokuwa sina uhakika nalo, utanisaidia Mhe. Waziri. Naomba sana uwatupie jicho la huruma hawa kama sijui wanalipwa posho au na wao mishahara yao imeangaliwa kwa jicho la huruma, hapo siwezi kujua. Nakuomba sana kwa sababu ni watu ambao kwa kweli wanastahiki sifa.

Kwa hivyo, baada ya kusama hayo nikutakie kila la kheria katika bajeti hii Mwenyezi Mungu akupe uwezo pamoja na watendaji wako ili tupitishe bajeti hii kama tulivyokwisha kuipitisha, tuweze kwenda sambamba na mambo ambayo tumeyaomba. Nakutakia kila la kheri. Naunga mkono.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi ya mwisho nikiwa kitinda mimba kutoa mchango katika bajeti yetu hii ambayo leo tunaipitisha kwa mwaka huu vile vile.

Mhe. Spika, mimi nilikuwa naomba Mhe. Waziri anisaidie tu kidogo katika haya mahesabu ya kwenye jaduweli tulilonalo hapa Nam. 1 tumeweza kuona zile fedha ambazo tumeweza kuziondoa kule kwenye milioni 884, tukaweka milioni 844. Zile pesa ziliondoka kule tukaja tukaziona katika Mfuko Mkuu wa Hazina. Lakini kuna pesa ambazo Mhe. Waziri alituletea kabrasha yake hapa hizi bilioni 17, kuna wizara ambazo zilikuwa zimepunguziwa. Ndio maana pale tulikuwa tunamuomba Mhe. Waziri atusaidie ule mtiririko wa mawizara ili tuweze kuliona hili. Kwa bahati mbaya alileta hisi hesabati kwa jumla wake. Sasa hivi fedha zilizochukuliwa kwa ujumla bilioni 17 zinaondoka katika zile wizara husika, zinakuja katika mfuko upi, mbona katika huu Mfuko Mkuu wa Hazina hazipo bado zimeendelea kubakia pale pale katika mifuko ile ya Mawizara.

Mhe. Spika, sasa tutakapokuja katika bajeti mwaka unaofuata, huyu Waziri tutakapokuja kumuuliza maswali katika tafauti hii ya fedha si itakuwa tatizo kwa upande wao. Nilikuwa naomba ufafanuzi wa jambo hilo tu la kwanza.
Jambo la pili naomba hizi fedha za OC wanazozisimamia Makatibu Wakuu wizara au serikali inatoa kuwakabidhi Makatibu Wakuu katika Mawizara yao. Lakini Makatibu Wakuu wahawatimizi yale malengo ambayo yalikuwa yamepengwa kwa mujibu wa yale matumizi ambayo wale walengwa walikuwa wanayahitaji. Ningelimuomba Mhe. Waziri hili aliangalie na alitengenezee utaratibu kwamba kadiri ya maombi yalivyokuwa yameletwa ndivyo vile vile Makatibu Wakuu wasimamie matumizi ya hizi OC kwa malengo ya kuendeleza shughuli zetu hizi.

Ahsante sana Mhe. Spika, naunga mkono hoja.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, kwanza nichukue nafsa hii kuwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. Lakini ninadhani kwamba watakubaliana na mimi kwamba leo ilikuwa ni marathon, toka tumeanza kujadili hapa mpaka hivi sasa inakaribia kuhitimisha sijaondoka, sijatetereka, nipo ninashirikiana na wao kutekeleza majukumu ya wananchi.

Nipo mbele yao kwa sababu ya mashirikiano na mshikamano walionipa na mimi ninataka niwaahidi nitafanya kazi pamoja nao kwa faida ya wananchi wetu. (*Makofi*).

Sasa Mhe. Spika, ninataka niwataje wale ambao waliochangia na wala hii haina maana kwamba wengine hawakupenda kuchangia ni kwa sababu tu ya muda, lakini ninaamini na wao wengine wangelipenda kuchangia kwa faida ya wananchi wetu.

Waliochangia nao ni:-

1. Mhe. Ismail Jussa Ladhu
2. Mhe. Abdalla Juma Abdalla
3. Mhe. Hamza Hassan Juma
4. Mhe. Hija Hassan Hija
5. Mhe. Asha Bakari Makame
6. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa

Nimepokea michango yao.

Lakini kabla sijaenda kifungu kwa kifungu kwa mujibu wa michango yao naomba niseme mambo mawili matatu ya ujumla.

Mhe. Spika, bajeti tuliyopitisha bajeti ya taifa, ile inajenga misingi mikuu ya bajeti yetu. Inaeleza tutatumia vipi, kiwango gani, kiasi gani kitakwenda katika recurrent, kwa maana ya bajeti ya kawaida na kiasi gani kitakwenda katika bajeti ya maendeleo pamoja na kutoa vipa umbele. Inaweka misingi mikuu na ndio kwa maana, mimi bajeti ile mara nyingi ninaisoma kwa muda wa masaa mawili.

Lakini bajeti za sekta moja moja zinaweza zikasomwa hata zaidi ya masaa mawili. Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi amesoma kwa masaa mawili na dakika 20, ameizidi ile ya taifa kwa sababu yeye ana uwezo wa kuichanganua ile bajeti ya sekta yote akainyumburua. Lengo ni kuonesha ile misingi mikuu niliyoweka katika bajeti ya taifa, yeye sasa anaipeleka katika sekta kwa mujibu wa malengo ya kila kifungu na kila kipengele.

Kwa hivyo misingi tuliyoiweka lazima isomwe mwanzo, bajeti ya taifa lazima isomwe mwanzo, halafu zinafuata bajeti za sekta. Munaweza mukapunguza bajeti ya sekta. Tulifanya tumepunguza milioni arobaini bajeti ya Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, lakini hamuwezi mukaizidishia bajeti ya sekta ya baada ya kupitisha bajeti ya taifa. Lazima tucheze na ile ile bajeti ya taifa ndio msingi, tumepanga tutumie bilioni mia sita basi tucheze na bilioni mia sita.

Ndio tulichokifanya na hilo linawezekana. Tukitaka bajeti yetu ya taifa kama ni ndogo, pale pale tunapoizungumzia bajeti ya taifa, tuseme hii ni bajeti ndogo na tuoneshe vyanzo vyake ili tuweze kutafuta fedha za ziada.

Nimeanza na hilo Mhe. Spika, kwa sababu ninataka nioneshe mkazo juu ya huu Mswada. Mswada huu una *cement*, vile vifungu ambavyo tulivyovipitisha, lakini wengine walionesha wasi wasi wakasema kwamba hesabu kidogo hapa kuna namba zimekosewa kosewa tofauti na zile. Ni kweli kwa sababu kule baada ya kuzijumlisha sasa kwa undani kabisa, unajumuisha vile vifungu kimoja kimoja vile vifungu vidogo vidogo unavijumlisha, ndio imeonekana vyengine kidogo vimepungua.

Lakini kule kumbukeni Waheshimiwa, kule tulikuwa tunajadili, hapa tunapitisha mswada wa sheria. Hapa tukishapitisha hizo ndizo tutakazozitumia, kwa sababu sasa tumeshampa Waziri mwenye dhamana ya fedha atumie vifungu hivi. Kule tulikuwa tunajadili. Kwa hivyo wataalamu niliwataka baada ya kuona hayo marekebisho kupitia kwenye kamati mbali mbali, nikawapa kazi kwamba sasa wapitie kifungu kimoja kimoja kwa kwa kujumuisha taratibu ndizo hivi ambavyo Mhe. Jussa na Waheshimiwa wengine wameona kwamba kuna figure zenye digital moja, mbili lakini halitutoi kwenye lengo kuu la bajeti yetu ile taifa. Hilo ndio msingi katika bajeti. Tukishakubaliana hapo Mhe. Spika, sasa naomba niende kidogo katika vile vifungu ambavyo vilivyochangiwa na Wajumbe haraka haraka.

Kwanza Mhe. Jussa alizungumzia maudhui ya Mswada huu. Mimi ninataka nikubaliane na yeye, maudhui ya mswada huu ni kutoa idhini, sasa Baraza hili linatoa idhini kwa Waziri mwenye dhamana ya fedha kwamba pesa hizi utumie kwa mujibu wa vifungu hivi na utumie kiwango hiki.

Mimi ninakubaliana naye kabisa na cha msingi hapa ni kusimamia. Waziri wa Fedha amepewa mamlaka ya kuhaulisha lakini mimi mamlaka haya siyafanyi peke yangu, ninayafanya baada ya kupokea frame ya uhaulisho

kutoka kwa Waziri wa sekta. Nitawaomba sana mawaziri wenzangu wa sekta wanaosimamia, huu uhaulisho basi uendane na ile mantiki hasa ya Baraza iliyokusudia. (*Makofi*).

Mhe. Spika, kwa sababu mimi sasa kuja pale nikamkatalia waziri mwenzangu kwamba sihaulishi, haitoleta uhusiano mzuri katika kazi lakini ikiwajibika itabidi nifanye. Sasa tusiende huko ninawaomba sana mawaziri wenzangu aangalieni vifungu vilivyohaulishwa, kile kinachotolewa pesa kuleta hapa hakina kazi tena. Waziri hoji upate maelezo na wewe ndio unaoanguka unaotia saini, ukishanitilia saini mimi ninajua kwamba Waziri kakubali kwa misingi hii. (*Makofi*).

Kwa hivyo hilo Mhe. Spika, ninakubaliana na wewe sana Mhe. Jussa lakini vile vile umetoa ushauri kwamba sheria ya fedha tuiangalie. Bado tunaitumia na bado inampa uwezo Waziri wa Fedha lakini kuna haja na msingi wa kuiangalia. Kama nilivyokubali pale awali, ninakubali tena kwamba sheria hii tutaiangalia na ninadhani wiki ijayo tutakaa na Katibu Mkuu wangu na watendaji wangu wengine tuangalie jinsi ya kuweza kui-*first track* hii sheria yetu ya fedha, kwa sababu tukiangalia hii na tukiirekebisha mapema iwezekanavyo kuna uwezekano mkubwa haya matatizo mengi na upotevu mwingi ukapungua. Kwa hivyo tutaangalia hilo na tuone jinsi ya kuweza kui-*first track*.

Umezungumza kitu ambacho amekizungumza vile vile alichokizungumza Mhe. Asha Bakari Makame, Idara ya Bajeti hii isimamie kwa karibu zaidi hivi vifungu na utumiaji basi uende sambamba na matakwa ya kifungu. Hili nimelipokea na tutajitahidi sana kulifanyia kazi.

Umetaka nikupe ufafanuzi haya madaraka niliyosema pale ninaweza nikayakasimu. Kiutaratibu hasa hili halijawahi kutokea lakini kwa mujibu wa sheria unatakiwa uweke full back position. Waziri ni binadamu unaweza ukawa hupo, madaraka yale kwa utekelezaji wa bajeti unamuachia Katibu Mkuu.

Lakini kuna uwezekano vile vile Katibu Mkuu akawa hayupo yupo Kaimu, ndiye nikasema kwamba afisa. Lakini kimantiki hasa nimejaribu kuwauliza wenzangu iliwahi kutokea hii, bahati nzuri Mwanasheria yupo kipindi kirefu sana Zanzibar, amewahi kuwa Katibu Mkuu wa Sheria na Katiba, sasa ni Mwanasheria Mkuu, amewahi kukaa pale mwanasheria muda mrefu, akaniambia kikawaida haijawahi kutokea hii lakini as full back position, kama ni sheria lazima mukiweke hiki kifungu ili incase ikitokea Waziri ni binadamu, kapindwa na tumbo hapo, ukasikia Waziri hayupo tena. Sasa anayekaimu pale madaraka haya ya kuendesha shughuli anatakiwa Katibu Mkuu azisimamie hizi pesa. Kwa hivyo ndio mantiki yake.

Ninadhani umeuliza ni tofauti inayotokana na majadweli yametokana na nini, nimeshaeleza. Hizi ni statistics area na sasa tumeshazi-cement kwa kuweka hii sheria.

Mhe. Abdala Juma ninadhani suala lake la mwanzo nimelitolea ufafanuzi wa ujumla kuhusiana na bajeti kuu na bajeti za sekta. Ninakubali kuna makosa hapa kidogo ya printing kwamba sio Kikoso ni Kikosi. Kwa hivyo naomba hiyo turekebishe.

Umeeleza concern nzuri sana. Hata mimi ninataka nikwambie withini the government machinery, ndani ya serikali kwa maana ya Baraza la Mapinduzi, concern yetu kwamba kupeleka pesa nyingi zaidi katika maendeleo, kwa maana ya zetu wenyewe.

Mchango wa serikali kwa pesa za maendeleo uwe ni mkubwa zaidi. Hii asilimia 14 tunajikongoja. Mwaka jana hatukuwa na asilimia 14, tunajikongoja. Mimi ninaamini kwamba ile spirit ambayo mumeonesha mwaka huu Waheshimiwa Wawakilishi, kuonesha *concern* yenu katika vifungu vya development current, tutaweza mwaka kesho kupeleka fedha zile katika development. Mimi nitawaambia sana watendaji wangu tuiangalie hii ili mwaka kesho tuwe na mchango mkubwa zaidi kwenye development.

Wahasibu watolewe macho. Mimi nitawatolea macho nitawaangalia vizuri zaidi ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi. Halafu siwatolei macho kwa maana ya kuwanyofoa, aah! tuwatizame.

Mhe. Abdalla alizungumzia Mhe. Rais kama anapata taarifa za ubadhirifu basi achukue hatua. Mimi ninadhani Mhe. Rais wetu ni msikivu na huwa anachukua hatua pale anapoona kwamba imethibiti. Maana yake time nyengine ndugu zanguni unaweza ukaja ukasikia rumour tu huko, kumbe ni matatizo ya watu tu basi. Lakini ikithibiti mimi

ninaamini Rais atachukua hatua. Akishakupata information ambayo ipo authentic kwamba huyu mtendaji wangu au waziri wangu huyu amesababisha au amefanya tatizo kadha wa kadha. Wazanzibari wapo wengi na Rais hafungiki na sisi tu, anaweza akatafuta Mzanzibari mwengine yeyote akampa hilo jukumu akafanya kazi.

Ninashukuru umesema kwamba vianzio vyetu vikisimamiwa basi mapato tunaweza tukapata mengi zaidi. Mimi ninasema tutavisimamia na kama ulivyosema kwa ushirikiano na Baraza hili Mhe. Spika, ninaamini tutapata mapato mengi zaidi.

Mhe. Hamza umezungumzia Chuo cha Utalii kitazamwe, fedha ziliwekewa ni chache. Mimi nikubaliane na wewe kwamba tutakuwa tukikiangalia. Lakini vile vile ninataka nikwambie kwamba kuna fedha za kuwafundisha, kutoa mafunzo kwa ajili ya watendaji hawa zipo aidha zitakuwa zipo chini ya Wizara ya Elimu au Wizara ya Habari. Nitaziangalia ili niweze kukupa taarifa kamili hasa juu ya chuo hiki. Kwa kweli chuo hiki tukikiimarisha vizuri zaidi kitasaidia hata sekta ya utalii.

Umezungumzia *ZECO* na bei ya umeme. Maelezo nimeyapata, Waziri wa Nishati hayupo hapa bado hajarudi safari. Lakini tutasaidiana katika hili. Umesema misamaha inayotolewa basi tupate nakala Waheshimiwa Wajumbe. Si baya. Tunatayarisha nakala kwa mujibu wa utaratibu kwa sababu hao waliomba na waliiomba ni serikali na sisi tuliwapa, basi hawa hawatoweza kukataa kama tuliwapa hiyo misamaha. Tutajiandaa hili ili tuweze kutoa basi muweze kuona Omar Yussuf Mzee ameingiza gari amepata msamaha wa kodi hii, kila mmoja mutamuona ili mujue kwamba waliopata misamahaka hawa. (*Makofi*).

Ulizungumzia suala la kwamba tulizungumza kuwa tutakapopeleka umeme Pemba tutaokoa milioni mia nane. Ni kweli kwa sababu ya yale mafuta ambayo yaliyokuwa yakitumika kwa ajili ya jenereta. Hivi sasa umeme unaotoka Tanga kwenda Pemba pale, ukiwasikiliza wenyewe watu wa nishati wanakwambia mkataba wao ni twenty megawatts.

Ile cable inachukua twenty megawatts lakini wao wanachokichukua ninadhani ni two six and eight megawatts. Kwa hivyo tumeweza kuokoa kwa maana ya yale mafuta. Sasa hivi hatununui tena mafuta kwa ajili ya majenereta. Sasa nitawasikiliza wenzangu ule uokozi uko wapi sasa na mimi wanisaidie kwa sababu hii ni sekta.

Mhe. Hija umetaka wizara zote zipatiwa fedha kulingana na mahitaji ya kila wizara. Hata mimi na mimi ninakubaliana na wewe. Lile suala la kwamba huyu amepewa asilimia 40 na huyu 100 haileti sura nzuri. Lakini fedha ni lazima zitolewe kwa mujibu wa *expenditures*. Jinsi utakavyotumia ndivyo utakavyopewa pesa. Sitaki nitaje kuja wizara hapa tuliitengea bajeti kwa ajili ya shughuli fulani, mpaka tunamaliza hawakuitekeleza hiyo shughuli.

Sasa huwezi kusema unawapelekea tu wakati wao wenyewe hawaoneshi iniatitives ya kuitekeleza hiyo shughuli. Kwa hivyo mimi ninataka niwaombe mawaziri kama ni wasimamizi, tusimamie hizi shughuli ili ziweze kutekelezwa na mutatu-push sisi kukuleteeni pesa ili muweze kutekeleza majukumu yenu.

Umesema vile vile pesa iende ilikokusudiwa kulingana na tulivyojipangia. Wazo ni zuri na ndio utaratibu na ndio sheria hii ndio inavyosema. Kwa hivyo hilo tumelipokea na tutalifanyia kazi.

Mhe. Asha Bajari umesema kwamba fedha hizi wizara ziwafikie kwa wakati. Mimi ninataka nikuhakikishieni nitatekeleza hilo, kwa sababu kila mwezi tuna *steering committee*, kuna Makatibu Wakuu wanaoshiriki wa mawizara makubwa makubwa hapa, karibu wanane ni wajumbe wa *steering committee*. Kwa sababu first charge ni mishahara, mishahara haina compromise, hiyo ndio *first charge*. Tukimaliza first charge tunakwenda contribution yetu katika development, halafu tunaangalia OC, tunagawana kile ambacho kilichobakia.

Sasa Katibu Mkuu anapokuja na hoja zake akajenga hoja zake katika *steering committee*, mara nyingi huwa anapewa pesa ili akatekeleze majukumu yake. Lakini anaposhindwa kujenga hoja, pale na tena Makatibu Wakuu wengine bahati mbaya kama kitu hawakitaki basi hata kukisogeza hata kwenye steering committee hakisogei.

Mimi ninawaomba Mawaziri wenzangu tusimamie, kila sekta tuliyoambiwa tuifanyie kazi, kila points tuliyoambiwa tuifanyie kazi basi tuhakikishe Makatibu Wakuu wetu wanakipeleka kutatufutiwa fedha ili tuweze kutekeleza.

Mhe. Asha Bakari alimalizia kwamba mambo yote yaende kwa mujibu wa mipango. Bila ya kutekeleza mambo yetu kwa mujibu wa mipango yetu, utakuwa umetekeleza kinyume cha bajeti, itakuwa ni kinyume cha sheria zetu. Hapa tunapitisha bajeti lakini with the *association* na mpango, kwa hivyo hapa utekelezaji wetu nao vile vile uende kwa mujibu wa mipango yetu. Hili nitawaomba sana ndugu zangu Makatibu Wakuu walisimamie ili Waheshimiwa Wawakilishi waone kwamba tumefanikisha yale malengo na matakwa ya wananchi wetu.

Umepongeza Idara yangu ya Bajeti na Kamishna yupo juu kule anakusikia, anakushukuru. Kamishna amenitupia mimi ameniambia bwana nitolee shukurani zangu. Umetuomba tuwaangalie. Kwa kweli wanafanya kazi kubwa sana. Bajeti zote za wizara zikipitisha hapa wapo wataalamu wa bajeti wanakuwepo juu pale, wanatusikiliza, hawaja miss wizara hata moja, wanajipanga tu, leo mtaalamu huyu, kesho mtaalamu huyu.

Mimi ninadhani bahati nzuri Katibu Mkuu yupo pale na Katibu Mtendaji ninamuona yupo na yeye, kwa hivyo wataiangalia hii idara ili waweze kutekeleza majukumu yao vizuri.

Mhe. Mahmoud Mussa umetaka nikutolee ufafanuzi. Hizi seven point one six six billion, mbona sijazinyofoa. Sikuweza kuzinyofoa kwa sababu wakati Mhe. Rais ananipa agiza la meli utakumbuka kwamba baadhi ya wizara zilikuwa zimeshapitishwa, kwa hivyo sikuweza kuzinyofoa. Lakini kwa mujibu wa uwezo niliopewa chini ya sheria ya fedha nitazihaulisha. (*Makofi*).

Kwa hivyo nimeziacha kama zilivyo na kile kiambatisho ambacho nimeshamkabidhi Katibu, tutawaandikia Makatibu Wakuu wote wajue kwamba ni kiasi gani tunatoa katika wizara yake, tutazihaulisha. Kwa hivyo hili usiwe na wasi wasi ni maelekezo ya Mhe. Rais wa nchi yetu tutalifanyia kazi.

Umetaka Makatibu Wakuu wasimamie vizuri OC zao. Mimi nitafikisha agizo hilo, kila watakapokuwa wanakaa kwenye steering committee, nitahakikisha ninampa maagizo Katibu Mkuu wangu akumbushie na kila watakapokuwa wanakaa kwenye kamati ya Makatibu Wakuu, nitahakikisha Katibu Mkuu wangu ninampa maagizo wakumbushie kusimamia OC.

Lakini siku hizi kuna bango kitita linasimamiwa na mwenyewe Mhe. Rais chini ya Wasaidizi wake wawili; Makamu wa Kwanza na Makamu wa Pili wa Rais. Hilo huchezei, maana Rais anaiona fedha uliyoipata, halafu anakuona umeitumia vipi na wanakuuliza na wanatuuliza kweli, wanamuuliza Waziri na wanamuuliza Katibu Mkuu na watendaji, wote watatu wanakuwepo hao. Kwa hivyo kama Waziri kama Katibu Mkuu hataki ajira hii shauri yake. Lakini mimi nitamuomba sana Katibu Mkuu wangu awe anawakumbusha.

Mhe. Spika, nimejitahidi kutoa ufafanuzi kwa kadri ya uwezo wangu na masuala niliyoulizwa. Baada ya maelezo hayo ninamalizia kwa kuwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe kwa kunivumilia, maana yake leo kutwa ilikuwa ni ya kwangu mimi.

Pia ninakushukuru wewe Mhe. Spika, kwa kuniruhusu kwamba leo kutwa jukwaa hili nilichezee mimi tu ninakushukuru sana.

Baada ya maelezo hayo, sasa naomba kutoa hoja. Ahsante sana Mhe. Spika. (*Makofi*).

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

KAMATI YA KUTUNGA SHERIA

Mswada wa Sheria ya Kuidhinisha Makisio na Matumizi ya Serikali

(Kusomwa kwa Mara ya Pili)

Kifungu cha Kwanza	Jina fupi
Kifungu cha Pili	Utoaji wa Shilingi Bilioni mia sita na arobaini na nane, mia tisa na arobaini na tatu milioni, mia saba na tisini na nane elfu kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali
Kifungu cha Tatu	Makisio ya fedha zilizokubalika
Kifungu cha Nne	Uwezo wa Waziri kukopa pamoja na marekebisho yake
Kifungu cha Tano	Uwezo wa Waziri wa maombi ya ziada
Kifungu cha Sita	Marejesho ya Mikopo na riba
Kifungu cha Saba	Kukubaliwa kwa mipango ya maendeleo
Kifungu cha Nana	Kukubaliwa kwa fedha zilizopitishwa kwa matumizi ya maendeleo

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, ilivyokuwa Kamati ya Kutunga Sheria umeupitia Mswada wangu kifungu kwa kifungu na kuukubali pamoja na marekebisho yake. Sasa naliomba Baraza lako tukufu liukubali. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, naafiki**.**

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mswada wa Sheria ya Kuidhinisha Makisio na Matumizi ya Serikali

(Kusomwa kwa Mara ya Tatu)

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, naomba kutoa hoja kuwa Mswada wa sheria ya Kuidhinisha Makisio na Matumizi ya Serikali usomwe kwa mara ya tatu.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, naafiki**.**

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, sasa naomba kuwahoji wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

TAARIFA YA SPIKA

Mhe. Spika: Waheshiwa Wajumbe, nami nichukue nafasi kuwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wote, mumekuwa watulivu kwa muda wote tangu saa 3:00 asubuhi mpaka hivi sasa kufikia tamati kwa shughuli zetu za leo na kwa mashirikiano makubwa.

Kwa hivyo, kabla ya kuahirisha kikao naomba nitoe matangazo manne.

Waheshimiwa Wajumbe, kazi tuliyofanya ni kubwa tena ni wajibu wetu tufike pahala tuwe tunapongezana na hasa kwa sababu ya Mwezi huu Mtukufu wa Ramadhani, basi tupongezani kwa utaratibu ambao kwa kawaida jioni huwa tunaufanya katika maeneo mbali mbali. Sasa Ofisi ya Baraza la Wawakilishi inategemea kesho penye majaaliwa kutoa futari kwa Waheshimiwa Wajumbe pamoja na watumishi wetu na wengine ambao wataalikwa pale *Zanzibar Beach Resort*. *(Makofi)*

Tulitegemea kwamba shughuli hiyo ingefanyika hapa katika eneo letu, lakini tulishauriwa kwamba kwa kuwa mtakuwa na vitu vya maji maji vingi namna ya usafirishaji kidogo inaweza kuleta matatizo na isifanikishe vizuri futari yetu hiyo.

Kwa hivyo, niwaombe Waheshimiwa Wajumbe, kesho jioni saa 12:15 sote tuhudhurie pale *Zanzibar Beach Resort*, ili baada ya kazi nzuri mlioifanya basi tumalize kwa kubadilishana mawazo pale na kupata chochote ambacho kilichotayarishwa na nyinyi Waheshimiwa Wajumbe na ofisi yetu. Naomba sana Waheshimiwa Wajumbe, tuhudhurie futari hiyo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe, hizi futari ziko nyingi, pia nimeombwa nitoe taarifa na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano na ilielezwa hapa kwamba miundo tayari anayo Mhe. Waziri na mbinu pia anatafuta na Mhe. Mwanasheria Mkuu anakumbuka. Kwa hiyo, na wao wanatayarisha futari kesho pale *Bwawani Hotel* na Waheshimiwa Wajumbe nyote mnaalikwa. *(Makofi)*

Sasa hii haina maana kwamba tukitoka hapa twende kule hapana, isipokuwa tutatafuta namna ya kujigawa, lakini ni vizuri tukashiriki katika shughuli zetu hizi mbili. Lakini mimi ya kwangu nasema ni ya kwenu nyote, pale *Bwawani Hotel*.

Taarifa nyengine ambayo hii nimeombwa na Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo, kwamba tarehe 26/08/2012 mnamo saa 12:00 za asubuhi yale mazoezi ya kawaida yatakuwepo katika viwanja vya Baraza na Waheshimiwa Wajumbe nyote mnaombwa muhudhurie mazoezi hayo pamoja na mimi naalikwa. Kwa hiyo, nikuombeni sana muhudhurie katika mazoezi hayo tarehe 26/08/2012 saa 12:00 asubuhi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe, tunaelewa kwamba kila mwaka tunao utaratibu wa kuwatembelea wenzetu wa Arusha kwa ajili ya michezo. Sasa nimeombwa na Mwenyekiti wa Bazara la Wawakilishi *Sport Club*, niwatangazie Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ile ya kuandaa masuala ya michezo wenyewe wanajitambua, kwamba wakutane kesho baada ya kuahirisha shughuli zetu za Baraza.

Wajumbe hao wakutane katika ukumbi wa juu pale, kwa ajili ya kuandaa utaratibu wa ziara zetu za kawaida za michezo, kesho maara baada ya kumaliza shughuli zetu na kuahirisha Mkutano wetu wa Nane. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe, baada ya hayo basi nichukue nafasi tena kuwashukuru kwa utulivu wenu na mashirikiano makubwa. Sasa naomba nichukue nafasi hii kuakhirisha kikao hichi hadi kesho tarehe 10/08/2012 saa 3:00 za asubuhi.

(Saa 11:10 za jioni Baraza liliakhirishwa hadi
tarehe 10/08/2012 saa 3:00 asubuhi)